# Nipashe

Jumatatu Aprili 15, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579892

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper




## Walipana posho za safari kila siku, mwaka mzima

UKURASA 2




UKURASA 13

# Spika Ndugai 'ampeleka' Prof. Assad kwa JPM

UKURASA 2



## Mama aua wanawe 6, naye auawa na wananchi

UKURASA 8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akikagua wachezaji wa Timu ya Taifa ya Vijana, Serengeti Boys kabla ya kuanza mechi ya michuano ya Afcon U-17 dhidi ya Nigeria katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam jana. Habari Uk. 32. **PICHA: OWM**

# UDSM yadahili mara tano ya uwezo wake

**YAELEZWA** ni hatari kwa ubora wa elimu, maendeleo ya taifa... *Endelea ukurasa wa 2*






**MICHEZO** STARS KUJIPIMA NGUVU NA MISRI, CAMEROON UK. 31

MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA

## UDSM yadahili mara tano ya uwezo wake

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

CHUO Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimebainika kudahili wanafunzi kwa zaidi ya mara tano ya uwezo wake na kuibua hofu ya ubora wa elimu kinayotoa kwa wahitimu wake.

Changamoto hiyo imeibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, katika ripoti yake ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/18, iliyowasilishwa bungeni jijini Dodoma Jumatano.

Katika ripoti yake kuhusu ukaguzi wa mashirika ya umma, CAG Assad anabainisha kuwa mnamo mwaka 2016/17, UDSM ilidahili wanafunzi kwa zaidi ya asilimia 560 ikilinganishwa na mpango wake.

"Hii ina maana kuwa idadi ya wanafunzi waliodahiliwa ilipita uwezo wa chuo hicho. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa udahili haukuwa umetolewa taarifa kwa kiwango ambacho kila kitivo kilielewa idadi ya wanafunzi waliotakiwa kudahiliwa," anabainisha.

"Majadiliano na baadhi ya maofisa yalionyesha kuwa kiwango cha juu cha udahili huo hakikuwa na uwiano na rasilimali nyingine za chuo kama vile rasilimali watu na

INAENDELEA UK. 8

# Ndugai 'ampeleka' Prof. Assad kwa JPM

**Na Gwamaka Alipipi**

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amemshauri Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, kwenda kwa Rais John Magufuli na kujieleza kuwa alikosea kuliita Bunge ni dhaifu.

Amesema hiyo ni mojawapo ya njia ya kumaliza mgogoro uliopo sasa kati yake (Prof. Assad) na Bunge, baada ya azimio kutolewa la kutokufanya naye kazi.

Spika Ndugai alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali yaliyojitokeza hivi karibuni baada ya CAG Prof. Assad kuwasilisha ripoti yake Jumatano jijini Dodoma, ambapo hata hivyo, wenyeviti wa kamati za Bunge hawakuhudhuria.

**AMSHAURI KWENDA KWA RAIS**

"Zipo njia za kumaliza mambo kama haya, mojawapo ni Prof. Assad aende kwa Rais akajieleze na kusema kuwa nimejipima nikaona nilikosea," alisema Ndugai.

Alisema kwa mujibu wa katiba ya nchi, Rais ni sehemu ya Bunge, hivyo kauli iliyotolewa na CAG Prof. Assad kuwa Bunge ni dhaifu inamaanisha amemtukana hadi Rais.

INAENDELEA UK. 8



Muuza matunda aina ya mafenesi akichambua tunda tayari kwa kuwekwa katika chupa maalum kwa ajili ya kuwauzia wateja wake katika Mtaa wa Samora jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**






# Walipana posho za safari kila siku, mwaka mzima

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amebaini matumizi mabaya ya fedha kwenye Tume ya Huduma za Walimu, ikiwa ni pamoja na wafanyakazi wake kulipwa posho za kuwa safarini kila siku kwa mwaka mzima.

Katika ripoti yake ya ukaguzi ya mwaka 2017/18 iliyowasilishwa bungeni na serikali Jumatano iliyopita, CAG Assad anasema amebaini wafanyakazi mbalimbali wa tume hiyo walilipwa posho inayofikia Sh. milioni 721.05 kwa lengo la kutekeleza shughuli za ofisi.

Anabainisha kuwa tume hiyo imewalipa wafanyakazi posho ya safari kwa siku 324, posho ya kazi za ziada kwa siku 365 na posho za vikao kwa siku 127.

"Hii si kwamba inaashiria matumizi yenye shaka, bali kutokuwa na uhakika kama wafanyakazi walikuwa nje ya kituo cha kazi kwa mwaka mzima, wakati rejista ya mahudhurio imeonyesha wafanyakazi hao walikuwapo ofisini kwa kipindi hicho.

"Ni mtazamo wangu kwamba, upungufu huu umesababishwa na udhibiti wa ndani hafifu juu ya kulinda na kutumia fedha za umma, ambapo kama hatua hazitachukuliwa, yanaweza kuchochea matumizi mabaya ya fedha za umma.

"Kwa sababu ya udhaifu ulioibuliwa hapo juu, nashauri menejimenti ya Tume ya Huduma za Walimu kuanzisha mifumo imara ya udhibiti wa ndani ikiwamo huduma za ukaguzi wa ndani, yenye vitendea kazi vya kutosha na mgawanyo imara wa majukumu ambao unaweza kuwa na umuhimu katika kupunguza vihatarishi vilivyotambuliwa.

"Nashauri zaidi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuchunguza kwa ukaribu suala hili, na itakapohitimishwa wahusika watapaswa kuwajibika," Prof. Assad anatahadharisha katika ripoti yake hiyo.

CAG Assad pia anabainisha kuwa ukaguzi wake ulibaini dosari kwenye matumizi ya Sh. bilioni 4.665 yaliyofanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) kwenda kampuni binafsi za kisheria bila kufuata makubaliano ya mkataba na upungufu katika usimamizi wa ankra za matibabu nje ya nchi Sh. bilioni 7.013.

Katika ripoti hiyo, CAG Assad anabainisha utata wa miamala iliyofanywa na Katibu Tawala wa Wilaya ya Tarime Sh. milioni 514, ongezeko la gharama za kukodi magari katika balozi za Tanzania zilizoko Moroni na Brasilia Sh. milioni 87.461, malipo yasiyo na vithibitisho Sh. bilioni 4.369, Kodi ya Zuio ambayo haijadaiwa Sh. milioni 722.173, malipo yasiyokuwa na risiti za kielektroniki (EFD) Sh. bilioni 1.432.

HABARI KITAIFA

# Biashara vyuma chakavu ruksa

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imeruhusu biashara ya taka hatarishi ikiwamo ya vyuma chakavu iliyokuwa imepigwa marufuku kusubiri mchakato wa kanuni.

Aidha, walioruhusiwa kuendelea na biashara hiyo ni wale wenye leseni na wameshakaguliwa na Baraza la Usimamizi wa Mazingira Tanzania (Nemc), na kupewa cheti cha ukaguzi na kwamba kanuni mya zitakavyoanza kazi watatakiwa kufuata utaratibu mpya.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), January Makamba, alitangaza uamuzi huo jana, wakati wa mkutano wa wadau wa taka hatarishi baada ya kusikiliza yao ambao walitaka kutenganishwa kwa viwango vya ada kulingana na mitaji.

Alisema serikali imesikia maoni ya wadau na katika kanuni zijazo watatenganisha ada za wakusanyaji, wasafirishaji, wauzaji na wenye viwanda kwa kuzingatia mporomoko wa bei za bidhaa mbalimbali.

"Katika kipindi hiki cha mpito tutazunguka kuongea na watu mahusus wataangalia vibali na iwapo itabainika mtu hajakaguliwa na kupewa cheti cha EAA ajue moja kwa moja atafungiwa kufanya biashara hiyo, hata zikija kanuni mpya wala asiombe leseni," alisema.

Kwa mujibu wa waziri huyo, baada ya mchakato kukamilika, serikali itatangaza viwango vipya vya leseni kwa kuangalia mporomoko wa bei kulingana na shughuli mbalimbali nchini, na kwamba walio na vibali wataendelea navyo hadi muda wake utakavyokwisha.

Aidha, alisema uamuzi wa kufanya mabadiliko kwenye kanuni za usafirishaji wa taka hatarishi ulitokana na kuwapo kwa idadi kubwa ya watu wanaosafirisha nje ya nchi taka ambazo zingefaa kuwa malighafi ya nondo nchini.

"Kuanzia Januari hadi sasa kontena 280 yaani kilo milioni tano za chuma chakavu zimetoka Tanzania kwenda nje, na zinazoingia pia ni nyingi, na hizo ni zilizorekodiwa pekee inaonyesha ni kiasi gani nchi inapoteza malighafi ambayo ingetumika nchini na mapato pia," alisema.

Alisema udhibiti wa vyuma chakavu ni muhimu kwa manufaa ya nje na kwamba yapo makontena yanayoshikiliwa bandarini ambayo yanachunguzwa na vyombo vya ulinzi na usalama kujua kilichotoka, kimetokaje na katika mazingira gani.

Awali, wadau hao waliitaka serikali kuwagawanya wafanyabiashara hao kwenye makundi kutokana na biashara zao na siyo kuwatoza Sh. milioni 5 kwa wakusanyaji na wasafirishaji na wenye viwanda Sh. milioni 10.

Walisema wafanyabiashara hao wanakabiliwa na kodi mbalimbali ikiwamo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kibali cha halmashauri na polisi wanaowakamata.

Nao, wakusanyaji wa vyuma chakavu waliiomba serikali kuangalia mitaji yao ambayo haizidi Sh. milioni 3 na kuwapa vitambulisho vilivyotolewa na Rais John Magufuli kwa Sh. 20,000 kwa mwaka.



Mwendesha guta akitoa msaada wa kumsukuma mwenzake kupanda kutokana na uzito wa mzigo aliochukua jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Zitto ahoji ziliko bil. 800/-

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, ameitaka serikali kuonyesha ziliko Sh. bilioni 800 anazodai matumizi yake hayaonekani katika mwaka wa fedha 2017/18.

Zitto alitoa kauli hiyo jijini Dodoma jana, alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka wa fedha 2017/18 iliyowasilishwa na serikali bungeni jijini hapa Jumatano iliyopita.

Zitto alidai chama chake kimeichambua ripoti hiyo katika maeneo 10 muhimu, huku akitoa mapendekezo tisa ambayo serikali inabidi kuyafanyia kazi likiwamo la kuimarisha mifumo.

Mbunge huyo wa Kigoma Mjini pia aliishauri serikali kutambua kuwa njia bora ya kupambana na rushwa na ufisadi ni kuwezesha mifumo kufanya kazi, akieleza kuwa mtu mmoja hawezi kamwe kuwa dawa ya ufisadi ulioota mizizi nchini.

Zitto alidai: "Serikali ionyeshe ilipo Sh. bilioni 800 isiyoonekana matumizi yake katika ripoti ya CAG ya mwaka wa fedha 2017/18. Sh. bilioni 800 hazikutolewa kwa ukaguzi.

"Katika uchambuzi wetu wa mwaka jana, tulionyesha kuwa asilimia sita ya fedha zilizokuwa zimekusanywa na serikali hazijulikani zilipokwenda."

Alidai kiwango hicho ni sawa na Sh. trilioni 1.5 ambazo mjadala wake ulichukua mwaka mzima hadi hoja hiyo iliposababisha kufanyika kwa uhakiki maalum wa CAG.

Zitto alidai bado serikali ilishindwa kuonye-

INAENDELEA UK. 8

MAENDELEO BANK
Together in Progress

MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES
Charges are VAT Exclusive

| | ITEM/TRANSACTION | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **OPENING BALANCE** | **TZS** | **USD** | **EUR** | **GBP** |
| | **1.1 SAVINGS ACCOUNTS** | | | | |
| | **Easy account** | NA | NA | NA | NA |
| | Achievers accounts | NA | NA | NA | NA |
| | Ordinary Person Savings account | 10,000.00 | 10 | 10 | 10 |
| | Salary account | NA | NA | NA | NA |
| | Executive savings accounts | 100,000.00 | 50 | 50 | 50 |
| | Maendeleo Wekeza account | 20,000.00 | 20 | 20 | 20 |
| | Maendeleo Juniour account | 10,000.00 | 10 | 10 | 10 |
| | Maendeleo Ahadi account | 20,000.00 | 50 | 50 | 50 |
| | Staff Account | - | 0 | 0 | 0 |
| | SGL Savings Account | - | 0 | 0 | 0 |
| | VICOBA Savings Account | 50,000.00 | 50 | 50 | 50 |
| | | | | | |
| | **(Monthly fees)** | | | | |
| | Easy Account | No charges | NA | NA | NA |
| | Achievers accounts | No charges | No charges | No charges | No charges |
| | Ordinary Person Savings account | 1,000.00 | No charges | No charges | No charges |
| | Salary account | No charges | No charges | No charges | No charges |
| | Executive savings accounts | 5,000.00 | 5 | 5 | 5 |
| | Maendeleo Wekeza account | No charges | No charges | No charges | No charges |
| | Maendeleo Juniour account | No charges | No charges | No charges | No charges |
| | Maendeleo Ahadi account | No charges | No charges | No charges | No charges |
| | Staff Account | No charges | No charges | No charges | No charges |
| | SGL Savings Account | No charges | No charges | No charges | No charges |
| | VICOBA Savings Account | No charges | No charges | No charges | No charges |
| | | | | | |
| | **1.3 CURRENT ACCOUNTS** | | | | |
| | Person Current Account | 50,000.00 | 50 | 50 | 50 |
| | Jamii Current Account | 50,000.00 | 50 | 50 | 50 |
| | Progressive Account | 50,000.00 | 50 | 50 | 50 |
| | Soleproprietor Account | 50,000.00 | 50 | 50 | 50 |
| | Limited Company Account | 100,000.00 | 100 | 100 | 100 |
| | Partnership Account | 50,000.00 | 50 | 50 | 50 |
| | | | | | |
| | **(Monthly fees)** | | | | |
| | Person Current Account | 6,000.00 | 6 | 6 | 6 |
| | Jamii Current Account | No charges | No charges | No charges | No charges |
| | Progressive Account | 6,000.00 | 6 | 6 | 6 |
| | Soleproprietor Account | 9,000.00 | 6 | 6 | 6 |
| | Limited Company Account | 10,000.00 | 10 | 10 | 10 |
| | Partnership Account | 9,000.00 | 6 | 6 | 6 |
| | | | | | |
| 2 | **OTHER CHARGES** | | | | |
| | Withdraw over the counter | Up to 5m 1500, 5m-20m 2500, 20m-50m 6000, 50m above 15000. | 0.5% Max 100 | 0.5% Max 100 | 0.5% Max 100 |
| | Fee per ATM withdraw | 1,300.00 | NA | NA | NA |
| | Atm mini statement | 500.00 | NA | NA | NA |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | **2.1 Statement** | | | | |
| | Current account per page | 2,000.00 | 2 | 2 | 2 |
| | Savings | 1,000.00 | 1 | 1 | 1 |
| | | | | | |
| | **2.2 Cheque** | | | | |
| | 100 leafs | 45,000.00 | 40 | 40 | 40 |
| | 50 leafs | 35,000.00 | 30 | 30 | 30 |
| | Dishonoured inward cheque -refer to drawer | 50,000.00 | 30 | 30 | |
| | Counter leaf cheque | 10,000.00 | 10 | 10 | 10 |
| | Stop Payment | 20,000.00 | 15 | 15 | 15 |
| | Standing order outside | 11,000.00 | | | |
| | Standing Order within | No charges | No charges | No charges | No charges |
| | Balance Inquring | 500.00 | 1 | 1 | 1 |
| | Clearing -Tach service | 1,000.00 | 1 | 1 | 1 |
| | Inhouse Cheque-insufficient | 50,000.00 | 40 | 40 | 40 |
| | New Atm Issuance | 10,000.00 | NA | NA | NA |
| | Atm card renewal or replacment | 10,000.00 | NA | NA | NA |
| | Over drawn account interest charge | 2.25%( maxim 100k per day) | 2.25% | 2.25% | 2.25% |
| | Unarrange overdraw | 2.25% | 2.25% | 2.25% | 2.25% |
| | Pin Replacement | 10,000.00 | | | |
| | **2.3 Mobile banking** | | | | |
| | Balance inquery | 200.00 | 1 | 1 | 1 |
| | Account to account transfer | 1,000.00 | 2 | 2 | 2 |
| | | | | | |
| | Foreign transaction withdraw | | 1% of the amount, Max 100.00 | 1% of the amount, Max 100.00 | 1% of the amount, Max 100.00 |
| | Reactivation of Savings accounts | No charges | No charges | No charges | No charges |
| | Reactivaion of Current accounts | No charges | No charges | No charges | No charges |
| | Introduction Letter | 30,000.00 | 15 | | |
| | Visa Letter | 50,000.00 | 25 | 25 | 25 |
| | TISS | 11,000.00 | 12 | 12 | 12 |
| | Closing Current account | 20,000.00 | 10 | 10 | 10 |
| | Closing Savings account | 10,000.00 | 10 | 10 | 10 |
| | Confirmation of Balance | 12,000.00 | 25 | 25 | 12 |
| | Clossing Account Less 6 months | 5,000.00 | 5 | 5 | 5 |
| | Salary Processing | 2,000.00 | 2 | 3 | 3 |
| | Bankers cheque | 10,000.00 | 10 | 10 | 10 |
| | BRELLA searching fee | 25,000.00 | 20 | 20 | 20 |
| | Internal account transfer | 2,000.00 | 2 | 2 | 2 |
| | | | | | |
| | **2.4 Telegrafic Transfer** | | | | |
| | Swift Outgoing Money Transfer charge | | 80.00 | 80.00 | 80.00 |
| | Swift Incoming Money Transfer charge | | 10.00 | 10.00 | 10.00 |
| | Ammendment of SWIFT RETURN | | 30.00 | 30.00 | 30.00 |

| **Prepared by:** | Job Title | Date | Signature |
|---|---|---|---|
| Mr. Bella Mushongi | Business Development Manager | 12.04.2019 | |
| | | | |
| | | | |
| **Authorized by:** | | | |
| Mr. George Wandwalo | Head of ICT and Operations | 12.04.2019 | |
| Mr. Peter Tarimo | Head of Finance | 12.04.2019 | |
| Mr. Ibrahim Mwangalaba | Managing Director | 12.04.2019 | |

215177502

# Sekondari wanolewa uombaji mikopo HESLB

**Na Mwandishi Wetu,** MASWA

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imeanza kuendesha programu za elimu kwa wanafunzi wa shule za sekondari waliopo mikoani ili kuwaelimisha kuhusu sifa na taratibu za kuomba mikopo kwa usahihi.

Akizungumza wilayani Maswa, mkoani Simiyu na wanafunzi 1,166 wa kidato cha sita kutoka shule zote 12 za mkoa huo, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema uendeshaji wa programu hizo unalenga kuondokana na changamoto wanazopata wanafunzi wakati wa kuomba mikopo ya elimu ya juu.

HESLB ilianza kuendesha programu hizo katika mkoa wa Dar es Salaam.

Wanafunzi hao wapo katika kambi iliyoandaliwa na uongozi wa mkoa wa Simiyu kwa ajili ya maandalizi ya mitihani ya kidato cha sita inayotarajiwa kufanyika mwezi ujao wa Mei. Kambi hiyo ipo katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Maswa.

"Uzoefu wetu na maoni ya wadau wetu umetufanya tuanzishe programu hizi nchini kote ili wakati wa kuomba mikopo, muombe kwa usahihi na wale wenye sifa wapate na hatimaye kutimiza ndoto zao," aliwaambia wanafunzi hao na kueleza kuwa kuanzia kesho (Aprili 15, 2019) maofisa wa HESLB watakuwa katika shule mbalimbali mikoani kutoa elimu hiyo," alisema.

Katika mikutano hiyo, wanafunzi wanaelezwa kuhusu sifa, nyaraka muhimu zinazotakiwa, namna ya kuomba na kuwasilisha kwa usahihi kwa njia ya mtandao na utaratibu na umuhimu wa kurejesha mkopo mara wamalizapo masomo. Katika programu hizi, wanafunzi pia hupata fursa ya kuuliza maswali na kupata ufafanuzi.

Kwa mujibu wa Badru, katika mwaka wa masomo 2018/2019, kati ya waombaji wa mikopo zaidi ya 57,000 ambao walipata udahili vyuoni, maombi zaidi ya 9,000 yalikuwa na upungufu mkubwa ikiwamo kukosa nyaraka kama vyeti vya kuzaliwa, vitambulisho sahihi vya wadhamini, kutosainiwa na waombaji, wadhamini au serikali za mitaa au vijiji.

Ofisa Mikopo Mwandamizi kutoka HESLB, Daudi Elisha, aliwasihi wanafunzi hao kusoma kwa makini mwongozo utakaotolewa na HESLB mwezi ujao ambao utaeleza hatua kwa hatua kuhusu uombaji wa mkopo.

# Uimarishaji wa mpaka Tanzania, Kenya kwa kasi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema kazi ya uimarishaji mpaka wa Tanzania na Kenya kuanzia eneo la Ziwa Natroni katika Wilaya ya Ngorongoro hadi Namanga Wilaya ya Longido mkoani Arusha, inaendelea kwa kasi kubwa na sasa ukaguzi kwa ajili ya kuhuisha mpaka huo umekamilika.

Ukaguzi huo unafuatia kukamilika zoezi la kuhuisha alama za mipaka ya nchi hizo mbili kuanzia Ziwa Victoria mkoani Mara hadi eneo la kijiji cha Engoserosambu kilichopo Wilaya ya Ngorongoro mkoani Arusha, ambapo alama za mpaka zimehuishwa umbali wa kilomita 238. Tayari timu za wataalamu kutoka Tanzania na Kenya zimefanya ukaguzi eneo la mpaka kuanzia Ziwa Natroni hadi eneo la Namanga, ambapo timu hizo zimeainisha mahitaji ya uimarishaji mpaka huo wa nchi hizo mbili na kilichobaki ni kuwasilishwa ripoti.

Kaimu Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Samuel Katambi, mwishoni mwa wiki alitembelea mpaka huo eneo la kijiji cha Engoserosambu, Ziwa Natroni na Namanga kwa ajili ya kujionea kazi ya ukaguzi iliyofanyika ikiwa ni maandalizi ya uhuishaji alama za mpaka.

Katambi alijionea jinsi wataalamu wa nchi hizo walivyoshiriki katika kazi ya ukaguzi kwa nia ya kuainisha mahitaji ya uwekaji alama katika maeneo ambayo vigingi vya mipaka vimeharibika, ili kupata picha halisi kwa ajili ya kuhuisha mpaka huo.

Kwa mujibu wa Katambi, ukaguzi wa mpaka wa Tanzania na Kenya katika eneo la kuanzia Ziwa Natroni hadi Namanga ni matokeo ya mkutano wa Narok uliofanyika Kenya, ambapo nchi husika zilikubaliana kabla ya kuanza kazi ya kuhuisha mpaka zifanye ukaguzi ili kujua mahitaji halisi wakati wa kuimarisha mpaka.

Alisema, zoezi hilo litakapokamilika litaendelea maeneo mengine kutoka Namanga kuelekea mpaka wa Tanzania na Kenya eneo la Tarakea mkoani Kilimanjaro hadi kijiji cha Jasini Wilaya ya Mkinga Mkoa wa Tanga, hivyo kukamilisha uhuishaji mpaka huo wenye urefu wa kilomita 760 kutoka Ziwa Victoria hadi Jasini.

Mkuu wa Kikosi Kazi cha Ukaguzi Uimarishaji Mpaka wa Tanzania na Kenya kwa upande wa Tanzania, Joseph Ikorongo, alisema, zoezi la ukaguzi kwa ajili ya maandalizi ya uimarishaji mpaka wa nchi hizo mbili eneo la Ziwa Natron hadi Namanga limeenda vizuri na jumla ya kilomita 138 zimeshakaguliwa likiwamo eneo ambalo halijawahi kuhuishwa tangu enzi za ukoloni la za Ziwa Natroni kati ya kijiji cha Nani na Jema lenye urefu wa kilomita 20.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

SUMATRA
For Competitive, Efficient, Quality and Safe Transport Services
Surface and Marine Transport Regulatory Authority
Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini

**TAARIFA KWA UMMA**

**MARUFUKU KUWATUMIA VISHOKA KUPATA HUDUMA ZA SUMATRA**

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu na Majini (SUMATRA) inatoa taarifa kwa wasafirishaji na Umma kuwa imebaini matukio kadhaa ya kitapeli yanayofanywa na vishoka katika baadhi ya ofisi za SUMATRA.

Wasafirishaji na watendaji wao wanaelekezwa kuhakikisha wanahudumiwa ndani ya ofisi za Mamlaka tu. Aidha hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mtu yeyote atakayebainika kushawishi kumsaidia mteja wa SUMATRA nje ya ofisi kinyume na taratibu.

**Imetolewana:**

**Salum S. Pazzy**
**Kny: MkurugenziMkuu,**
**SUMATRA**

215169902

TANGAZO


TANZANIA
UGANDA
COMOROS
DJIBOUTI
AFCONIKA
na Exim
TWENDE TUKALIAMSHE MISRI
Malazi
Tiketi ya Ndege
Chakula
Tiketi ya Mechi
TANZANIA
SHINDA safari ya kwenda kuliamsha Misri na TAIFA STARS! EXIM inawapa wateja wake wapya na wa sasa nafasi ya kwenda kuishangalia timu ya Taifa AFCON. Ili kuweza kupata nafasi hii, Weka kiwango cha Tshs. 500,000 au zaidi kwenye akaunti ya Akiba, Tshs. 10,000,000 kwenye akaunti ya Biashara au Tshs. 5,000,000 kwenye akaunti ya Amana maalum. Nafasi ni yako mteja mpya na mteja wa sasa wa EXIM! #AfconikaNaExim
*Vigezo na Masharti Kuzingatiwa
Namba ya simu: 0800 780 111 Barua pepe: customercare@eximbank.co.tz
EXIM BANK
Innovation is life

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Ahadi Serengeti Boys ikifuzu zitolewe sasa

**FAINALI** za Mataifa ya Afrika kwa vijana wenye umri chini ya miaka 17 (Afcon U-17), zimeanza kutimua vumbi nchini, safari hii Tanzania ikiwa mwenyeji kwa mara ya kwanza katika historia ya michuano hiyo.

Utepe wa fainali hizo ulikatwa rasmi katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salama jana, kwa wenyeji Serengeti Boys kucheza dhidi ya Nigeria kabla ya Angola kuvaana na Uganda, hizo zikiwa ni mechi za Kundi A. Leo michuano hiyo itaendelea kwa upande wa Kundi B kwa Guinea kuvaana na Cameroon na baadaye tukiishuhudia Morocco ikicheza na Senegal.

Wenyeji Tanzania, Serengeti Boys watarudi tena uwanjani Jumatano kuvaana na Angola katika mechi yake ya pili kwenye mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika, Caf. Ikumbukwe michuano hiyo ndiyo itakayotoa wawakilishi wanne wa Afrika katika fainali za Kombe la Dunia U-17 zitakazofanyika nchini Brazil Oktoba mwaka huu. Na kwa mujibu wa Caf, mshindi wa kwanza na wa pili kutoka katika kila kundi atafuzu moja kwa moja fainali hizo za Kombe la Dunia.

Kutokana na mchakato ulivyo, timu itakayoshinda mechi mbili tu, itakuwa tayari imejihakikishia tiketi ya kushiriki fainali hizo Oktoba mwaka huu. Hivyo, kinachotakiwa kwa sasa ni kuendelea kuisapoti Serengeti Boys ndani na nje ya uwanja ili iweze kufuzu kwani ushindi wake ni wa Watanzania wote.

Tunatumai Watanzania kwa ujumla wataendelea kujitokeza kwa wingi kuisapoti Serengeti Boys kama walivyotumia vema nafasi yao kwa kuwasapoti kaka zao, Taifa Stars dhidi ya Uganda (Cranes) na hatimaye kufuzu Afcon 2019 nchini Misri.

Tunatambua shabiki ni mchezaji wa 12 kwa timu inapokuwa dimbani, hivyo Watanzania hatuna budi kuitumia nafasi hiyo muhimu hasa ukichukulia michuano hii inafanyika ardhi ya nyumbani, kwani mahudhurio ya jana hayakuwa na afya kama ambavyo wengi walijitokeza kwenye mechi ya Stars dhidi ya Uganda. Hatuna budi kuanza kwa kuhakikisha tunakuwa kitu kimoja kwa kuisapoti kwa hali na mali ifuzu kwanza Kombe la Dunia na kisha ndipo tugeukie kutumia nafasi zetu kuiwezesha kutwaa ubingwa huo wa Afcon U-17.

Hata hivyo, ili kuhakikisha hilo linawezekana, kama ambavyo tumeona Mlezi wa Serengeti Boys, Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, akiahidi kutoa Sh. milioni 20 kwa kila mchezaji endapo watafuzu Kombe la Dunia, ndivyo ambavyo kwa wingi wetu tunatakiwa kujitokeza kutoa ahadi zetu sasa.

Kuna 'kautamaduni' kamejengeka kusubiri hadi mafanikio yapatikane ndipo mhusika aanze kuzawadiwa na ahadi kedekede zikitolewa, katika hilo Watanzania tunapaswa kubadilika sasa kwa kuiga hiki kilichofanywa na Dk. Mengi kwa kuwaahidi mapema Serengeti Boys mamilioni ya shilingi kila mmoja.

Nipashe tunaamini ahadi kama hizo zikitolewa mapema zitaongeza morali ya kupambambana kwa wachezaji na hatimaye kufuzu kirahisi na kabla ya kuutwaa kabisa ubingwa huo.


Lengo letu ni kuona Tanzania ikiandika historia mpya kwa kufuzu michuano ya Kombe la Dunia na kutwaa ubingwa wa U-17 mwaka huu, hivyo hilo linaweza kutimia kirahisi zaidi kama wote tukiguswa kama Dk. Mengi kwa kuwaongezea ari Serengeti Boys.

Kunapokuwa na zawadi mbali ya kufuzu Kombe la Dunia na kutwaa ubingwa huo, ni wazi moyo na ari ya kujituma zaidi itaongezeka kuliko kusubiri mwishoni baada ya timu hiyo kupata mafanikio. Hivyo, ni matarajio yetu Watanzania wenye mapenzi mema ya kuona Serengeti Boys inapata mafanikio hayo mbali na kwenda uwanjani kuisapoti, watajitokeza sasa kutoa ahadi kwa wachezaji ili kuwaongezea kiu ya kufikia malengo yao hayo.

Na katika hili Nipashe tunapenda kusisitiza kuwa halihitaji hadi uwe na mamilioni ndipo ujitokeze kuahidi, kwa kuwa kidogo chako ni kikubwa katika kuyatafuta mafanikio kwa vijana hawa waliodhamiria kuitoa kimasomaso Tanzania. Tunaitakia Kila la Kheri Serengeti Boys.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

### TFF imeshindwa sakata la Kakolanya?

Na Adam Fungamwango

**ZAIDI** ya miezi sita sasa kumekuwa na msuguano kati ya Klabu ya Yanga na kipa wao, Beno Kakolanya.

Pamoja na mambo mengine, Kakolanya aliandika barua kuomba kuvunjwa mkataba wake kwenye klabu hiyo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo kutotimiziwa maslahi yake waliyokubaliana.

Msuguano huo ulisababisha Kakolanya kusuasua kwenda mazoezini kiasi cha kumkasirikia Kocha Mkuu, Mwinyi Zahera.

Alichofanya ni kumtimua Kakolanya katika kikosi cha Yanga wakati akiwa bado na mkataba mpaka mwaka 2020 kwa madai kuwa ni msaliti kutokana na kugoma kuitumikia timu hiyo akishinikiza kulipwa madai yake.

Kipa huyo wa zamani wa timu ya Tanzania, Taifa Stars, akaandika barua kwa waajiri wake, lakini bila majibu, hivyo akawa halipwi, hatakiwi kwenye kikosi na hata hakuna makubaliano yoyote angalau ya pande zote mbili kuachana kwa amani ili kila mmoja afanye mambo yake.

Hali ilipozidi meneja wake, Selemani Haroub, aliandika barua kupeleka Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi. Hata yeye mwenyewe anashangaa hadi leo suala hilo limekuwa na kigugumizi.

"Tulilipeleka TFF kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi, lakini mpaka sasa bado," anasema meneja huyo.

Anasema mpaka sasa kipa huyo hajui msimu ujao atakuwa na timu gani kutokana na TFF kushindwa kulipatia ufumbuzi suala lake hilo na Yanga.

Utata unaanzia hapa. Kwa nini TFF ambayo pamoja na kwamba inaongoza soka, lakini pia ni mpatanishi wa klabu na wachezaji haiwaweki pamoja ili kumalizana?

Kwa nini TFF kupitia kamati zake haiwaiti Yanga pamoja na Kakolanya mwenyewe ili kuwaweka sawa na wakipatana arudi kundini?

Na kama ikishindikana kwa nini haitumii sheria na kanuni ili kuangalia tatizo lilipoanzia hadi lilipoishia na kubaini nani amevunja vipengele vya mkataba ili yeyote katika pande hizo mbili amlipe mwenzie ili kila mmoja achukue hamsini zake maisha yaendelee?

Hivi TFF kukaa kimya huku mchezaji akiwa hachezi ni kuua kipaji chake ikichukuliwa kuwa alikuwa kipa wa timu ya taifa, lakini kwa sasa ameachwa kwa sababu hajacheza muda mrefu?

TFF haidhani kuwa kitendo cha Yanga kuwa kimya ni kama vile kumkomoa mchezaji, huku na yenyewe pia ikiwa kimya ni kutomtendea haki mchezaji kwa sababu anayeumia hapo ni Kakolanya na si klabu?

Cha ajabu ni kwamba hata Chama cha Wachezaji nchini (Sputanza) kimekaa kimya kwenye hili, huku mchezaji akiwa hajui hatima yake wakati wakiwa wakali sana kwenye masuala ya mikataba inapohusu wachezaji wengine.

Mimi nadhani imefika wakati sasa TFF kufanya maamuzi kwenye hili kwa sababu limechosha masikioni mwa mashabiki wa soka nchini, huku mchezaji akiwa haelewi hatima yake.

Soka ni ajira kwa sasa na si kukomoana na ndiyo maana hata Shirikisho la Soka nchini (Fifa) huwa linatoa kibali cha miezi sita kuitumikia klabu nyingine kwa mchezaji ambaye anaonekana ana matatizo ya kimkataba au kimaslahi na klabu yake mpaka hapo utata wa tatizo lake litakapotatulia.

Fifa wanafanya hivyo kwa kusudi la kulinda kipaji cha mchezaji na kufanya maishi yaendelee.

Nashauri kama TFF haiwezi kufanya hivyo, basi imsaidia mchezaji huyo ili suala lake liende Fifa ambao wao wataamua bila woga, badala ya kuheshimu mihemko au kuogopa siasa za soka nchini.

# TANGAZO

China Commercial Bank
中國商業銀行

## PUBLICATION OF FINANCIAL STATEMENTS

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2018
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-18 | Mwaka wa sasa 31-Dec-17 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 748 | 442 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 6,762 | 1,357 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 1,475 | 5,084 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,356 | 22,034 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 365 | 15 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 696 | 1,917 |
| 12 | Mali Nyingine | 222 | 354 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,256 | 2,123 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **12,880** | **33,326** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | - | 6,851 |
| 18 | Amana za Wateja | 3,989 | 11,856 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 292 | 1,024 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | - |
| 27 | Dhima Nyingine | - | - |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **4,280** | **19,730** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **8,599** | **13,596** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 20,881 | 20,881 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 115 | 19 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (14,319) | (11,468) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | - | - |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,922 | 4,164 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **8,599** | **13,596** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo Chechefu | 193 | 32 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 50 | 32 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | -66% | 41% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 25% | 2% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 20% | 10% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 6% | 6% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 87% | 87% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -197% | 36% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -61% | 4% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2018 (Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-18 | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-17 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 1,322 | 2,869 |
| 2 | Gharama za Riba | (301) | (790) |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2) | **1,020** | **2,079** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo/Mali zingine | (636) | (3,217) |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **552** | **198** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 21 | 41 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 441 | 148 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 89 | 8 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **(3,682)** | **(5,443)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (936) | (1,591) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | (1,880) | (2,946) |
| | 7.3 Gharama Nyingine | (867) | (906) |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(2,745)** | **(6,383)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 9 | 9 |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(2,754)** | **(6,392)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | **-** | **-** |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(2,754)** | **(6,392)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 19 | 28 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (9,795) | (9,795) |
| 15 | **Idadi ya Matawi** | 1 | 1 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -12% | -20% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -25% | -41% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | -197% | -177% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 8% | 7% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
KWA ROBO/MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA, 2018
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-18 | Mwaka wa sasa 31-Dec-17 |
|---|---|---|---|
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (2,745) | (6,383) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| | - Hasara Katika Mali | 1,502 | 4,122 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 1,221 | (265) |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (6) | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (14,718) | 4,906 |
| | - Mabadiliko Halisi uwekezaji kwenye benki nyingine | 506 | (5,635) |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (733) | 855 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 132 | (353) |
| | -Faida/Hasara miamala ya fedha za kigeni | (21) | (41) |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **(14,861)** | **(2,794)** |
| **II.** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (23) | (24) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Manunuzi ya/uwekezaji kwenye dhamana za serikali | 3,610 | 370 |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **3,586** | **346** |
| **III.** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | (2,242) | 2,581 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **(2,242)** | **2,581** |
| **IV.** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | (13,517) | 133 |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 21,401 | 21,268 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | **7,884** | **21,401** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA ROBO/MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2018
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **28,128** | **(11,468)** | **-** | **19** | **16,679** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (2,754) | - | - | **(2,754)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | 1,922 | - | - | - | **1,922** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | 110 | (110) | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | 5 | - | (5) | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **30,050** | **(14,107)** | **(110)** | **14** | **15,847** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **25,547** | **(5,099)** | **17** | **26** | **20,489** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | (6,392) | - | - | **(6,392)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | **-** |
| Miamala na wanahisa | 2,581 | - | - | - | **2,581** |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | **-** |
| Ziada ya Kisheria | - | 17 | (17) | - | **-** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | 7 | - | (7) | **-** |
| Mengineyo | - | - | - | - | **-** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **28,128** | **(11,468)** | **-** | **19** | **16,679** |

### BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA INAYOISHIA 31 DESEMBA, 2018

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| Jina na Cheo | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| XIONG ZHENGLIN (Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu) | IMESAININWA | 28.04.2018 |
| GABRIEL JULIUS (Mkuu wa Fedha) | IMESAININWA | 28.04.2018 |
| VICTORIA EDWARD (Mkaguzi Mkuu wa Ndani) | IMESAININWA | 28.04.2018 |

Sisi tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa Taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathimini taarifa hizi,na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya kimataifa vya uwasilishaji wa Taarifa za fedha na matakwa ya sheria ya Benki na Taasisi za fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi

| | | |
|---|---|---|
| **LIU LIN** MJUMBE WA BODI | IMESAININWA | 28.04.2018 |
| **ZHU JIN FENG** | IMESAININWA | 28.04.2018 |

## The Banking and Financial Institutions (Disclosures) Regulations, 2014
## MINIMUM DISCLOSURES OF CHARGES AND FEES
## (Made under Regulation 11)

| No. | ITEM/TRANSACTION | CHARGE/FEE | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **Current Accounts** | **TZS** | | **USD** | |
| | (a) Required minimum opening balance | | | | |
| | Personal Current Account | TZS | 100,000.00 | $ | 100.00 |
| | Business Account | TZS | 200,000.00 | $ | 200.00 |
| | Imperial Business Account | TZS | 5,000,000.00 | $ | 5,000.00 |
| | Community Account | TZS | 200,000.00 | $ | 200.00 |
| | Call Account | TZS | 10,000,000.00 | $ | 10,000.00 |
| | (b) Monthly service fee (break down per customer type) | | | | |
| | Personal Current Account | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Business Account | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Imperial Business Account | TZS | 25,960.00 | $ | 25.96 |
| | Community Account | Free | | Free | |
| | Call Account | Free | | Free | |
| | (c) Cheque withdrawal over the counter | TZS | 1,947.00 | 0.75% of withdrawal amount | |
| | (d) Fees per ATM Withdrawal | | | | |
| | Personal Savings (5 free withdrawals per month) | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | Imperial Savings (5 free withdrawals per month) | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | Student Boom Account | TZS | - | $ | - |
| | Junior Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | Senior Savings Account (3 free withdrawals per month) | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | Personal Current Account | TZS | 1,300.00 | $ | - |
| | (e) ATM mini statement | TZS | 300.00 | $ | - |
| | (f) Interim statement (Below 3 months) | TZS | 3,894.00 | $ | 2.60 |
| | (g) Periodic scheduled statement | Free | | Free | |
| | (h) Cheque book (per leaf) | TZS | 519.20 | $ | 0.52 |
| | (i) Dishonoured Cheque | | | | |
| | Inward Unpaid Cheque | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Outward Unpaid Cheque | TZS | 38,940.00 | $ | 38.94 |
| | (j) Special clearance | | | | |
| | Personal Accounts | TZS | 51,920.00 | $ | 51.92 |
| | Business Accounts | TZS | 64,900.00 | $ | 64.90 |
| | (k) Counter cheque (per leaf) | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | (l) Stop payment (per leaf) | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | (m) Standing order | | | | |
| | Internal | Free | | Free | |
| | External | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Unpaid | TZS | 6,490.00 | $ | 6.49 |
| | (n) Balance enquiry | Free | | Free | |
| | (o) New ATM card issuance | Free | | Free | |
| | (p) ATM card renewal or replacement | TZS | 12,980.00 | $ | - |
| | (q) Overdrawn Account interest charge | 10% above the Banks Base Lending Rate | | | |
| | (r) Unarranged overdraft | 10% above the Banks Base Lending Rate | | | |
| | (s) Interbank transfer | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | (t) Bill payments through ATM | TZS | 713.90 | $ | - |
| | (u) Deposit fee | Free | | Free | |
| | (v) Other (please specify) | | | | |
| | ATM withdrawal limit per transaction | TZS | 400,000.00 | $ | - |
| | ATM withdrawal daily limit | TZS | 1,000,000.00 | $ | - |
| 2 | **Savings Accounts** | | | | |
| | (a) Required minimum opening balance | | | | |
| | Personal Savings Account | TZS | 50,000.00 | $ | 50.00 |
| | Student Boom | TZS | 20,000.00 | $ | 20.00 |
| | Senior Savings Account | TZS | 50,000.00 | $ | 50.00 |
| | Joint Savings Account | TZS | 50,000.00 | $ | 50.00 |
| | Imperial Savings Account | TZS | 2,000,000.00 | $ | 2,000.00 |
| | Junior Savings Account | TZS | 10,000.00 | $ | 10.00 |
| | (b) Monthly service fee | | | | |
| | Personal Savings Account | TZS | 9,086.00 | $ | 9.09 |
| | Student Boom | Free | | Free | |
| | Senior Savings Account | TZS | 9,086.00 | $ | 9,086.00 |
| | Joint Savings Account | TZS | 9,086.00 | $ | 9,086.00 |
| | Imperial Savings Account | TZS | 19,470.00 | $ | 19.47 |
| | - Imperial Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | - Imperial Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | - Junior Savings Account | TZS | - | $ | - |
| | (e) Deposit rate (Personal savings accounts) | | 2.5% | $ | 0.01 |
| 3 | **Electronic Banking** | | Free | | Free |
| | (a) Internet Banking monthly fee | | FREE | | FREE |
| | (b) Internet transfers | | FREE | | FREE |
| | (c )SMS Banking | | NA | | NA |
| | (d) Other | | | | |
| | E-Banking Statement request(Self downloaded) | | FREE | | FREE |
| | E-Banking Password resetting | | FREE | | FREE |
| | E-Banking Statement request (printed by the Bank) per page | | TZS 1,298 | | $1.298 |
| 4 | **Foreign Exchange Transaction** | | | | |
| | (a) Purchase/sale of TCs transactions over the counter | | - | | - |
| | (b) Purchase of foreign cheque | | - | | - |
| | (c) Sale/Purchase of cash passport | | - | | - |
| | (d) Telegraphic Transfer (TISS/RTGS) | | | | |
| | Outward TT | TZS | 12,980.00 | $ | 12.98 |
| | Inward TT | | Free | | Free |
| | (e) Telex/Swift | | | | |
| | Outward TT | | | $ | 64.90 |
| | Inward TT | | | $ | 12.98 |
| | (f) Transfer from foreign currency denominated Account to local current Account ( within bank and to other bank) | | - | | - |
| 5 | **Loans** | | | | |
| | (a) Processing/Arrangement/Appraisal fee | | | | |
| | (i) Personal loans | 2% of the facility amount | | | |
| | (ii) Overdrafts | 2% of the facility amount | | | |
| | (iii) Mortgage finance | 2% of the facility amount | | | |
| | (iv) Asset finance | 2% of the facility amount | | | |
| | (b) Unpaid loan instalment | 10% above interest rate | | | |
| | (c) Early repayment | 3% of amount to be settled early | | | |
| | (d) Valuation fees | As per service provider rates | | | |
| | (e) Legal Fees | As per service provider rates | | | |
| | (f) Base Lending Rates | | 21% | $ | 0.09 |
| | (g) Maximum Spread Above the Base Lending Rate (BLR) | | 5% | $ | 0.05 |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

| | Name | Signature | Designation | Date |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Xiong Zhenglin | | Chief Executive Officer | 12.04.2019 |
| 2 | Joseph Phales | | Ag: Head of Business & Operations | 12.04.2019 |

215178402

# Ndugai 'ampeleka' Prof. Assad kwa JPM

INATOKA UK. 2

"Rais ni sehemu ya sisi na ndiyo maana tumepitisha sheria kuwa lazima apitishe mkono wake ili iwe sheria," alisema Spika na kuongeza:

"Mfano hii bajeti tutajadili, tutapanga vifungu weee, hata tufanyaje, bila ya kibali cha Rais haiwezi kuwa bajeti. Kwa maneno yale aliyoyatoa dhidi ya Bunge, maana yake Rais yuko humo, Waziri Mkuu, Spika, Baraza la Mawaziri."

Ndugai alisema alichokisema Prof. Assad dhidi ya Bunge kina maana kuwa serikali ni dhaifu katika udhibiti wa fedha, alisema duniani ni hatari mkaguzi kuliambia Bunge ni dhaifu.

**AMPA ANGALIZO**

Spika Ndugai alimtaka CAG Prof. Assad (pichani), ajitathmini mwenyewe na aone kama ni busara kuendelea kufanya kazi na chombo ambacho kimemkataa.

Alisema katika nchi zingine Bunge likionyesha kutokuwa na imani ya kufanya kazi na mtu fulani, basi mhusika huyo anapaswa kujiuzulu.

Mbali na hilo, alimuonya Prof. Assad kuacha kuendelea kutumia lugha ya kulidhalilisha Bunge kwa kuliita dhaifu, vinginevyo ataitwa kuhojiwa kwa mara ya pili kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, jambo ambalo litakuwa baya zaidi.

"CAG anaposema mbele ya umma kuwa ataendelea kutuita dhaifu wakati ni jina ambalo hatulipendi na tumelikataa tunashindwa kumwelewa, kama analipenda hilo jina si ajiite yeye," alisema na kuongeza:



"Hilo neno sisi hatulipendi, natumia mkutano huu kumwambia neno hilo hataki, tunasisitiza hatulipendi jina hilo, ukirudia tutakuita tena halafu sijui nini kitatokea."

Ndugai alisema hana chuki binafsi na Prof. Assad, lakini tatizo kubwa ni lugha za udhalilishaji anazotumia dhidi ya Bunge.

Alisema ripoti ya CAG haina mambo yoyote ya ajabu ambayo Bunge inaogopa, bali ni ripoti ya kawaida.

"Tatizo letu ni maneno aliyoyasema Prof. Assad akiwa Marekani, na alipokuwa Dodoma akarudia kuwa atayasema tena. Maneno yale sisi tumeyakaa, siyo ya kistaarabu, hilo ndilo tatizo na wala siyo ripoti yake, Kwani taarifa ya CAG mmesikia kuwa Bunge limesemwa vibaya hadi tukasirike na tugombana naye?" Alihoji Ndugai.

Ndugai alisema ripoti ya CAG iliyowasilishwa bungeni itafanyiwa kazi kwa kupelekwa katika Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) pamoja na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), ambazo zitawaita na kuwahoji watuhumiwa wote waliotajwa katika ripoti hiyo, kisha taarifa itarudishwa bungeni kwa ajili ya kujadiliwa na wabunge ambao watatoa maazimio kwa serikali kuhusu nini kifanyike.

"Narudia tena kumwambia Prof. Assad taarifa tutaifanyia kazi, na Watanzania watapata mrejesho wa kila jambo lililotajwa katika ripoti hiyo. Sisi Bunge hatuhukumu watu haraka haraka," alisema Spika.

**AELEZA GHARAMA MATIBABU YAKE**

Kadhalika, Ndugai alizungumzia kuhusu taarifa zinazomhusu yeye kutumia gharama kubwa ya fedha kwa ajili ya matibabu nje ya nchi, baada ya kuulizwa swali na mmoja wa waandishi.

Ndugai alisema alipelekwa kutibiwa India kwenye moja ya hospitali ya kawaida ambayo Watanzania wengi hutibiwa.

"Nilipelekwa India mwaka 2015/16 baada ya kuwaapisha wabunge. Katika matibabu hatuangalii gharama za matibabu, tunaangalia mgonjwa kupona, au mlitaka nife?" Alihoji na kuendelea: Ni hospitali ya kawaida, nilitibiwa."

Alisema wakati akipatiwa matibabu kwenye hospitali hiyo, alikutana na Watanzania wengi waliokuwa wakipatiwa matibabu, na kwamba alipelekwa kwenye matibabu kwa utaratibu wa kiserikali ambao mwananchi yeyote lazima aufuate.

# Mama adaiwa kuwaua kwa panga watoto 6 na yeye auawa

**Na Halima Ikunji,** NZEGA

MAMA mmoja anayedaiwa kuwa mgonjwa wa akili, Nana Maganga (35), amewaua watoto wake sita kwa kuwacharanga mapanga, tukio lililotokea katika kitongoji cha Mwakilezu, Kijiji cha Luzuko, wilayani Nzega, mkoani Tabora na yeye kuuawa wakati akidhibitiwa asiendeleze mauaji hayo.

Tukio hilo limetokea majira ya saa 11 alfajiri Machi 14, mwaka huu, wakati mama huyo alipowaua watoto wake watano wa kuwazaa na mmoja akiwa mtoto wa kaka yake, huku akijeruhi watu wanne.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora Kamishna Msaidizi, ACP Emmanuel Nley, amethibitisha kutokea kwa mauaji hayo ya watu saba.

Kamanda alisema katika tukio hilo, mwenye nyumba ambaye ni shemeji ya mama aliyefanya mauaji, alimkamata na kuanza kupambana naye.

Kamanda Nley alisema Nana alikuwa ni mgonjwa wa akili, hivyo alikwenda kwa mganga wa jadi ambaye ni shemeji yake kwa lengo la kupatiwa matibabu ndipo mkasa huo wa kuwakata mapanga watoto wake ambao alikuwa amelala nao ulipotokea.

Kamanda Nley alisema kuwa waliomdhibiti Nana, walikana kumuua wakidai walimkamata na kumfunga kamba mikononi na kudai kifo chake kimetokana na yeye kunywa sumu, jambo ambalo kamanda Nley amelikanusha.

Alisema Jeshi la Polisi linawashikilia watu watano akiwamo mume wa Nana na mganga wa jadi kwa tuhuma za kumuua mwanamke huyo na kuongeza kuwa upelelezi wa tukio hilo unaendelea ili kujua chanzo cha mauaji hayo.

Aliwataja watoto waliouawa kuwa ni Pala Massanja (3), Shija Dotto (2), Nyawele Dotto (2), Sida Dotto (5), Kulwa Dotto (4), Dotto Dotto (4) na mama yao Nana.

Aliwataja waliojeruhiwa kuwa ni Kundi Dotto, Nembwa Dotto, Milembe Massanja na Mwashi Massanja.

Mkuu wa Wilaya ya Nzega, Godfrey Ngupulla, alisema tukio hilo limeibua hisia kali kwa wananchi kwa kuwa ni mara ya kwanza kutokea, hata hivyo, aliwataka wananchi kuwapeleka hospitali wagonjwa wa akili ili kuepusha madhara kama hayo.

Ngupulla alisema mgonjwa huyo huenda alitumia dawa nyingi za mitishamba hadi kusababisha kuchanganyikiwa na kuanza kushambulia watoto na hatimaye kusababisha mauaji hayo.

Mwenyekiti wa kijiji hicho Jilatu Lukwizu alisema mgonjwa huyo alifika nyumbani kwa mganga huyo ambaye ni shemeji yake Massanja Gisengi, majira ya saa mbili usiku, ndipo walipofanya maandalizi ya kulala na watoto wake na saa 11 alfajiri mama huyo alianza kuwashambulia kwa mapanga hadi kuwaua watoto hao.

## UDSM yadahili mara tano

INATOKA UK. 2

miundombinu ili kukidhi bila shida ongezeko hilo."

CAG Assad anabainisha kuwa ongezeko hilo kubwa la udahili linahatarisha ubora wa elimu watakaopata wahitimu, hivyo kuwa na athari ya muda mrefu kwa maendeleo ya taifa.

"Ninapendekeza UDSM itayarishe na kutekeleza mpango wa udahili ambao utatokana na tathmini ya mahitaji na uwezo wa chuo kikuu," Prof. Assad anasema.

Katika ripoti yake hiyo, CAG Assad pia anaushauri uongozi wa UDSM kuzingatia mkataba na kampuni hodhi ya Mlimani City ili kufuatilia kasi ya kukamilika kwa miradi iliyochelewa.

Anabainisha kuwa tarehe ya kukamilisha mradi wa Mlimani City siyo tena Septemba Mosi, 2006, kwa kuwa tarehe ya awali ilisogezwa mbele kupitia mkataba wa utendaji ambao umeainisha tarehe ya kumalizika kuwa ni Desemba 31, 2019.

"Wakati wa mkutano wa pamoja uliofanyika Aprili 20, 2017 kati ya UDSM, Kituo cha Uwekezaji (TIC) na Mlimani Holdings Ltd (MHL), MHL alisema kuwa ana nia ya kuweka bustani ya mimea Mlimani City kabla ya mwisho wa kipindi cha mkataba, lakini hapakuwa na mipango ya kujenga hoteli ya nyota nne.

"Hata hivyo, UDSM na TIC walimwomba MHL kutafakari upya suala la hoteli kulingana na mkataba uliopo na MHL aliahidi kufanya hivyo. UDSM tayari imeanzisha mchakato wa kurekebisha mkataba wa kukodisha ardhi," Prof. Assad anabainisha.

# Zitto ahoji ziliko bilioni 800/-

INATOKA UK. 3

sha zilipokwenda fedha hizo, zaidi ya kudai kuwa ilihamishia Ikulu matumizi ya Sh. bilioni 976 bila kumpa CAG uthibitisho wa uhamisho huo.

Aidai kuwa katika ukaguzi wa CAG wa bajeti ya mwaka 2017/18, ambayo ni ya pili kwa serikali ya awamu ya tano, ameonyesha bajeti ya Sh. trilioni 31.7 iliidhinishwa na Bunge.

"Serikali iliweza kukusanya Sh. trilioni 27.7 tu kutoka kwenye vyanzo vyote vya kodi, vyanzo visivyo vya kodi, mikopo ya ndani na nje, na misaada ya wahisani na washirika wa maendeleo.

"Ilishindwa kukusanya kiasi cha Sh. trilioni nne kama ilivyokuwa mwaka uliopita ingawa sasa ni sawa na asilimia 13 ya bajeti yote ya mwaka 2016/17," Zitto alidai.

Aliendelea kudai kuwa CAG anaonyesha Sh. trilioni 26.9 tu ndiyo zilitolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali na kwenda kutumika, hivyo Sh. bilioni 800 kati ya Sh. trilioni 27.7 zilizokusanywa kutokujulikana ziliko na hazikutolewa kwa ukaguzi.

Zitto alinukuu ripoti ya CAG ya mwaka 2017/18 ukurasa wa 91 akisema: "Ikilinganishwa taarifa ya kutoa fedha (exchequer issue report) na taarifa ya fedha zilizopokewa na kuripotiwa katika taarifa za fedha za mafungu husika pamoja na barua za kukiri mapokezi ya fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, imebaini utofauti wa taarifa zilizoripotiwa."

"CAG ameeleza kuwa tofauti hiyo imesababishwa na kutokuwapo kwa mifumo thabiti ya usuluhishi kati ya fedha zilizotolewa na Hazina na fedha zilizotolewa na wahisani wa maendeleo moja kwa moja kwenye miradi ya maendeleo katika wizara.

"Ni muhimu sana kusisitiza hapa kuwa kwa mujibu wa CAG kuna fedha Sh. trilioni 4.8 ambazo makusanyo yake hayakuingizwa mfuko mkuu wa serikali. Kiongozi huyo pia alidai Sh. bilioni 678 za mamlaka nyingine ziliporwa na mlipaji mkuu wa serikali.

Alidai kwenye ripoti ya CAG ya 2017/18 imeonyeshwa kuwa bado serikali inatumia fedha ambazo siyo zake (ring fenced) kama ilivyoonyeshwa kwenye ripoti ya mwaka 2016/17.

Alidai kwa mwaka 2017/18 CAG amebaini jumla ya Sh. bilioni 678 zilizokusanywa na Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa niaba ya taasisi nyingine, hazikuhamishwa kwenda kwenye taasisi husika, na badala yake zilihamishiwa kwa Katibu Mkuu Hazina, ambapo huko hazikuonekana kwenye ukaguzi kama sheria inavyotaka.

"Fedha zilizoporwa na Hazina ni pamoja na Sh. bilioni 169 za Shirika la Reli, Sh. bilioni 168 za wadau wa korosho nchini na Sh. bilioni 16 za Wakala wa Umeme Vijijini (REA).

"CAG kwa mara nyengine tena amependekeza sheria iheshimiwe kuhusu matumizi ya fedha hizi za taasisi mbalimbali. Kwenye ripoti ya CAG ya mwaka 2016/17 kiasi cha Sh. trilioni 2.2 za mamlaka mbalimbali nchini hazikurejeshwa kwenye mamlaka husika baada ya fedha hizo kukusanywa na TRA," Zitto alidai.

Pia aliitaka serikali ieleze kwanini Sh. trilioni 4.8 hazikupita kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ili utolewaji wake ufuate masharti ya katiba na sheria za nchi.

"Fedha hizi za wafadhili zinaonekana katika vitabu vya bajeti, lakini CAG hazioni kuingia Mfuko Mkuu na hivyo kutoka kwake kunaweza kuwa ni kinyume cha sheria," alidai.

Zitto aliishauri serikali kutambua kuna njia ya bora ya kupambana na rushwa na ufisadi ni kuwezesha mifumo kufanya kazi, akieleza kuwa mtu mmoja hauwezi kamwe kuwa dawa ya ufisadi ulioota mizizi nchini.

# TANGAZO

# LETSHEGO BANK (T) LIMITED

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONYESHAJI) YA MWAKA 2014

## UONYESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA 31 OF DECEMBER 2018

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2018
(Kiasi kwa millioni shilingi )

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-2018 | Mwaka wa uliopita 31-Dec-17 |
|---|---|---|---|
| A. | **MALI** | | |
| 1 | Fedha taslimu | 726 | 531 |
| 2 | Salio katika Benki Kuu ya Tanzania | 4,113 | 1,097 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | - | - |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 1,465 | 6,182 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 229 | 63 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa Kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo (Baada ya tengo la mikopo) | 28,918 | 31,504 |
| 12 | Mali Nyingine | 3,276 | 2,747 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za Udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,339 | 1,475 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **40,066** | **43,600** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 3,400 | 10,116 |
| 18 | Amana za Wateja | 11,397 | 5,818 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa fedha Tslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | - | - |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 | Limibikizo za Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 | Dhima la Tozo Kwaajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Meneja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo | 123 | 97 |
| 27 | Dhima Nyingine | 888 | 1,815 |
| 28 | Madeni | 9,224 | 7,006 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **25,032** | **24,853** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 KUTOA 20)** | **15,034** | **18,747** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 38,048 | 36,251 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | - | - |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (23,282) | (16,846) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 268 | (658) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya wenye Hisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **15,034** | **18,747** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo chechefu | 5,843 | 5,011 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 8,281 | 4,616 |
| 41 | Mali nyingine chechefu | - | - |
| | | - | - |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 38% | 43% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi (Zaidi ya Siku 90) | 15% | 15% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 251% | 228% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 72% | 72% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 101% | 86% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -7% | 0% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | -8% | 0% |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2018
(Kiasi kwa millioni shilingi )

| Mwaka wa Sasa | | Mtaji wa Hisa | Mtaji utokanao na hisa za | Tengo la Ziada ya Jumla | Ziada ya Kisheria | Mengineyo IFRS9 | Hasara Kusanyiko | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwak** | | **29,237** | **6,236.30** | 282.84 | 211.14 | - | (17,220.07) | **18,747** |
| 1 | Mapatao mengine yaliyojumuishwa | | **2,283.60** | | | | | 2,284 |
| 2 | Tengo la ziada ya Jumla | | | 8.58 | | | (8.58) | (0) |
| 3 | Ziada Ya Kisheria | | | | (211.14) | | 211.14 | - |
| 4 | Mengineyo - ( IFRS -9) | | | | | (6,264.17) | | (6,264) |
| 5 | Faida /(Hasara) baada ya kodi ya mapatao | | | | | | 268 | 268 |
| 6 | Mengineyo | | | | | | | - |
| 7 | | | | | | | | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | | **29,237** | **8,520** | **291** | **-0** | **-6,264** | **-16,750** | **15,035** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | | |
| **Salio la Mwanzo wa Mwaka** | | 29,237 | 4,000.00 | 194.99 | | | (16,263.70) | 17,168 |
| 1 | Mapatao mengine yaliyojumuishwa | | 2,236.30 | | | | | **2,236** |
| 2 | Transfer to general Provision reserve | | | | | | | |
| 3 | Tengo la ziada ya Jumla | | | **87.85** | | | (87.85) | **0** |
| 4 | Ziada Ya Kisheria | | | | 211.14 | | (211.14) | **(0)** |
| 5 | Faida /(Hasara) baada ya kodi ya mapatao | | | | | | (657.37) | **(657)** |
| 6 | Mengineyo | | | | | | | - |
| 7 | | | | | | | | |
| **Salio la Mwisho wa Mwaka** | | **29,237** | **6,236.30** | **282.8** | **211.14** | - | **(17,220.07)** | **18,747** |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI TAREHE 31.12.2018
(Kiasi kwa millioni shilingi )

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-2018 | Mwaka wa uliopita 31-Dec-17 |
|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Riba | 10,271 | 10,424 |
| 2 | Gharama za Riba | (2,930) | (2,142) |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **7,341** | **8,282** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | 0 |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la Tengo katika Mikopo | (417) | (1,429) |
| **6** | **Mapato yasiyo na Riba** | **1,756** | **1,497** |
| | 6.1 Faida/(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | (16) | 32 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 1,221 | 746 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 551 | 720 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba** | **(8,376)** | **(8,973)** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | (4,522) | (5,228) |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | - | - |
| | 7.3 Gawio | (3,855) | (3,745) |
| **8** | **Faida / (Hasara) ya Uendeshaji** | **304** | **(622)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | (36) | (36) |
| **10** | **Faida / (Hasara) Hasili Baada ya Kodi ya Mapato** | **268** | **(658)** |
| 11 | Idadi ya Waajiriwa | 169 | 192 |
| 12 | Mapato kwa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| 13 | Mapato ya Hisa zilizochujwa | 0.00 | 0.00 |
| 14 | Idadi ya Matawi | 5 | 5 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1% | -2% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa fedha za wanahisa | 1% | -4% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 86% | 100% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazo Zalisha | 24% | 26% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA TAREHE 31.12.2018
(Kiasi kwa millioni shilingi )

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-2018 | Mwaka wa uliopita 31-Dec-17 |
|---|---|---|---|
| | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 304 | (622) |
| | **Marekebisho Kwa Ajili ya:** | | |
| | -Badiliko Halisi Katika Mikopo | 2,288 | 1,708 |
| | -Hasara Katika Mali za Kudumu | - | - |
| | -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji kabla ya Mabadiliko ya Mtajikazi** | **2,592** | **1,086** |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mikopo | (4,095) | (13,311) |
| | -Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali nyingine | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana | (1,138) | 7,160 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana za muda mfupi | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Amana Inayohitajika Kisheria | - | - |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (900) | 1,022 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,071 | (2,191) |
| | -Kodi iliyolipwa | (36) | (25) |
| | -Mengineyo | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uendeshaji** | **(1,507)** | **(6,260)** |
| **II.** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| | Gawiwo Lililopokelewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (253) | (492) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(253)** | **(492)** |
| **III.** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Madeni ya Muda Mrefu | 2,284 | 64 |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawiwo Lililipwa kwa Fedha Taslimu | 737 | 5,651 |
| | Mengineyo | - | - |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **3,020** | **5,715** |
| **IV.** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | | |
| | **Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu** | **1,260** | **(1,036)** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo mwaka | **4,315** | 5,670 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo mwaka** | **5,576** | **4,315** |

Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uendeshaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikuwa na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka sasa,

Sisi, tuliotajwa hapo juu chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benk na Taasisi za Fedha ya Mwaka 2006, nazinaonesha hali halisi.

| Signed by: | Saini | Tarehe | | Saini | Tarehe |
|---|---|---|---|---|---|
| **Thabit Ndilahomba**<br>Ofisa Mtendaji Mkuu | | 12/4/19 | **Simon Jengo**<br>Mwenyekiti wa Bodi | | 12/4/19 |
| **Andrew Tarimo**<br>Mkuu wa fedha | | 12/4/19 | **Dr. Ellen Okoedion**<br>Mkurugenzi Asiye Mtendaji | | 12/4/19 |
| **Rashid Sendoro**<br>Mkaguzi mkuu wa ndani | | 12/4/19 | | | |

215178802

# Utafiti viwango vya mishahara wapiga hatua

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema imefikia hatua nzuri katika mchakato wa kufanya utafiti unaolenga kuboresha zaidi viwango vya mishahara na maslahi kwa watumishi wa umma nchini.

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma), Dk. Francis Michael, wakati akifungua Baraza Kuu la Wafanyakazi la Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA), wilayani Bagamoyo mkoani Pwani baada ya baraza hilo kuiomba serikali kuboresha maslahi ya wafanyakazi wake.

Dk. Michael alisema Bodi ya Mishahara na Maslahi ya Watumishi wa Umma ambayo ilipewa kazi ya kufanya utafiti wa kuangalia viwango vya mishahara kutoka taasisi zote za serikali imeshamaliza kazi yake hiyo ya kufanya utafiti na kuiandikia ripoti.

"Mishahara iko tofauti kati ya taasisi moja ya umma na nyingine, na kwa kuwa zote ziko chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, ndiyo maana Bodi ya Mishahara ya Watumishi wa Umma imepewa kazi ya kuhakikisha inafanya utafiti na kutoa mapendekezo ambayo yanaweza kuboresha kwa usahihi tofauti hizo za viwango vya mishahara na maslahi ya watumishi kutoka katika taasisi hizo na kuangalia viwango ambavyo vinaweza kuwafaa na kuongeza tija kwa watumishi wa umma nchini," alisema na kuongeza:

"Bodi imekwishamaliza kazi hiyo na imeshaandika ripoti na kuiwasilisha, kwa hiyo kinachosubiriwa ni vikao halali ambavyo vinatakiwa vikae na kuijadili na baada ya hapo kupelekwa kwa Rais kwa ajili ya maamuzi na ninaamini kwamba kwa kuwa ripoti imeshaandikwa na kuwasilishwa, kazi hiyo imeshafikia katika hatua nzuri."

Mkurugenzi Mtendaji wa TPA, Deusdedit Kakoko, alisema miongoni mwa vigezo vikubwa vya mafanikio ambavyo wamejiwekea ni pamoja na kuhakikisha wanaongeza idadi ya shehena na meli bandarini na uzalishaji wa tija katika sehemu mbalimbali.



Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, akikagua gwaride kabla ya kufunga mafunzo ya kijeshi kwa askari 140 wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) katika kambi ya mafunzo ya kijeshi Mlele mkoani Katavi. **PICHA:WMU**

# NEMC yashauriwa kutumia umma kulinda mazingira

**Na Mwandishi Wetu,** RUFIJI

ELIMU kwa umma na ushirikishwaji wake vimetajwa kuwa ni mambo muhimu katika kulinda uhifadhi mazingira ya Tanzania kwa vizazi vya sasa na vijavyo.

Akifanya majumuisho ya ziara ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Baraza la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Mwenyekiti wa Bodi, Prof. Esnati Osinde Chaggu, alisema bodi itaihimiza NEMC kueneza elimu na mbinu za kulinda mazingira, ili jukumu la kulinda mazingira ya Tanzania liwe jepesi na endelevu.

"Maisha ya Watanzania na utajiri wao vinategemea mazingira salama huko wanakoishi na kufanya kazi zao. Mazingira lazima yalindwe," alisema na kuongeza: "Lakini watu watalinda kitu wanachoelewa faida zake na umuhimu wake. Kwa hiyo bodi italihimiza baraza kuwaelimisha wananchi juu ya faida ya kulinda na kuhifadhi mazingira."

Prof. Chaggu alifafanua kuwa ulinzi na uhifadhi wa mazingira ni suala shirikishi na kueleza kwamba pasipo kuwashirikisha na kuwaelimisha wananchi wakati wote, kazi ya kulinda mazingira haiwezi kufanikiwa vizuri kwa sababu watu katika shughuli zao za kila siku wanaweza kuhama au kudhuru mazingira hapo walipo. "Kwa hiyo elimu kwa umma ni jambo muhimu sana," alisisitiza.

Dk. Catherine Masao, mjumbe wa bodi na mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, alisema wajumbe wamejionea na kujifunza mambo mengi ikiwamo utayari wa wananchi waishio kando ya vyazo vya maji kupokea elimu juu ya uhifadhi wa mazingira na kuyalinda.

"Jukumu letu kama bodi ni kusimamia baraza kuratibu zoezi la utoaji wa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutunza mazingira na faida yake kwa maisha yao ya sasa na vizazi vijavyo," alisema Dk. Masao.

Alisema kuna kila sababu ya kuunganisha nguvu kutoka serikalini na wadau wa maendeleo katika kuhamasisha elimu ya mazingira ili jamii itambue umuhimu wa kutunza mazingira na faida zake katika maendeleo ya taifa na kuinua uchumi.

Alisema Tanzania itaondokana na ukame iwapo wananchi wataelimishwa umuhimu wa kutunza mazingira.

Akitumia mfano wa mradi wa umeme wa Stiegler's Gorge unaojengwa katika Bonde la Rufiji, Dk. Masao, alisema Mto Rufiji na bonde lake hupokea maji kutoka sehemu za mbali. Alifafanua, ni muhimu vyanzo vya maji yanayoingia katika bonde la Mto Rufiji vilindwe ili mradi wa umeme unaojengwa uwe salama na endelevu.

Damas Masologo, Mjumbe wa Bodi ya NEMC, alipongeza ziara ya wajumbe wa bodi na kusema imewajengea uwezo na kuwaweka katika nafasi nzuri ya kuishauri NEMC katika kutekeleza majukumu yake.

"Jambo la umuhimu sasa hivi ni kulinda vyanzo vyote vya maji vinavyomwaga maji katika Mto Rufiji ili mradi wa umeme upate maji unayoyahitaji wakati wote," alisema Masologo.

# Waziri awafunda wahitimu maliasili

**Na Mwandishi Wetu,** KATAVI

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Costantine Kanyasu, amewataka askari wa misitu waliohitimu mafunzo ya kijeshi kuhakikisha wanarejesha uoto wake wa asili katika maeneo yote ya misitu ambayo yameharibiwa.

Kanyasu alisema hayo alipokuwa akifunga mafunzo ya kijeshi kwa askari 140 wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) katika kambi ya mafunzo ya kijeshi Mlele mkoani Katavi.

"Leo mmehitimu na tumewaapisha, mmekuwa askari kweli wa TFS, lakini tambueni kuwa kazi za kiuchumi zinapelekea uharibifu mkubwa sana wa mazingira, na hatuwezi kusema zisiendelee. Zinatakiwa kuendelea katika namna ambayo haitaifanya nchi yetu kuwa jangwa.

"Kuhitimu kwenu hakumaanisha mnakwenda kuzuia maendeleo, kunamaanisha mnakwenda kushirikiana na wanaotaka maendeleo kwa kufanya kazi wakifikiria maendeleo endelevu," alisema.

Alisema kwa sasa nchi inakabiliwa na athari kubwa za mabadiliko ya tabinchi yanayosababishwa na uharibifu wa mazingira ikiwamo ukataji wa miti, ukame, mvua nyingi na mafuriko ambapo vyote hivyo husababishwa na matumizi mabaya ya kazi za kiuchumi.

Kanyasu alisema ni matarajio ya serikali baada ya askari hao kuhitimu pamoja na kazi yao ya msingi ya ulinzi watafanya kazi ya kuhakikisha wanarejesha uoto wa asili uliopotea.

Mtendaji Mkuu wa TFS, Prof. Dos Santos Silayo, alisema taifa limekuwa likikumbwa na changamoto mbalimbali za kiuhifadhi ikiwamo shughuli za kibinadamu pamoja na mmomonyoko wa maadili kwa watumishi na mambo yote hayo yanapelekea mafunzo hayo kuwa muhimu katika uhifadhi wa mapori na misitu ya hifadhi nchini.

# H'shauri yatofautiana na Takukuru madiwani kulipwa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), imebaini madiwani wote mkoani Manyara, wamelipwa kimakosa posho za vikao kwa miaka miwili, hivyo, imewaamuru kuzirejesha hadi ifikapo Juni, mwaka huu.

Hata hivyo, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, mwishoni mwa wiki, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Babati, Nicodemus Tarimo, alisema hakuna diwani anayelipwa posho zisizo halali badala yake wapo baadhi ya madiwani wanasahau kusaini kwenye daftari la mahudhurio.

"Ukiwaangalia kwenye muhtasari majina yao yapo, hayo ni makosa ya kawaida ya kibinadamu," alisema.

Alifafanua wanapotofautiana na Takukuru ni kuingilia posho za madiwani ambazo zipo kiuhalali na taasisi hiyo kuwakatalia wasilipwe posho za kujikimu kwa ajili ya malazi, wakati mwingine vikao humalizika usiku na hivyo kushindwa kusafiri. Katika hatua nyingine, alisema taasisi hiyo imefuatilia miradi ya maendeleo iliyopo mkoani hapa yenye thamani ya Sh. bilioni 20.6 na zimeokolewa Sh. 368,130,545.3 ambazo zingeweza kufanyiwa ubadhirifu.

Katika taarifa ya Takukuru kwa vyombo vya habari mwishoni mwa wiki, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya taasisi hiyo kuanzia Januari hadi Machi, 2019, iliyotolewa kwa waandishi wa habari, ilisema hawakubaini kila diwani alilipwa kiasi gani cha fedha kimakosa kama posho. Badala yake ilisema wamebaini madiwani wamekuwa wakilipwa posho zisizo halali kwa maana ya baadhi yao kulipwa posho za kujikimu kwa ajili ya kulala na wakati hawalali.

Aidha, alisema madiwani wamesharidhia kuwa walilipwa kimakosa na wameanza kulipa fedha hizo na kudai Halmashauri ya Simanjiro imeishalipa kiasi cha Sh. milioni 14 ambazo walilipwa na halmashauri hiyo kimakosa.

Taarifa hiyo iliyosainiwa na Naibu Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Isdory Kyando, iliwapa madiwani hao muda wa kuzirejesha fedha hizo hadi Juni, mwaka huu, ili zikafanye kazi za kuwaletea huduma za kijamii wananchi.

Kyando aliyataja madhara ambayo yanaweza kujitokeza iwapo madiwani wangeendelea kuzitafuna posho hizo kuwa ni pamoja na jamii kuzikosa huduma za kijamii ambazo zingeweza kutengenezwa kutokana na fedha hizo. Aidha, alisema kama madiwani watakuwa wanakubali kulipwa posho zisizo halali watashindwa kuwasimamia watumishi kuanzia mkurugenzi, kwa kuwa wao wana dhamana ya kuisimamia halmashauri yao.

"Katika tatizo hili tumeishakaa na watendaji wa halmashauri hasa wakurugenzi na kuwaambia waache kuwalipa posho zisizo halali na tukigundua wapo waliokuwa wanawalipa kwa makusudi tutawashughulikia na hata kutoa taarifa kwa waajiri wao," alisema.



Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Adam Kobelo, akizungumzia Sh. milioni 16 za elimu zilizochangwa na wananchi kwenye kikao cha Baraza la Mamlaka ya Mji huo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mwenyekiti UWT awafunda wahitimu kidato cha sita

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Umoja wa Wanawake wa CCM, Mkoa wa Arusha, Yasmin Bachu, amewapa hamasa wahitimu wa kidato cha sita kutumia elimu walioyoipata kama chachu ya kuwakomboa wenyewe na jamii inayowazunguka.

Alisema hayo wakati akizungumza katika mahafali ya 20 ya wanafunzi 154 wa kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Enaboishu iliyopo mjini hapa.

Alisema wanapaswa kutumia elimu hiyo kutatua changamoto mbalimbali katika jamii kwa kuwa ndiyo wanaotegemewa kuleta mabadiliko chanya.

Aidha, aliwataka wanafunzi hao kuhakikisha wanatoa elimu na kupinga vitendo viovu vya matumizi ya dawa za kulevya kwa vijana wenzao na kupiga vita unyanyasaji wa kijinsia ambao ndiyo umeshamiri katika jamii nyingi kutokana na mila na desturi zilizopo.

"Nawaombeni jamani mkawe mfano wa kuigwa, muwe mabalozi wazuri wa kubadilisha jamii kwa kutoa elimu kwa vijana wenzenu juu ya vitendo mbalimbali viovu, ili kupitia nyie tuweze kuona mabadiliko makubwa," alisema.

Kwa upande wake, Mkuu wa shule hiyo, Godwin John, alisema shule hiyo imekuwa ikiwaandaa wanafunzi kufanya vizuri ikiwamo kutoa motisha kwa wanafunzi wanaofanya vizuri pamoja na walimu ili kuongeza kiwango cha ufaulu zaidi shuleni hapo.

Hata hivyo, alisema shule hiyo imekuwa ikikabiliwa na changamoto ya ukosefu wa vioo vya vyumba vya madarasa, ukosefu wa madarasa, ulipaji ada wa kusuasa, hivyo kuwataka wazazi pamoja na walezi kuhakikisha wanawekeza zaidi kwa watoto wao kwa kuwa huo ndio urithi pekee unaotakiwa kutolewa kwa watoto.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo, Titi Mzava, aliwataka wanafunzi hao kutobweteka na elimu waliyoipata badala yake wakawe mfano bora wa kuigwa katika kujiendeleza kielimu na kuitangaza shule hiyo.

Aliwataka wanafunzi hao pindi wanaporejea mtaani wakawe chachu ya mabadiliko kwa vijana wenzao kupitia elimu hiyo waliyoipata.

## Mbunge apewa jukumu kutafuta gari la wagonjwa

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Babati imesema haina gari la kubebea wagonjwa wanaozidiwa kwa ajili ya kuwahishwa hospitali za rufani na kumtwisha mzigo huo mbunge kufanya machakato wa kupata gari hilo.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Nicodemus Tarimo, alisema hayo wakati akizungumza na Nipashe katika Kituo cha Afya Mamire baada ya kupokea msaada wa vifaa vya umeme wa nguvu ya jua na vifaa vingine vya kuwezesha upatikanaji wa huduma bora kwa mama wanaojifungulia kituo hicho uliotolewa na Shirika la So They Can kutoka nchini Australia.

Alisema miongoni mwa changamoto inayokikabili kituo hicho na halmashauri kwa upande wa huduma za afya ni ukosefu wa gari la kubebea wagonjwa wanaozidiwa.

Alisema maombi yameishatolewa kupitia kwa Mbunge wa Jimbo la Babati Vijijini, Vrajil Jituson, ili afikishe sehemu husika.

Alisema huduma ya afya kwa halmashauri hiyo ni nzuri na kwa sasa wana vituo vya afya vinane ambavyo vinatoa huduma na vingine serikali imeviboresha kwa kuvitengea fedha za kutosha ili vitoe huduma kwa wananchi.

Tarimo ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Mamire, alisema changamoto nyingine inayokikabili Kituo cha Afya Mamire ni tatizo la maji na kudai anadai halmashauri inalifanyia kazi kuona kama linaweza kuisha ili kuepusha adha kwa wagonjwa.

Mkazi wa Mamire, Amina Ramadhan, aliambia Nipashe kuwa kukosekana kwa gari la kubeba wagonjwa katika kituo hicho kunaweza kusababisha ongezeko la idadi ya wanawake wanaopoteza maisha kwa kushindwa kuwafikisha hospitali za rufani ili kupata matibabu kwa haraka.

Mkazi mwingine, Neema Sulle, aliiomba serikali kuipatia halmashauri hiyo gari la kubeba wagonjwa ambalo litakuwa msaada kwa wagonjwa watakaozidiwa.

# DC amtumbua Mkuu wa Shule kwa kushindwa kukemea ubakaji

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, 'amemng'oa' katika wadhifa wake Mkuu wa Shule ya Sekondari Sawe, Cecilia Kulaya, kwa kushindwa kuchukua hatua za awali za kukemea tukio la ubakaji na kupachikwa ujauzito mwanafunzi wa kidato cha nne katika shule hiyo mwenye umri wa miaka 17.

Mwanafunzi huyo anadaiwa kupewa ujauzito na makamu mkuu wa shule hiyo ambaye hivi sasa ametoroka kazini na kukimbilia kusikojulikana, baada ya kutekeleza tukio la ubakaji. Pia wanafunzi wengine wawili wamekatisha masomo mwaka huu shuleni hapo kwa ujauzito.

Ole Sabaya alifikia uamuzi huo mgumu wa kumwondoa shuleni hapo mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Shule hiyo, wakati alipokwenda kuzungumza na walimu na wananchi wa Kata ya Masama Mashariki.

"Tafadhali, mimi katika hili Mkurugenzi Mtendaji, mama sina cha kukusaidia, lakini nataka siku ya leo uondoke hapa shuleni. Huu utaratibu mwingine mtauchukua ninyi. Nakushukuru Ofisa Elimu Sekondari (Julius Kakyama) na wewe nikupongeze, jambo hili umelifanyia kazi vizuri kwa kusema ukweli. Watoto hawa ni wa kwenu, tunazungumza, tunamtafuta mhalifu wa ubakaji na ninyi wazazi mpo, mmeshindwa kumpata mtu aliyebaka na ni mwalimu?

"Mkuu wa shule, umeshindwa kuchukua tu hata hatua za awali kwa kuona kwamba hili jambo ni la ovyo na unalikemea? Na kazi zote nzuri za ujenzi hapa ulizozifanya ambazo naambiwa, katika hili umefeli, mimi sikuhitaji kwenye Shule ya Sekondari Sawe...Mazuri yako yote yamefunikwa na jambo hili, unaweza ukafaa mahali pengine."

Akionyesha kukerwa na jambo hilo, Ole Sabaya alisema anazo taarifa kwamba Makamu Mkuu wa shule aliyetekeleza tukio hilo, huwa anakwenda kwa wazazi kuzungumza na mwanafunzi huyo na anatuma fedha. "Mpaka pesa anatuma, anatumaje? Anatumaje pesa kwa yule mtoto ili asiseme au kumtaja kwamba amembaka, kwa mara nyingine OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya), nitafutieni huyo mtu, mkamateni mwekeni chini ya ulinzi, aende kujibu mashtaka ya ubakaji," aliagiza mkuu huyo wa wilaya.

Kabla ya kumng'oa Mkuu wa Shule, Sabaya alieleza kushangazwa kwake na kusuasua kwa Bodi ya shule hiyo kutangaza kujiuzulu kwa kushindwa kusimamia wajibu wao.

"Halafu bodi imeshindwa kusimamia shule yenu, mmeshindwa kusimamia wajibu wenu na mmeshindwa kuwawajibisha walimu wazembe walioshindwa kufanya wajibu wao. Mtoto anabakwa na mwalimu, Mwenyekiti (wa bodi) mtoto wako anabakwa na mwalimu au mtoto wenu, yuko mtaani, mwalimu amekaa hapa siku zote mpaka anakimbia. Mmeshindwa kuchukua wajibu wa kulinda heshima ya mwanafunzi, mmejiabisha sana," alisisitiza Ole Sabaya.



Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya (aliyekaa kwenye kiti), akizungumza na wanafunzi wa kike wa Shule ya Sekondari Sawe, muda mfupi baada ya kumwondoa shuleni hapo Mkuu wa Shule hiyo. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wilaya ya Hai kuja kivingine kiuchumi

**Na Godfrey Mushi,** HAI

WILAYA ya Hai, mkoani Kilimanjaro imewasha 'indiketa' ya kuashiria kuja kwa mabadiliko makubwa ya kiuchumi, baada ya serikali kutangaza mapendekezo yake ya kutekeleza miradi 10 mipya ya kimkakati ambayo itabadili sura ya Mji wa Bomang'ombe na kuongeza mapato ya ndani.

Mapendekezo hayo ya utekelezaji wa miradi hiyo yaliwasilishwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Yohana Sintoo katika Baraza la Madiwani na kisha kuungwa mkono kwa asilimia 100.

"Miaka huja na kupita, lakini katika muda wangu wa uongozi nitakaokuwa hapa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, sitasahaulika kirahisi kutokana na mikakati kabambe tunayoisuka kwa sasa kwa ajili ya kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani, na mikakati hii naamani itaacha kumbukumbu ambazo pengine hazitafutika kirahisi," alisema Sintoo.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, miradi hiyo ni ujenzi wa soko la kimataifa eneo la Kwasadala, ujenzi wa maduka makubwa ya kisasa (shopping mall) katika mji wa Bomang'ombe, ujenzi wa jengo la kitega uchumi katika eneo la kituo kikuu cha mabasi cha Bomang'ombe na soko la walaji Hai Mjini na ujenzi wa machinjio ya kisasa na kiwanda cha nyama Gezaulole.

Mingine ni ujenzi wa uwanja wa michezo (Hai Stadium) na maduka eneo la Bomani, uboreshaji wa masoko ya Mula, Kalali na Rundugai, uboreshaji wa vituo vya utalii vya Chemka na Nshara, uboreshaji wa kituo cha Redio cha Boma Hai Fm, ujenzi wa mabwawa makubwa ya umwagiliaji ya Boloti, Lambo, Kimashuku, Kwa Tito na Sanya Station.

Pia umo uboreshaji wa eneo la uwekezaji la Mashine Tools na kutafuta wawekezaji katika viwanja vinne vinavyomilikiwa na halmashauri katika eneo hilo.

Kabla ya Mkurugenzi Mtendaji kuitangaza miradi hiyo, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Dk. Joel Nkya, alisema kuna mapendekezo ya mipango mkakati imewasilishwa mbele yao na wanahitaji kuijadili na kuipitisha kwa kuwa wanaona ina manufaa kwa wilaya yao na wananchi wanaowaongoza.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mipango wa Halmashauri hiyo, Erick Marsham, alisema kama vipaumbele hivyo vitatekelezwa kwa haraka, ni wazi kuwa halmashauri hiyo itapata fedha nyingi kupitia vyanzo hivyo.

Katika mkutano huo pamoja na mambo mengine, Mkurugenzi huyo aliarifu baraza hilo kuwa Halmashauri ya Wilaya hiyo, imefanikiwa kupata tena hati safi kwa mara ya nne mfululizo.

"Tumeshapata hati safi mara nne mfululizo, siri kubwa ya mafanikio kwenye hati safi ni kujipanga kama timu, wataalamu na kuwa na ushirikiano mkubwa," alieleza.

# Polisi yachunguza wanafunzi kuwekwa kinyumba

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

POLISI mkoani Kilimanjaro imethibitisha kuanza uchunguzi wa tukio la wanafunzi wawili wa kike wa Shule ya Sekondari Kilimani, iliyopo eneo la Moshi Vijijini kuwekwa kinyumba kama 'wake' na mkazi mmoja wa Wilaya ya Hai.

Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi Hamisi Issah, ameeleza kuwa wanafunzi hao wamepelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Mawenzi kwa ajili ya kufanyiwa vipimo.

"Ni kweli hao wanafunzi wanaodaiwa kuwekwa kinyumba na mtu mmoja huko Wilaya ya Hai, tumewapeleka kufanyiwa vipimo kwanza na tumeshafungua jalada la uchunguzi," alisema kamanda huyo.

Wanafunzi hao wawili wa kike ni wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Kilimani iliyopo Kirua Vunjo, Marangu. Mmoja ana umri wa miaka 15 na mwingine miaka 19.

Kugunduliwa kwa tukio hilo la kuwekwa kinyumba kama wake za mkazi mmoja wa eneo la Kingereka 'B' katika Mji Mdogo wa Bomang'ombe kulitokana na taarifa hizo kuwafikia kamati ya malezi, makuzi na ulinzi wa mtoto ya Kata ya Bondeni.

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Kingereka B, Seif Mkambala, aliiambia Nipashe kuwa walifanikiwa kuwapata watoto hao baada ya kupata taarifa za awali kutoka kwa msamaria mwema katika eneo hilo.

Kwa upande wake, Exaud Massawe, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi wa Mtoto, alisema walipata taarifa kutoka kwa msamaria mwema mmoja ambaye aliwatonya kuwa kuna mtu anaishi na mabinti wawili kwenye nyumba moja iliyopo hapo Kingereka B.

Alisema baada ya kufuatilia wakiwa na mwenyekiti wa mtaa huo walifanikiwa kuwakuta mabinti hao wawili wakiwa na dada mmoja ambaye ni mwenyeji wao na kisha kuwapeleka katika ofisi ya mtaa huo kwa ajili ya mahojiano.

Katika maelezo yao, mabinti hao walidai ni wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kilimani, kidato cha pili na kwamba walikwenda Bomang'ombe kutafuta kazi, lakini waliishia kuishi na kijana mmoja waliyemtaja kwa jina.

"Tulifahamiana na kijana huyo kwa muda mrefu, yeye ana salon ya kiume ya kunyolea nywele katika eneo la Kirua Vunjo, Stendi ya Karumeli-Marangu. Alituahidi kuwa atatutafutia kazi mkoani Morogoro, lakini safari inatakiwa kuanzia wilayani Hai," alieleza mmoja wa wanafunzi hao.

Nipashe
# Spotika
NIPASHE JUMATATU APRILI 15, 2019



SAFARI YA SERENGETI BOYS KWENDA BRAZIL UK.18

## KATA FUNUA...



### ISIKUPITE

MOISE Kean ameweka rekodi ya kuwa mchezaji kinda zaidi kuweza kufumania nyavu katika mechi nne mfululizo za Ligi Kuu Italia, Serie A katika kipindi cha miaka 10, ambapo sasa anaipiku rekodi iliyokuwa ikishikiliwa na Mario Balotelli. Straika huyo wa Juventus, Kean amekuwa akifananishwa na Balotelli, ambaye alifunga katika mechi tatu mfululizo za Serie A mwaka 2009, aliipiku rekodi hiyo Jumamosi wakati akichezea kichapo cha mabao 2-1 ugenini dhidi ya SPAL.

Beki wa Manchester United, Phil Jones (chini), katika harakati za kumdhibiti mshambuliaji wa West Ham, Felipe Anderson, katika mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa Uwanja wa Old Trafford juzi na wenyeji kushinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**




# KWA NINI JUVENTUS HAITATWAA UEFA

**TURIN,** Italia

JUVENTUS inatarajia kushinda taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kwa mara ya nane mfululizo msimu huu.

Ikiwa na rekodi ya kushinda taji hilo mara 34 na lile la Coppa Italia mara 13, Juventus ndio klabu yenye mafanikio makubwa zaidi kwenye historia ya soka la Italia. Hata hivyo, pamoja na kutawala soka la nyumbani, 'Bianconeri' hao wameshindwa kutamba Ulaya.

Miamba hao wa Turin wameshinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mara mbili, lakini kwa mara ya mwisho ilishinda taji hilo mwaka 1997, hata hivyo kwa maumivu imepoteza katika fainali nne zilizopita.

Msimu huu, wameonyesha kuwa wapo imara na kuweza kutoka nyuma na kuiondoa Atletico Madrid katika raundi iliyopita ya hatua ya 16-bora.

Hata hivyo, msimu huu Juventus imekuwa na ndoto kubwa ya kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa msimu huu. Na hapa tunaangalia sababu tano kwa nini hawataweza kulitwaa taji hilo.

**5- Kuumia kwa Ronaldo**

Cristiano Ronaldo alikuwa nyota kwenye mchezo dhidi ya Atletico Madrid, akiwa ndio kinara aliyeiwezesha kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Wiki tatu baadaye mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alikuwa kwenye mechi za kimataifa akiichezea nchi yake.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or aliumia misuli ya nyama za paja na wakati wa mchezo wa kwanza wa robo fainali dhidi ya Ajax hakutarajiwa kuwa fiti, ingawa alicheza na kufunga bao moja, wakati wakilazimishwa sare ya 1-1.

**4. Wachezaji wachache wenye uzoefu kushinda Uefa**

Kikosi chote cha wachezaji cha Juventus ambacho kimeshinda mataji, hakuna wachezaji wenye uzoefu wa kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ingawa kwa sasa wachezaji kama Cristiano Ronaldo, Sami Khedira na Mario Mandzukic wameshaonja raha ya kulitwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, hata hivyo kushinda taji hilo kunahitaji kikosi cha wachezaji wasioshuka kiwango, lakini tatizo kubwa ni kwamba linapokuja suala la Ligi ya Mabingwa Ulaya, wachezaji wengi hawajalitwaa taji hilo.

Hatua hii ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya inaweza kuwa na nafasi nzuri kwa Juventus kusonga mbele kwenye nusu fainali, lakini ukweli ni kwamba, wachezaji wake hawana uzoefu wa kutosha.

Ni miaka 22, sasa tangu Juvetus imetwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, na nafasi hii imekuwa ikipewa nafasi kubwa kwamba inaweza kulitwaa taji hilo, lakini ukweli ni kwamba, nafasi hiyo ni ngumu kwao.

**3. Wanamtegemea zaidi Ronaldo**

Wakati Juventus ilipovunja benki kumsajili Ronaldo kipindi cha majira ya joto mwaka jana, matarajio yao makubwa ni kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku wakiamini kwamba Mreno huyo anaweza kutimiza ndoto zao za muda mrefu.

Ronaldo amejipambanua yeye mwenyewe kuwa mmoja wa wachezaji muhimu zaidi kwenye kikosi hicho, kwa sababu ana uzoefu mkubwa wa michuano hiyo.

Akiwa na mabao 124, aliyofunga kwenye michuano hiyo, Juventus wanamuona kama ndiye tegemea lao kubwa zaidi katika ndoto zao za kulitwaa taji hilo msimu huu.

Alikuwa msaada mkubwa kwa Juventus kwenye mchezo dhidi ya Altetico wakitoka nyuma kwa mabao 2-0 na wakafanikiwa kupata ushindi mzuri, huku yeye akifunga mabao matatu.

Na hilo ndio tatizo kubwa kwa Juventus, kwa sababu iwapo atashindwa kuwa kwenye kiwango chake, inamaanisha kwamba timu haitakuwa na uwezo wa kutapata matokeo mazuri.

**2. Historia ya hivi karibuni haiwapi nafasi**

Ni wazi kwamba Juventus kwa mara ya mwisho walishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 1997.

Lakini tangu wakati huo, wameshindwa kufanya lolote licha ya kutinga fainali na kushindwa kufungwa.

Real Madrid walitibua sherehe ya kulitwaa taji hilo kwenye fainali za mwaka 1998 na miaka 19 baadaye yaani mwaka 2017, huku AC Milan na Barcelona wakiwafunga pia kwenye fainali ya mwaka 2003 na ile ya mwaka 2015.

**1. Shinikizo kubwa**

Katika klabu zote zilizopo kwenye michuano hiyo, Juventus ndiyo yenye shinikizo kubwa ya kushinda taji hilo msimu huu.

Klabu hiyo imekuwa na hamu ya kushinda taji hilo kwa miaka kadhaa na sasa kwa uwepo wa Ronaldo kumeongeza zaidi shinikizo, kama kwa macho ya mashabiki na wasio na wasiwasi.

**JE, WAJUA?**

MANCHESTER United ndiyo timu inayoongoza kupata penalti nyingi zaidi (12) katika timu za Ligi Kuu msimu huu. Kadhalika, ndiyo idadi kubwa zaidi kwa 'Mashetani Wekundu' hao kuwahi kuzawadiwa kwa msimu mmoja.



MICHEZO

## NJE YA UWANJA




## VIDAL: MAN UTD CHANZO SARE VS HUESCA

**BARCELONA,** Hispania

KIUNGO wa Barcelona, Arturo Vidal, amekiri kuwa sare tasa waliyoipata Jumamosi kwenye La Liga dhidi ya Huesca, imetokana na kuathirika kwa kuiwaza Manchester United kuelekea mechi yao marudiano ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kocha Mkuu, Ernesto Valverde, alifanya mabadiliko ya wachezaji 10 kutoka timu iliyoichapa United bao 1-0 katika Uwanja wa Old Trafford, wakati wakiifuata timu hiyo inayoburuza mkia kwenye La Liga, na hawakuweza kupenyeza lango la wapinzani wao hao, hivyo kupata sare tasa.

Kadhalika, timu ya Barca iliyowachezesha kwa mara ya kwanza Moussa Wague na Jean-Clair Todibo, ilishindwa kupata shuti lililolenga lango katika kipindi cha pili, ingawa matokeo hayo yanaifanya kukaa kileleni kwa pointi 11 zaidi ya Atletico Madrid kwenye msimamo wa ligi.

Hata hivyo, Vidal anadhani kila mmoja katika klabu hiyo alikuwa akiiwaza United itakapowafuata Camp Nou kesho, ingawa pia anahisi mazingira hayakuwa rafiki kwa mfumo wa Barca.

"Wote tuliifikiria Manchester United, wale wote tuliokuwapo hapa na waliobaki nyumbani," aliiambia beIN SPORTS.

"Ilikuwa timu tofauti. Tuliwachezesha wale waliocheza mechi chache, na walifanya vizuri. Ilikuwa sare ya haki kwa pande zote.

"Mambo mengi yalitokea kwa sababu tulicheza kwa mfumo mpya, kwa kutumia wachezaji watatu nyuma. Uwanja ulikuwa mkavu, na mpira haukukimbia, pamoja na mambo mengine, lakini hatukupoteza, kitu ambacho kilikuwa muhimu."



Baadhi ya wachezaji wa timu ya soka ya Taifa Stars.

# USIYOYAJUA KUNDI C LA STARS AFCON 2019

**Na Adam Fungamwango**

TANZANIA imeangukia Kundi C, kwenye fainali za Mataifa ya Afrika zinazotarajiwa kufanyika Juni mwaka huu, nchini Misri.

Katika droo iliyochezeshwa Ijumaa usiku nchini Misri, imeifanya timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars kuangukia Kundi C, ikiwa na jirani zao Kenya, zote zikitoka Afrika Mashariki. Pamoja na Kenya, timu zingine zilizo kwenye Kundi C ni Algeria na Senegal, kitu ambacho kinaashiria kuwa siyo kundi la kitoto.

Shirikisho la Soka Afrika (Caf) limepanga makundi sita, huku kila kundi likiwa na timu nne, hivyo kutakuwa na timu 24 zikipambana kutafuta mbabe wa Afrika kwa mwaka 2019.

Mwenyeji wa michuano hiyo, Misri yupo kwenye Kundi A, akiwa na timu za Zimbabwe, Uganda na DR Congo, huku Kundi B likiwa na timu za Burundi, Madagascar, Guinea na Nigeria.

Kwenye Kundi D ipo Afrika Kusini, Namibia, Ivory Coast na Morocco na Kundi E kuna Angola, Mauritania, Mali na Tunisia, wakati Kundi F ambalo ndilo la mwisho likiundwa na Guinea Bissau, Benin, Ghana na Cameroon.

Mwandishi wa makala haya anazichambua timu za Kundi C zilipotoka hadi kuingia kwenye fainali hizo, pamoja na ushiriki wao miaka ya nyuma.

**1. Algeria**

Timu ya Taifa ya Algeria imetoka kwenye Kundi D yakiwa ni makundi ya awali kutafuta timu za kufuzu.

Ilikamata nafasi ya kwanza kwenye kundi hilo kwa kucheza mechi sita na kujikusanyia jumla ya pointi 11. Ilishinda mechi tatu, sare mbili na kupoteza mechi moja tu.

Ilifuatiwa na Benin ambayo nayo imefuzu ikiwa na pointi 10, huku timu za Gambia na Togo zikitupwa nje.

Imetwaa ubingwa wa Afcon mara moja, nayo ilikuwa ni mwaka 1990 yenyewe ikiwa ni mwenyeji.

Algeria imeshawahi kukutana na Taifa Stars kwenye michuano mbalimbali ya kimataifa mara 10, ikishinda mechi tano, sare nne na kufungwa mechi moja na Tanzania.

**2. Senegal**

Timu hii imetoka Kundi A wakati wa kinyang'anyiro cha kufuzu fainali hizo. Nayo vile vile ilikamata nafasi ya kwanza kwenye kundi lake ikijizolea pointi 16, ikishinda mechi tano, sare moja na haijafungwa hata mchezo mmoja kwenye hatua hiyo.

Timu iliyoifuatia ilikuwa ni Madagascar ambayo nayo imefuzu kwa kuzoa pointi 10, huku timu za Equatorial Guinea na Sudan zikiambuliwa patupu.

Hata hivyo, pamoja na kutisha kwake kote, ikiwa na wachezaji nyota wanaosakata kabumbu Ulaya, Senegal haijawahi kutwaa Kombe la Mataifa ya Afrika. Senegal imewahi kukutana na Taifa Stars mara mbili tu, na imeshinda mechi moja na kutoka sare moja.

**3. Kenya**

Harambee Stars, timu ya Taifa ya Kenya, ilikuwa kwenye Kundi F kwenye hatua za makundi kusaka tiketi ya Afcon. Ilishika nafasi ya pili kwenye kundi hilo ambalo liliongozwa na Ghana iliyomaliza ikiwa na pointi tisa, huku Kenya ikimaliza mechi nne ikiwa na pointi saba.

Ilishinda mechi mbili, na kutoa sare moja, ikapoteza mechi moja. Ikumbukwe kundi hili lilikuwa na timu tatu tu ambazo ni Ghana, Kenya, Ethiopia, huku Sierra Leone ikiondolewa kwenye michuano hiyo.

Kenya imekutana na Tanzania mara 48 kwenye michuano mbalimbali ya kimataifa, imeshinda mara 20, imetoa sare mara 14 na kupoteza 14 pia.

**4. Tanzania**

Taifa Stars, timu ambayo inafuzu mara ya pili baada ya kufanya hivyo awali mwaka 1979 na kushiriki fainali hizo 1980. Imefuzu ikiwa kwenye nafasi ya pili ya Kundi L lililokuwa na timu za Uganda, Lesotho na Cape Verde. Imemaliza mechi sita ikiwa na pointi nane, ikishinda mbili, sare mbili na kufungwa mechi mbili pia.

Kinara wa kundi alikuwa ni Uganda, aliyemaliza na pointi zake 13, huku timu za Lesotho na Cape Verde zikiambulia patupu.

Tanzania inaunda mlolongo wa timu nyingi ambazo hazijawahi kutwaa kombe hili, huku Burundi, Madagascar na Maurtania zikiweka rekodi ya kutinga Afcon kwa mara ya kwanza kwenye historia ya michuano hiyo.

Extra Time

## NUKUU

"Najisikia vibaya, na kukatishwa tamaa na tutakuwa kwenye wakati mgumu kwenye kipindi hiki cha mwishoni mwa msimu. Ni imani yetu si tatizo kubwa, lakini itachukua muda kurudi kwenye hali yake ya kawaida," **Tottenham Mauricio Pochettino akizungumzia majeraha ya Harry Kane baada ya kuumia kwenye mechi ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester City.**



"Inatuacha katika hali hii kwenye mechi ya marudiano, ila mara nyingine 1-0 inaweza kuwa bora kuliko 0-0 kwa sababu unajua dhahiri nini unatakiwa kufanya. Kwa 0-0, unajua kama unakwenda kushambulia ama kuzuia, lakini tunajua tunapaswa kufunga mabao. Tutachambua matokeo, lakini kwa sasa ninajisikia vizuri kuhusu namna tulivyocheza - tulitawala mchezo na pengine wiki ijayo hilo litakwenda kufanya kazi," **Pep Guardiola baada ya Manchester City kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Tottenham kwenye mechi ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Ulaya.**



"Pauni milioni 100 ni rahisi sana, katika soko la sasa ni rahisi sana. Tuliona kila bei nadhani katika soko la dirisha la usajili lililopita. Hivyo nadhani ni vigumu sana kumbadili Hazard na mchezaji mwingine. Siwezi kufanya lolote kumbakisha yeye, kwa sababu klabu imekubaliana naye, lakini kama Eden Hazard anataka kupata uzoefu mwingine, ni vigumu sana kumbakisha, nadhani tutajaribu kumshawishi, ila nadhani ninapaswa kuheshimu uamuzi wake," **Kocha wa Chelsea, Maurizio Sarri.**



# Nyota wa4 wanaoweza kubeba Ballon d'Or 2019

**PARIS,** Ufaransa

TUZO ya Ballon d'Or inabaki kuwa ndiyo kubwa zaidi kwa mchezaji binafsi kwenye soka duniani. Ni tuzo inayotoa utambuzi wa hali ya juu zaidi kwa mchezaji duniani na kuwa mwanasoka Bora wa Dunia, ikiwa inatolewa na Jarida la Soka Ufaransa. Tuzo hiyo ilikuwa imetawaliwa na Lionel Messi na Cristiano Ronaldo hadi Luka Modric alipovunja mwiko na kuitwaa mwaka jana.

Baada ya Messi na Ronaldo kushinda mara tano tuzo hii, ikatwaliwa na Modric, ambaye alishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid na aliiongoza Croatia kwenye fainali ya Kombe la Dunia. Modric alishinda Mpira wa Dhahabu kwenye Kombe la Dunia.

Hata hivyo, sasa inaonekana wazi kwamba tuzo hiyo itakuja kuchukuliwa na sura nyingine. Kwani Modric na Real Madrid yake tayari wapo nje ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na Kombe la Mfalme ('Copa Del Rey'). Huku wote, Ronaldo na Messi wakiendelea kuwa na kiwango cha juu licha ya kufikisha umri wa zaidi ya miaka 30.

Pamoja na yote, hapa tunaangalia majina ya wachezaji wanne ambao wanaweza kuitwaa tuzo ya Ballon d'Or mwishoni mwa mwaka huu.

**1. Lionel Messi**

Tangu kuanza kwa msimu wa 2018/19, mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina bado ameendelea kuonyesha kipaji chake kipo juu. Licha ya umri kuonekana kumtupa mkono, lakini nyota huyo wa Barcelona bado anaonekana ana nafasi nzuri zaidi msimu huu wa kutwaa mataji matatu.


Katika umri wake wa miaka 31, Messi kwa sasa ndiye anayeongoza kwa ufungaji mabao kwenye Ligi Kuu tano kubwa za Ulaya akiwa amefunga mabao 41 kwenye mashindano yote. Messi pia anaongoza kwenye mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu, akiwa amefunga mabao mengi zaidi kuliko mchezaji yeyote kwenye ligi tano za Ulaya.

Ndiye mchezaji anayeongoza kwa kufunga mabao kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, akiwa na mabao 31 na pia anaongoza kwenye ufungaji kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na mabao nane. Lakini ukweli ni kwamba, Messi anaongoza kwa kutoa pasi za mwisho, huku 14 zote zikitoka kwenye La Liga.

Hivyo, bado anaweza kushinda Ballon d'Or ya sita, maana uwezo bado anao.



Messi


Djik


Ronaldo


Mbappe

**2. Virgil Van Djik**

Pengine, huyu ndiye mchezaji ambaye jina lake si maarufu zaidi kwenye orodha hii, lakini anafanya makubwa zaidi pale Liverpool kwenye safu ya beki wa kati na huyu ni Virgil Van Dijk. Beki huyu wa Uholanzi anafurahia mafanikio yake kwa 'Wekundu' hao katika kiwango cha juu tangu alipojiunga na kikosi hicho cha kocha, Jurgen Klopp Januari mwaka jana.

Mara zote ni mara chache mno mabeki kuingia kwenye orodha ya kuwania tuzo kama hii, lakini Van Dijk anaonekana anaweza kutengeneza tofauti mwaka huu. Amekuwa kiongozi bora kwenye safu ya ulinzi na kuifanya Liverpool kuongoza katika msimamo wa Ligi Kuu kwa sasa, huku ikipata ushindani kutoka kwa Manchester City, ambao baada ya mechi ya jana sasa wote wameshuka dimbani mara 33.

Vijana hao wa Klopp tayari wamefuzu kucheza robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya kuitupa nje Bayern Munich kwenye hatua ya 16-Bora.

Lakini lolote linaweza kutokea na kujikuta akibeba tuzo hii na kumfanya kuwa katika mafanikio makubwa zaidi katika maisha yake ya uchezaji soka.

**3. Cristiano Ronaldo**

Tangu kutua kwake kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, kipindi cha majira ya joto, Ronaldo ameonyesha umahiri wake nchini Italia. Lakini kutokana na ligi hiyo kuchezwa zaidi kwa mtindo wa kuzuia, Ronaldo amejikuta kwenye wakati mgumu wa kufunga mabao mengi ikilinganishwa na mpinzani wake Messi.

Licha ya sasa Ronaldo kutokuwa na nafasi nyingi za kufunga, lakini si haba, kwani tayari ameshatikisha nyavu mara 19, huku akitoa pasi za mwisho nane kwenye Ligi Kuu. Na matokeo yake 'Kibibi Kizee' hicho cha Turin kinaongoza msimamo kwa tofauti ya pointi 15 wakifuatiwa na Napoli waliopo nafasi ya pili.

Ronaldo alionekana kuanza kwa ugumu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, wakati Juventus wakifungwa mabao 2-0 na Atletico Madrid, lakini wakafanikiwa kupindua matokeo kwenye mchezo wa marudio, wakati yeye akifunga mabao matatu peke yake, 'hat-trick' na kupindua matokeo na kuipeleka Juventus robo fainali.

Hivyo, kutokana na hili Ronaldo anajua umuhimu wa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwani ndiye yenye nafasi kubwa zaidi ya kuweza kutwaa tuzo ya Ballon d'Or, hivyo bado ana nafasi ya kuitwaa kwa mara ya sita.

**4. Kylian Mbappe**

Katika umri wake wa miaka 20, pengine ndiye mpinzani wa Messi kwenye ufungaji wa mabao katika ligi tano za Ulaya msimu huu. Mbappe yupo katika nafasi ya pili kwenye ufungaji wa mabao Ulaya akiwa na mabao 26 kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, katika mechi 23 akiwa na Paris Saint-Germain.

Mbappe pia ametoa pasi za mwisho 15 kwenye mashindano yote msimu huu, hivyo naye kujiweka kwenye nafasi nzuri katika mbio za kuwania tuzo hiyo.

Licha ya kutolewa na PSG kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Manchester United, bado nafasi yake ya kuwapo kwenye orodha hii ni kubwa kwake.

## Michezo



Baadhi ya wachezaji wa Serengeti Boys wakishangilia kwa staili ya aina yake kwenye moja kati ya mechi zao zilizofanyika Uwanja wa Taifa.

# SAFARI YA SERENGETI BOYS KWENDA BRAZIL

**Na Adam Fungamwango**

TANZANIA imeingia kwenye rekodi ya kuwa mwenyeji wa fainali za Mataifa ya Afrika kwa Vijana chini ya miaka 17 (Afcon U-17).

Michuano hiyo ilianza jana kwenye ardhi ya Tanzania na itachezwa kwenye viwanja vitatu vya Taifa, Azam Complex na Uhuru.

Michuano hiyo inayotarajia kumalizika Aprili 28, timu ya vijana ya Tanzania, Serengeti Boys inatabiriwa kufanya vizuri kutokana na kikosi bora ilichokuwa nacho na matokeo mazuri inayoyapata kwenye michuano mbalimbali hivi karibuni.

Watanzania wanawatizama vijana wa Serengeti Boys kuandika historia kwa kutwaa ubingwa kwa mara ya kwanza.

Endapo pia itafanya vyema kwenye michuano hiyo kwa kushinda mechi mbili tu, basi itafuzu moja kwa moja kushiriki michuano ya Kombe la Dunia la Vijana U-17 ambalo litafanyika mwaka huu nchini Brazil.

Hivi majuzi vijana hao wameahidiwa kitita cha Sh. milioni 20 kila mmoja iwapo itashinda mechi mbili tu ambazo zitawawezesha kutinga Kombe la Dunia la Vijana.

Ahadi hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa IPP, ambaye ni mlezi wa timu hiyo, Dk. Reginald Mengi na kutangazwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Ushindi, Paul Makonda ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam.

Serengeti ambayo inafundishwa na kocha Oscar Mirambo, imekuwa na rekodi ya kufanya vyema katika michezo yake tofauti hivi karibuni na kutokana na sapoti kubwa waliyonayo Watanzania kwa sasa juu ya timu zao za taifa, dhamira hiyo inaweza kufanikiwa.

Tanzania iko kwenye Kundi A, ikiwa na timu za Uganda, Angola na Nigeria, huku Kundi B likiwa na timu za Senegal, Morocco, Guinea na Cameroon.

Hebu tuziangazie timu zinazoshiriki michuano hiyo inayopigwa kwenye viwanja vya Taifa, Uhuru na Azam Complex.

**1. Uganda**

Uganda ni timu moja kati ya timu inayotabiriwa makubwa kwenye michuano hiyo. Ni kikosi kilichokamilika na kinachoonekana huenda ndicho kikwazo kikubwa kwa Tanzania kwa sababu ya kucheza mara kwa mara na kuwa ni timu zinazojuana.

Timu hiyo imefanikiwa kufika hapo baada ya kukamata nafasi ya pili kwenye Kundi B nyuma ya Ethiopia ambayo ndiyo ilikuwa kinara.

Ilicheza mechi nne, ikashinda tatu na kufungwa moja, huku ikijikusanyia jumla ya pointi tisa na kutinga hatua ya nusu fainali.

Nusu fainali ikaichapa Serengeti Boys mabao 3-1, kabla ya kuwa mabingwa wa michuano hiyo ya vijana na kukata tiketi ya kucheza fainali za Afcon kwa kuichapa Ethiopia mabao 3-1 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Agosti 26, mwaka jana nchini Tanzania.

**2. Angola**

Timu ya vijana ya Angola imefanikiwa kutinga hatua hiyo baada ya kushinda mechi zake zote tatu kwenye Kundi C.

Ilizifunga Malawi, Eswatini na Zimbawe na kujikusanyia jumla ya pointi tisa na kutinga hatua ya nusu fainali.

Kwenye hatua ya nusu fainali ikaifanyia umafia Namibia kwa kuitwanga mabao 7-0, kabla ya kuifunga Afrika Kusini bao 1-0 kwenye hatua ya fainali Julai 29, mwaka jana na kupata tiketi ya kusafiri nchini Tanzania kwa ajili ya Afcon.

**3. Nigeria**

Nigeria yenyewe ilicheza mechi mbili tu na kuweza kutinga hatua ya nusu fainali ikiwa pamoja na wenzao Ivory Coast kutoka Kundi B.

Zote zilikusanya pointi tatu na kwenda hatua hiyo kupambana na timu za kundi lingine. Wakati wenzao Ivory Coast wakitolewa na Ghana kwa mabao 2-0, Nigeria waliitwanga Niger mabao 2-1 na kutinga fainali.

Ilifanikiwa kukata tiketi ya Afcon baada ya kuifunga Ghana mabao 3-1 kwa mikwaju ya penalti kufuatia sare ya bao 1-1 kwa dakika 120.

**4. Tanzania**

Tanzania ilikuwa mwenyeji wa michuano ya kusaka tiketi ya Afcon ikizipokea timu za Kundi A na B ambazo mechi zake zilichezewa nchini Tanzania.

Lakini pia tayari kabla ya michuano hiyo, Tanzania ilikuwa imeshafuzu kwa sababu ndiyo waandaaji wa fainali hizo. Serengeti Boys ikawa kinara wa Kundi A baada ya kucheza mechi tatu, ikikusanya pointi tisa, huku ikifuatiwa na Rwanda iliyomaliza ikiwa ya pili kwa pointi sita.

Kwa bahati mbaya sana, timu zote mbili za Kundi A zilikwenda kutolewa hatua ya nusu fainali na timu zilizotoka Kundi B. Wakati Rwanda ikichapwa mabao 4-2 kwa mikwaju ya penalti baada ya sare ya mabao 2-2, Tanzania iliondoshwa kwa mabao 3-1 dhidi ya Uganda.

Timu zote za Kundi B ziliingia fainali na Uganda kushinda mabao 3-1, lakini Serengeti Boys ilicheza mechi ya kutafuta mshindi wa tatu dhidi ya Rwanda kwa kushinda kwa penalti 4-3, baada ya sare ya mabao 2-2.

**NAJUA WAJUA**

MANCHESTER United haijapoteza katika mechi 14 za Ligi Kuu ilizocheza uwanja wa nyumbani, (imeshinda 9 na sare 5) tangu ilipopoteza kwa mabao 3-0 dhidi ya Spurs Agosti mwaka jana. Ni Liverpool (37) na Arsenal (16) ndizo timu pekee kwa sasa ambazo zimecheza mechi nyingi nyumbani bila kupoteza kwa sasa katika ligi hiyo.

## MAKALA




# BARCELONA YA MIAKA 10 ILIYOPITA SIO HII

**LONDON,** England

WAKATI naangalia mechi ya wiki iliyopita kati ya Manchester United na Barcelona, kitu pekee ambacho kilikuwa kinakuja kwenye kichwa changu ni fainali ya Ligi ya Mabingwa barani Ulaya kati ya Barcelona na Arsenal.

Fainali ya moto, fainali ambayo iliwakutanisha watu ambao walikuwa wa moto. Watu ambao walikuwa na wajuaji kila upande.

Arsenal ilikuwa na majemedari haswaa! Ndicho kipindi ambacho Arsenal ilikuwa na Thierry Henry. Nyota ambaye aliacha alama kwenye mioyo ya mashabiki wa Arsenal.

Ndiyo, Arsenal ambayo ilikuwa na Robert Pires na ndiyo Arsenal ambayo ilikuwa ya mwisho mwisho kupata mafanikio makubwa barani Ulaya.

Tangu hapo hawakupata nafasi ya kufanya vizuri tena kwenye Ligi ya Mabingwa barani Ulaya kama ambavyo walifanya kipindi kile.

Inawezekana kabisa kadi nyekundu ya Jens Lehman iliwafanya watoke mchezoni siku ile. Iliwezekana kabisa kadi ile ilipunguza nguvu ndani ya kikosi cha Arsenal.

Kwa sababu tu, ilimbidi Robert Pires atoke ili kipa mpya aingie kwa ajili ya kuziba pengo la Jens Lehman ambaye alikuwa ametolewa kwa kadi nyekundu.

Yaani ndani ya dakika moja tu Arsenal ikawa imewakosa wachezaji wawili muhimu ndani ya kikosi chake, Robert Pires na Jens Lehman.

Hili lilikuwa pigo kubwa sana kwa kocha Arsene Wenger na hii inaweza ikawa sababu moja wapo ya Arsenal kupoteza ile mechi.

Lakini kuna sababu moja kubwa ambayo huwezi kuikwepa kabisa. Uimara wa kikosi cha Barcelona. Hapana shaka kwa kipindi hicho Barcelona ilikuwa imara sana.

Na hii ni moja ya sababu ambayo ilisababisha Barcelona washinde ile mechi. Hapa siongelei uwapo wa Ronaldinho ndani ya kikosi.

Ingawa huwezi kukwepa kabisa kuutambua uwezo binafsi wa Ronaldinho katika kuamua mechi ndani ya uwanja.

Lakini ninachojaribu kuongelea ni uwezo wa kitimu kiujumla wa Barcelona. Barcelona ilikuwa ni timu bora kiujumla kwa kipindi hicho.

Ndiyo maana fainali hii ilizikutanisha timu ambazo zilikuwa za moto kwa kipindi hicho (Arsenal na Barcelona).

Baada ya fainali hii timu zote mbili zilichagua njia mbili tofauti za kupita. Njia ambazo ziliwatofautisha sana kimafanikio.

Arsenal walichagua kurudi nyuma. Hawakutaka tena kabisa kutembea kwa kwenda mbele. Ila Barcelona walichagua kutembea kwa kwenda mbele.

Ndipo hapo walipomchukua Pep Guardiola kuwa kocha wao mkuu. Mabadiliko ambayo yalijenga jeshi ambalo lilikuwa na uwezo mkubwa wa kushinda kila vita.

Ndipo hapo tuliposhuhudia Barcelona ambayo ilikuwa imekamilika idara nyingi. Sehemu ya kiungo kulikuwapo na utatu mtakatifu.

Utatu uliokuwa umebeba majina ya Sergio, Iniesta na Xavi. Utatu ambao ulikuwa na uwezo wa kupiga pasi mpaka 300 kutoka miguuni mwao tu.

Utatu ambao ulikuwa unaitengeneza timu. Utatu ambao uliifanya Barcelona ionekane kama kituo cha kucheza.

Nani ambaye alikuwa anaichukia kuitazama Barcelona kipindi hicho? Barcelona ambayo kila muda ilikuwa inatamani kuwa na mpira mguuni.

Ilikuwa ngumu kushindana na Barcelona katika umiliki wa mpira, walihakikisha wanamiliki mpira, huku wakiupaka rangi kuhakikisha unakupendezesha machoni mwako.

Barcelona hii haipo tena. Haina uwezo tena wa kuhakikisha inacheza mpira unaovutia kama kipindi cha nyuma. Barcelona ya sasa imekuwa tofauti sana.


Haivutii kutazamika kama kipindi cha nyuma. Barcelona ambayo kwa muda mrefu inamtegemea Lionel Messi, yeye ndiye kila kitu kwa sasa tofauti na kipindi cha nyuma.

Yeye akikosekana timu inayumba. Imeshindwa kujitoa kwenye kivuli cha kumtegemea Messi kwa sasa. Imeshindwa kurudi kwenye nyakati zake.

Nyakati ambazo kila timu ilikuwa inaogopa kukutana nayo. Kwa sasa ukimtoa Messi kwenye kikosi cha Barcelona, inaonekana timu ya kawaida. Barcelona inaonekana hatari kwa sababu tu ina Messi kikosini.

**NDANI YA 18**

PAUL Pogba amefunga penalti saba msimu huu, ni Ruud van Nistelrooy pekee msimu wa 2002-03 (penalti 8) aliyefunga penalti nyingi zaidi kumshinda katika klabu ya Manchester United kwa msimu mmoja.





TUZO ya Ballon d'Or inabaki kuwa ndiyo kubwa zaidi kwa mchezaji binafsi kwenye soka duniani. Ni tuzo inay-otoa utambuzi wa hali ya juu zaidi kwa mchezaji duniani na kuwa mwanasoka Bora wa Dunia, ikiwa inatolewa na Jarida la Soka Ufaransa. Tuzo hiyo ilikuwa imetawaliwa na Lionel Messi na Cristiano Ronaldo hadi Luka Modric alipovunja mwiko na kuitwaa mwaka jana.

**Uk. 16-17**



Baadhi ya wachezaji wa Manchester United

# KLABU 3 ZINAZOWEZA KUTWAA 'NDOO' TATU

**LONDON,** England

KUSHINDA mataji matatu ni wakati ambao klabu inatwaa taji la Ligi Kuu, Kombe la Chama cha Soka katika nchi husika na lile la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Hii ni ndoto ya klabu nyingi Ulaya. Hata hivyo, kwa Ulaya ni timu tatu tu zimeweza kushinda mataji matatu kwa msimu hadi sasa.

Makala haya inaziangalia klabu tatu ambazo msimu huu zinaweza kutwaa mataji matatu...

**3. Manchester City**

Miamba hii ya Ligi Kuu England, tayari imeshinda Kombe la Ligi msimu huu na pia inaweza kumaliza msimu ikiwa na mataji matatu. City wapo kwenye fainali ya Kombe la FA, wapo kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na pia wapo kwenye mbio nzuri katika ubingwa wa Ligi Kuu.

Kwenye Kombe la FA, Man City walionekana kupenya kwa urahisi, walianza kuitoa Rotherham, Burnley na Newport City.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, City walipoteza mchezo wake wa kwanza nyumbani dhidi ya Lyon kabla ya kuangukia pua hatua ya robo fainali mchezo wa mkondo wa kwanza dhidi ya Tottenham. Hata hivyo, ndivyo vimebaki kuwa vipigo pekee kwao hadi sasa. Baada ya kuitoa Schalke kwenye hatua ya mtoano wa timu 16, City iliangukia kwa Tottenham na vijana hao wa Guardiola wakakutana na kipigo cha bao 1-0 na hivyo kwa sasa wanajipanga kwa ajili ya mchezo wa marudiano.

Hivyo, kama wakifanikiwa kupindua matokeo na kupata ushindi kwenye mchezo wa marudiano, watakuwa na nafasi ya kutinga nusu fainali na hatimaye fainali.

Kwenye Ligi Kuu ya England, wanashika nafasi ya pili wakiwa wamepitwa pointi mbili na Liverpool waliopo kileleni, lakini City wakiwa na mchezo mmoja mkononi. Hivyo chochote kinaweza kutokea kwao. Hivyo wao wana nafasi kubwa ya kulitwaa taji hilo msimu huu.

**2. Ajax Amsterdam**

Vijana hawa wa Kiholanzi wapo kwenye wakati mzuri zaidi kwa sasa, na wana nafasi nzuri zaidi ya kushinda mataji matatu msimu huu, kwani wamekuwa fiti katika kila michuano waliyoingia. Kocha Erik ten Hag amekuwa na kikosi chenye vijana wenye njaa ya mafanikio makubwa.

Ajax tayari wametinga fainali ya Kombe la KNVB na watacheza na Willem II Mei mwaka huu. Timu hizo mbili tayari zimekutana kwenye ligi mara mbili na zote Ajax walishinda, ikiwamo ushindi wa 4-1. Baada ya kufunga mabao 17 katika mechi tano na wanapewa nafasi ya kushinda taji hilo.

Kwenye ligi wana nafasi kubwa. Ajax kwa sasa wapo kileleni mwa msimamo wa ligi, lakini wakiongoza kwa tofauti ya mabao. PSV Eindhoven na Ajax zote zina pointi 71 kutoka katika mechi 29, lakini Ajax wanaongoza kwa tofauti ya mabao. Cha kufurahisha ni kwamba, Ajax imefunga mabao 106 katika mechi 30 kwenye ligi. Huku mechi nne zilizobaki kumalizika msimu huu, Ajax wana nafasi ya kulitwaa taji hilo.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mchezo wa kwanza wa robo fainali dhidi ya Juventus walitoka sare ya kufungana bao 1-1. Lakini waliweza kupindua matokeo dhidi ya Real Madrid, hivyo, Ajax wana nafasi ya kufanya hivyo dhidi ya Juventus kwao.

Kwa mara ya mwisho Ajax kushinda mataji matatu kwa msimu mmoja ilikuwa ni msimu wa mwaka 1971/72.

**1. Barcelona**

Barcelona, msimu huu wanaweza kushinda mataji matatu! Miamba hao wa Katalunya walishinda mataji matatu katika msimu wa 2008/09 na pia msimu wa 2014/15. Tangu hapo walikaribia kushinda mataji matatu, lakini hawakufanikiwa.

Mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, ni wazi ziko kwenye upande wao. Kwa sasa Barcelona wanaongoza msimamo wa ligi hiyo kwa tofauti ya pointi 11 kileleni, huku zikiwa zimebakia mechi sita ligi kumalizika. Wamekuwa kwenye kiwango kizuri zaidi msimu huu. Washindani wao wa karibu, Atletico Madrid wapo nafasi ya pili, huku Real Madrid wakiwa nafasi ya tatu. Na ni wazi kwamba timu hizo mbili hazina nafasi ya kuweza kutoa ushindani kwenye mbio za ubingwa wa ligi hiyo msimu huu.

Barcelona tayari wapo kwenye fainali ya Kombe la Mfalme ['Copa del Rey'] na watacheza na Valencia Mei mwaka huu. Timu hizi zimekutana mara mbili kwenye ligi na mara zote mechi hizo zilimalizika kwa sare. Lakini Barcelona wana nafasi kubwa zaidi ya kulibeba taji hilo.

Kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya, Barcelona walishinda mchezo wao wa kwanza kwa 1-0 dhidi ya Manchester United na sasa watarudiana wiki hii, na Barca wana nafasi kubwa zaidi ya kushinda na kusonga mbele.

**USILOLIJUA**

KIUNGO wa Tottenham, Christian Eriksen, amefikisha pasi za mwisho 60 kwenye Ligi Kuu England, ambazo ni nane zaidi kuliko mchezaji mwingine yeyote tangu alipoanza kuichezea klabu hiyo kwa mara ya kwanza Septemba 2013.





# HABARI MBEYA

## Wakulima wapata mikopo zaidi ya bil. 60/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKOPO wa zaidi ya Sh. bilioni 60 imechukuliwa kwa ajili ya kusaidia miradi mbalimbali ya viwanda na kilimo kwa wakulima wadogo na wa kati ili kuunga mkono sera ya kuifanya Tanzania ifikie uchumi wa kati.

Mkurugenzi wa Benki ya CRDB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Benson Mwakyusa, alisema wakati wa mkutano wa mwaka wa wanahisa ambao ulilenga kutoa elimu mbalimbali na kuwapa uelewa wa maendeleo ya benki yao.

Alisema lengo ni kuhakikisha wakulima na wananchi wanainuka kiuchumi kupitia mikopo inayotolewa na taasisi hiyo na kwamba mikopo hiyo ilikuwa inatolewa hasa kwa kuwapatia vifaa.

Mwakyusa alisema wakulima waliofaidika zaidi na mikopo hiyo ni wa mpunga hasa katika Wilaya ya Mbarali na wakulima wa tumbaku katika Wilaya ya Chunya na kwamba benki hiyo inaendelea kutoa mikopo kwenye maeneo mengine.

"Lengo kubwa la mikopo yetu kwa wakulima, wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo wadogo ni kuhakikisha wanainuka kiuchumi kama serikali ya awamu ya tano inavyotaka na kwa sababu tunakopesha zaidi vifaa dhamana yake wakati mwingine huwa ni vifaa vyenyewe," alisema Mwakyusa.

Meneja Mikopo wa CRDB kutoka Makao Makuu, Mussa Lwila, alisema biashara nyingi zimekuwa zikifa kutokana na wafanyabiashara kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusu biashara wanazotaka kufanya.

Alisema ili mtu aweze kuanzisha biashara endelevu ni lazima mwenyewe awe na uelewa nayo badala ya kuchukua mikopo na kuanza kufanya biashara kwa kuiga kutoka kwa mtu mwingine.

Lwila alisema kitendo cha mfanyabiashara kupata elimu inasaidia kuondoa changamoto za biashara aliyoianzisha kuweza kufa na kuendelea kurejesha marejesho ya mkopo aliyoukopa kutoka katika taasisi za kifedha.

Hata hivyo baadhi ya wanahisa walisema kuwa pamoja na benki ya CRDB kuwasaidia wakulima kwa kuwapa mikopo wanashauri kiwapo kitengo cha kuwatafutia masoko ya mazao yao ili wazalishe wakiwa na uhakika wa masoko.

Mmoja wa wanahisa hao, Catherine Ndawi, alisema wakulima wakitafutiwa masoko itasaidia kuzalisha mazao kwa wingi na kuwa na uhakika wa kurejesha mikopo yao katika taasisi hizo za kifedha kwa maelezo kuwa wengi wao wameshindwa kulipa madeni na kutelekeza mikopo hiyo.



Baadhi ya wananchi wa Kijiji cha Kikondo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakionyesha eneo la mpaka kati ya kijiji chao na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ambayo wanadai ilihamishwa na eneo lao kuchukuliwa bila kulipwa fidia. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wamwomba JPM kuingilia kati mgogoro wa ardhi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa Kijiji cha Kikondo, Kata ya Ilungu, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamemwomba Rais Dk. John Magufuli, kuingilia kati mgogoro kati ya kijiji chao na Hifadhi ya Taifa ya Kitulo ambao umedumu zaidi ya miaka 50 wakidai kuwa wanaporwa haki yao na kunyanyaswa.

Aidha, wamelilalamikia jopo la makatibu wakuu wanane waliofika katika kijiji hicho hivi karibuni kwa ajili ya kutekeleza maagizo ya Rais ya kumaliza migogoro ya hifadhi za taifa na vijiji 366 nchini na kudai makatibu hao walitoa taarifa za kupotosha kupitia vyombo vya habari kwa kusema hakuna mgogoro kati ya hifadhi na wananchi hao.

Wakizungumza na Nipashe kijijini hapo, wananchi hao walisema mgogoro huo umedumu kwa muda mrefu bila kupatiwa ufumbuzi na kwamba mwaka 2015 Rais Magufuli alipokuwa kwenye kampeni aliwaahidi kuwa atahakikisha anaumaliza mapema.

Mmoja wa wananchi hao, William Mponela, ambaye amewahi kuwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wa kijiji hicho, alisema mgogoro huo ulianza mwaka 1965 serikali ilipokuwa inaanzisha shamba la mifugo na ilichukua maeneo yao bila kuwalipa fidia. Alisema wakati huo wakazi wa eneo hilo walikuwa 26 na serikali iliahidi kuwalipa fidia ambayo ilikuwa haizidi senti tano, lakini haikutekeleza hali ambayo ilisababisha wananchi hao kuendelea kuongezeka na kufikia zaidi ya 2000, huku fidia ikipanda mpaka kufikia zaidi ya Sh. bilioni 1.8. "Mwaka 2007 Tanapa walianza kubomoa nyumba zetu bila kutulipa fidia na eneo lenyewe lina urefu wa kilomita 1.4, tunamwomba Rais atusaidie ili waturejeshee eneo letu maana hakuna wanachofanyia na sisi hatuna eneo la kulima," alisema Mponela.

Mponela alisema kwa sasa wananchi hao hawana eneo la kuwatosha kulima, kujenga wala kuchunga mifugo kwa madai kuwa mifugo ikiingia kwenye eneo hilo ambalo waliporwa na hifadhi inakamatwa na wanatozwa faini isiyopungua Sh. 100,000 kwa kila mfugo.

Agape Swalo ambaye pia ni mkazi wa kijiji hicho, alisema walianza kupata matumaini ya kurejeshewa eneo lao baada ya Rais kutangaza kuwa vijiji vyote 366 nchini ambavyo vilikuwa vinadaiwa kuwa vipo ndani ya hifadhi visiondolewe.

Alisema matumaini yao yalianza kufifia baada ya jopo la makatibu wakuu wa wizara nane kutembelea kijiji hicho na kutowashirikisha wananchi kisha kutoa taarifa kuwa hakuna mgogoro isipokuwa kijiji kipo kwenye chanzo cha Mto Ruaha.

Swalo alisema wananchi wa kijiji hicho ni vinara wa kutunza vyanzo vya maji kwa maelezo kuwa hawalimi wala kufanya shughuli yoyote kwenye maeneo ya vyanzo vya maji na badala yake wanapanda miti kwa ajili ya kuvitunza vyanzo hivyo.

"Makatibu hao walikuja hapa jioni sana wakitokea Makete, tulikuwa hatuna taarifa ya aina yoyote, lakini walipofika hapa walikuwa na maaskari ambao walikuwa wameshika bunduki na mabomu ya machozi, wananchi wote waliogopa na hakuna aliyesogea, tulisikia kwenye vyombo vya habari wakisema hatuna mgogoro na Tanapa," alisema Swalo.

Alisema taarifa iliyotolewa na makatibu hao ni ya upotoshaji na inalenga kuwanyima haki yao, huku akidai kuwa mgogoro huo hata Rais anaufahamu vizuri hivyo wanashangaa makatibu hao kutoa taarifa hizo.

Kwa upande wake, Sevelina Mahinya, alisema kwa sasa wanawake wa kijiji hicho wanakosa hata kuni za kupikia kwa madai kuwa hawaruhusiwi kwenda kuzitafuta kwenye eneo ambalo ni mali yao na kwamba wakikutwa wanapigwa na kutozwa faini kubwa.

# Wasichana 900 wakiri kufanyiwa ukatili

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

ZAIDI ya wasichana 900 katika Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya wanadaiwa kuwa wamefanyiwa ukatili wa kijinsia wakiwa na umri wa chini ya miaka 18, ambao umewasababishia madhara ikiwamo kukatisha masomo na kuambukizwa magonjwa ikiwamo virusi vya Ukimwi.

Mabinti hao wamebainika kufanyiwa ukatili huo baada ya asasi isiyo ya kiserikali ya Kiwohede, kuendesha mradi uitwao 'Sauti' wilayani humo uliolenga kuwapatia wasichana elimu ya afya ya uzazi, kuwaepusha na maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi na kuwainua kiuchumi.

Akizungumza katika Siku ya Jukwaa la Mabinti wilayani Kyela, Meneja wa Mradi wa Sauti wilayani Kyela, Baraka Mwaifunga, alisema kuwa mradi huo umefanikiwa kuwahoji mabinti 3847 kuhusu ukatili wa kijinsia.

Alisema kati ya mabinti waliohojiwa, 900 walibainika kuwa walishafanyiwa ukatili wa kijinsia na kuwasababishia madhara makubwa ikiwamo kukatisha masomo, kuambukizwa virusi vya Ukimwi na kupata mimba za utotoni.

"Mradi wetu wa Sauti umefanikiwa kuwahoji mabinti 3,847 na tukabaini kuwa kati yao mabinti 900 wamefanyiwa ukatili wa kijinsia na kupata madhara," alisema Mwaifunga.

Alisema kuwa baada ya kubaini ukatili huo, mradi ulijaribu kuwapatia huduma mbalimbali za kujikwamua na ukatili huo na ukafanikiwa kuwasaidia mabinti 250 kati yao.

Mwaifunga alisema mradi huo ulitoa huduma mbalimbali ikiwamo kuwawezesha kiuchumi na baadhi yao wamekuwa wakiwezeshwa kwa kila mmoja kupewa Sh. 70,000 kila baada ya miezi mitatu ili wazitumie kwa shughuli za ujasiriamali utakaowaingizia kipato halali.


Alisema kuwa mabinti hao pia wamepewa elimu ya ujasiriamali ambayo imewawezesha kutambua fursa za kiuchumi zilizopo kwenye maeneo yao na baadhi yao tayari wameanza kufanya biashara ndogondogo zinazowaingizia vipato halali.

"Tuligundua kuwa baadhi ya mabinti hawa wanafanyiwa ukatili kutokana na kutokuwa na kipato na wengine walikuwa wakifanya biashara haramu ya kuuza miili yao ndipo wapate riziki, mradi huu umewawezesha kwa kuwapa elimu ya ujasiriamali na kisha tukaanza kuwapatia mitaji kidogo," alisema Mwaifunga.

Wakitoa ushuhuda wa maisha yao na namna walivyofanyiwa ukatili, baadhi ya mabinti hao walisema kuwa walifanyiwa na ndugu zao wa karibu hasa baada ya wazazi wao kufariki dunia.

Agness Ndembo alisema yeye alilazimika kuanza majukumu ya kulea familia akiwa na umri mdogo, baada ya wazazi wake kufariki na kumwacha yeye na wadogo zake wanne waliokuwa wakimtegemea.

Alisema kuwa wakati wazazi wake wakifariki alikuwa anasoma kidato cha kwanza, lakini ikambidi aache masomo ili awalee wadogo zake ambao walikuwa ni wadogo na hawakuwa na msaada wowote kutoka kwa ndugu zake wa karibu.





# Wakulima asilimia 72 wamesajiliwa

**Na August Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesema hadi sasa asilimia 72 ya wakulima wa mazao nane ya biashara wameshasajiliwa ili waweze kupatiwa vitambulisho bure.

Hasunga alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini hapa, baada ya kupokea vifaa mbalimbali zikiwamo `tablets' 50 zitakazosaidia kusajili wakulima nchini. Alisema kuwa kuna tatizo kubwa la takwimu za wakulima na kwamba kutokana na hali hiyo, wizara imeanza kuwasajili ili watambulike mazao wanayolima, kwa ukubwa gani na wapo kwenye maeneo gani. "Umefika wakati mwafaka sasa mkulima kuwa na kitambulisho, hivyo kanzidata hii itaambatana na utoaji wa vitambulisho kwa wakulima ili watembee kifua mbele na ifikapo Juni mwaka huu, zoezi hili litakuwa limekamilika ili tujue tuna wakulima wangapi kwenye mazao yetu," alisema.

Alitaja mazao hayo kuwa ni pamba, miwa, korosho, kahawa, chai, pareto, alizeti na michikichi na hadi Machi 31, mwaka huu, wameshaandikishwa wakulima 1,274,337 sawa na asilimia 72.

Alisema lengo ni kuwafikia wakulima milioni 1.7 na kuzitaka bodi za mazao hayo zikamilishe kanzidata hiyo ili kujua wako wapi.

Hasunga alisema kwa sasa kuna mashamba 134 makubwa ya kahawa, pareto, mkonge, chai, pamba na korosho na alitaka kujua kama kuna mazao mengine ambayo yana mashamba makubwa, hivyo aliwaagiza kukamilisha usajili ili kujua mashamba hayo.

Alilishukuru Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo (UNDP), kwa kutoa vifaa hivyo kwa ajili ya kusaidia usajili wa wakulima nchini kitengo ambacho kitaongeza ubora na uhakika wakulima walipo. Aliwataka pia waongeze mtandao wa usajili wa kutumia mitandao ambayo itaunganishwa na simu, kompyuta na `tablets' ili kuhakikisha viongozi wakiwa mahali popote wanajua.

Alisema wizara imeweka malengo manne ya kukamilisha sheria kwa kuwa kulikuwa na sera pekee, ili sheria hiyo isaidie kuweka ardhi katika mipango mazuri. Awali, Mratibu wa Mpango wa Haraka wa Kusaidia Kuboresha Mikakati ya Wizara ya Kilimo (RARIS), kuhusiana na utekelezaji wa mradi wa RARIS, Dk. Oswald Mashindano, alisema imesaidia vifaa mbalimbali kwa lengo la kuhakikisha wizara inafanikiwa katika kusajili wakulima.

Naye, Mwakilishi Mkazi wa UNDP, Natalie Boucly, alisema wametoa vifaa hivyo kwa lengo la kusaidia serikali katika kampeni yake ya kusajili wakulima kwa kuwa takwimu ni muhimu katika uwekaji wa mipango endelevu.



Profesa Helmut Asche kutoka vyuo vikuu vya nchini Ujerumani, akitoa somo la kuhusu uchumi kwa wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, mwishoni mwa wiki, chuoni hapo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Viongozi wa dini watakiwa kubuni miradi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

VIONGOZI wa dini wameshauriwa kuwa wabunifu wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao, ili kutoa ajira kwa makundi mbalimbali nchini.

Ushauri huo ulitolewa na Katibu Mkuu wa Baraza la Waislamu Tanzania (Bakwata) Mkoa wa Dodoma, Khalid Swai, wakati wa mkutano wake na

viongozi wa dini uliofanyika katika Kata ya Babayu, wilayani Bahi, mkoani Dodoma.

Swai alishauri viongozi wa dini kuwa wabunifu wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao kwa kuanzisha miradi itakayowasaidia kuongeza vipato

na kutoa ajira kwa watu wote bila kujali itikadi ya dini.

Aliitaja miradi hiyo kuwa ni kujenga shule kuanzia ngazi ya awali hadi sekondari, pamoja na kujenga vyuo vya kati ambavyo vitasaidia kuwapa

ujuzi vijana wanaomaliza masomo ya elimu ya sekondari. Swai alisema kutokana na ujio wa makao makuu Dodoma wananchi wake wanatakiwa kuchangamkia fursa hiyo kwa kuanzisha miradi ya maendeleo ili kwenda na kasi ya ujio huo.

Aidha, kwa upande wa viongozi wa misikiti aliwataka kujenga uwazi wa taarifa za mapato yanayoingia kwenye maeneo ikiwa ni pamoja na sadaka zinazotolewa.

"Usiri wa kukosekana kwa taarifa hizo imekuwa ndio chanzo kikubwa cha migogoro katika maeneo mengi nchini na hatuwezi kumtafuta mchawi, tatizo hakuna uwazi wa taarifa katika eneo hilo," alisema.

Naye Katibu wa Bakwata Wilaya ya Bahi, Miraji Sufiani, alisema changamoto kubwa iliyopo kwa waumini wa dini hiyo ni kununua maeneo madogo ya ujenzi wa nyumba za ibada ambayo hayawezi kujenga miradi mingine ya maendeleo.

"Lakini kutokana na mabadiliko ya uongozi wetu wa Bakwata Mkoa kuja na wazo hili litasaidia kubadilika na kununua maeneo zaidi ili kuanzisha huduma zingine za kijamii," alisema.

Katibu Kata wa Babayu, Mohamed Msala, ambaye aliwakilisha serikali alisema wanawategemea viongozi wa dini kusaidia kuhimiza shughuli za maendeleo.

Msala alisema viongozi hao wana watu wengi wanaokutana nao, hivyo baadaya kuwahubiria neno la Mungu wanatakiwa kuongeza kuwajengea uwezo wa kiuchumi.

## Jiji la Dodoma lajipanga kuwa safi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

HALMASHAURI ya Jiji la Dodoma kupitia mradi wa uendelezaji miji ya kimkakati Tanzania (TSCP), imetoa pikipiki za magurudumu matatu na vifaa vya kutunzia uchafu ili kuhakikisha linakuwa safi.

Vifaa hivyo vina thamani ya Sh. milioni 28.4 ambavyo vitatumika kuzoa taka ngumu kwenye makazi na maeneo ya biashara.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alikabidhi pikipiki hizo jana kwa vikundi vitatu ambavyo ni Dodoma Youth Environmental Care and Sanitation Group cha Kata ya Kizota, Mshikamano Group-Nzuguni C, ambacho kinafanya kazi zake kwenye kata ya Nzuguni pamoja na Soft Chivwele Group cha Kata ya Miyuji.

Akizungumza kwenye makabidhiano hayo, Mahenge alisema kuwa kupatikana kwa vifaa hivyo ni juhudi mbalimbali zinazofanywa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma, ikiongozwa na Mkurugenzi wake Godwin Kunambi katika kuhakikisha jiji linakuwa katika mazingira safi na salama.

"Jiji la Dodoma ni lazima liwe la kisasa, tuna bahati kwamba tumepata fursa hiyo ya kujenga makao makuu ya nchi kwenye karne hii ya 21 ambayo imejaa teknolojia za kisasa, kwa hiyo tukitumia vizuri teknolojia tutakuwa na jiji la kisasa kuliko majiji mengine duniani," alisema Dk. Mahenge.

Alisisitiza vikundi hivyo visitumie pikipiki hizo kufanya biashara nyingine tofauti na kazi ya uzoaji taka katika kata mbalimbali za halmshauri ya jiji hilo, ikizingatiwa kuwa zimegharimiwa kwa fedha nyingi.

Aliagiza jiji hilo kuhakikisha shughuli za kilimo na ufugaji hazifanyiki katikati ya mji.


"Dodoma tunayo ardhi ya kutosha kufanya kilimo na ufugaji nje ya eneo la makao makuu ya nchi, ufugaji katikati ya mji unaweza kusababisha ajali, kwa hiyo ni marufuku na nimekwisha waagiza viongozi wote wanaohusika," alisisitiza.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, aliwataka wakazi wake kushirikiana kwa karibu na halmashauri ili kuhakikisha mazingira yote yanakuwa safi.

Aidha, aliwataka kujenga utamaduni wa kutoa fedha za tozo ya uzoaji taka kwa ajili ya kuviwezesha vikundi hivyo kufanya kazi hiyo ya uondoshaji kwa ufanisi mkubwa.

Hata hivyo, alisema bado kuna baadhi ya wananchi na taasisi hazitoi ushirikiano kwenye utoaji tozo za taka.

Naye, Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Ally Mfinanga, alivitahadharisha vikundi husika kuwa pikipiki hizo zinapaswa kuwa katika hali nzuri kwa kipindi chote cha matumizi na vinawajibu wa kulipa kodi stahiki za serikali zinazohusiana na uendeshaji wa pikipiki hizo.



## HABARI ZANZIBAR



Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohamed Baucha (kushoto), akimkabidhi Ilhilal General Hemed, mmoja wa washindi kupitia promosheni ya Zantel ya Tumia EzyPesa Ushinde mfano wa hundi yenye thamani ya shilingi milioni moja katika hafla iliyofanyika Unguja mwishoni mwa wiki, wanaoshuhudia pichani ni Meneja Bidhaa Kitengo cha EzyPesa, Leonard Kameta (kushoto) na Meneja wa Chapa ya Zantel, David Maisori. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Balozi Iddi ashangaa Z'bar kuagiza nazi nje

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, ameziagiza manispaa na halmashauri za wilaya Zanzibar kuimarisha vitalu kwa uzalishaji wa miche ya minazi na kusimamia kampeni ya upandaji wa miche hiyo kwenye maeneo ya wazi, ili Zanzibar irudi katika historia yake ya uzalishaji wa zao la nazi.

Alisema serikali itaendelea kutoa miche ya mikarafuu na minazi bila ya malipo kwa utaratibu maalum na wananchi watapaswa kuomba kupitia katika shehia na halmashauri husika na baadaye maombi yao kupelekwa Wizara ya Kilimo kwa hatua za kupatiwa miche hiyo.

Akizungumza katika Siku ya Upandaji Miti Kitaifa katika shamba la serikali la minazi lililopo Selemu, Wilaya ya Magharibi "A" Unguja, Balozi Iddi, alisema zao la nazi Zanzibar hivi sasa limepungua uzalishaji wake kwa miaka kadhaa na sasa bidhaa hiyo huagizwa kutoka nchi jirani.

Alisema hali halisi sasa inaonyesha mahitaji ya zao la nazi ni makubwa jambo ambalo halilingani na kasi ya uzalishaji wa zao hilo muhimu kwa uchumi wa taifa. Balozi Iddi alisema kwa mujibu wa Ripoti ya Sensa ya Miti ya mwaka 2013/ 2014, imekadiriwa uwapo wa miti ya minazi ipatayo milioni 3.4, tofauti ya minazi milioni 5.7 iliyowahi kuwapo mwaka 1993.

Alisema hali hiyo inatokana na kasi kubwa ya ukataji wa minazi kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa barabara, makazi, uchongaji wa vitu vya samani, maeneo ya kilimo pamoja matumizi mabaya ya misumeno ya moto iliyokwisha pigwa marufuku matumizi yake.

Aidha, alieleza kwamba hakuna mwananchi asiyeelewa umuhimu wa nazi kwa maisha na uchumi wa taifa kwa kipindi kirefu kutokana na ilivyokuwa ikizalisha bidhaa za mbata, mafuta ya nazi na kazi nyingine zinazotokana na usumba kama vile mazulia. Alisema kutokana na kupungua kwa idadi ya minazi, hali hiyo imesababisha kupanda kwa bei ya zao hilo pamoja na bidhaa zote zinazotokana na minazi. "Asilimia 95 ya zao la nazi huuzwa na kutumika katika masoko ya ndani ikiwamo madafu, makuti, mafuta ya nazi, nishati, mbao na kamba," alisema Balozi Iddi.

Alieleza kwamba hatua zinastahili kuchukuliwa kutokana na faida kubwa ya zao la nazi ili kuhakikisha hadhi ya zao hilo inaimarika kama ilivyokuwa katika miaka ya nyuma.

Balozi Iddi alisema katika kuimarisha zao hilo, serikali imeweka mkakati maalum ikiwamo kampeni ya upandaji minazi kitaifa, kuandaa mpango wa miaka 10 wa kuendeleza minazi pamoja na kutayarisha sera na sheria zinazosimamia maendeleo ya zao la nazi nchini. Akitoa taarifa ya kitaalamu ya upandaji minazi Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Maryam Juma Saadala, alisema miche 200,000 ya minazi itakuwa ikipandwa kila mwaka katika kampeni endelevu ya upandaji miti ya minazi.

Maryam alisema hatua hiyo inatokana na takwimu za uzalishaji wa mbata na mafuta ya nazi kupungua hadi kufikia tani 276 mwaka 2002 kutoka tani 1,684 za mbata na mafuta ya nazi mwaka 1984.

Alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kupitia Wizara ya Kilimo, imeshatumia jumla ya Sh. milioni 80 kwa ajili ya uzalishaji wa miche ya minazi ili kufanikisha kampeni hiyo ya upandaji ninazi.

Maryam alieleza kwamba katika msimu huu wa 2018 - 2019, jumla ya miche 4,520,850 imeshaoteshwa katika vitalu vya serikali pamoja na watu binafsi.

# WEMA yahimiza wazazi ufuatiliaji wanafunzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu Zanzibar (WEMA) imewataka wazazi kulea watoto kwa pamoja na kufuatilia maendeleo ya masomo yao kwa kushirikiana na walimu ili kuongeza kiwango cha ufaulu cha wanafunzi visiwani Zanzibar.

Wito huo ulitolewa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Simai Mohamed Said, alipokuwa akizungumza katika hafla ya kuwazawadia wanafunzi 50 waliofanya vizuri katika matokeo ya mtihani ya kidato cha nne katika shule za sekondari za Kijini na Matemwe Mbuyutende, Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Alisema iwapo wazazi watashirikiana na walimu katika kufuatilia maendeleo ya wanafunzi kiwango cha elimu kitaendelea kuimarika Zanzibar hasa vijijini badala ya majukumu yote kuachiwa walimu.

Simai alisema serikali imeamua kuimarisha miundombinu ya sekta ya elimu ikiwamo kujenga shule za ghorofa pamoja na kuondoa tatizo la upungufu wa madawati na kumpongeza Rais wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein kwa kuendelea kuimarisha sekta ya elimu Zanzibar. Aidha, alipongeza mradi wa huduma za jamii wa Best of Zanzibar kwa kutoa masomo ya ziada ya Kiingereza, Hesabati na Sayansi ambayo yamesaidia kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi wa Kijini na Matemwe Mbuyutende, kila mwaka.

Meneja mradi wa huduma za jamii wa Best of Zanzibar, Aminata Keita, alisema mradi huo umegawanyika sehemu tatu kutoa elimu ya afya na mazingira, kuinua kiwango cha ufaulu wa kutoa masomo ya ziada pamoja na kampeni ya kuvisha watoto viatu kuanzia wenye umri wa miaka minne mpaka minane katika shule hizo.

"Lengo letu ni kuona watoto hawa wanakwenda shule na viatu kwa ajili ya usalama wao, kuongeza ufanisi na kuinua ufaulu wa wanafunzi," alisema Aminata na kuongeza kuwa viatu 400 vitatolewa kwa wanafunzi na elimu ya maandalizi na darasa la kwanza katika Shule ya Kijini na Matemwe Mbuyutende, mwaka huu.

Kwa upande wake Ofisa Mradi wa Best of Zanzibar, Ali Suleiman Hamad, alisema kuwa mradi huo umeamua kuongeza walimu wa masomo ya ziada kutoka 10 mpaka 16 wa kufundisha masomo ya Sayansi, Hesabu na Kiingereza baada ya matunda kuanza kuonekana katika mradi huo.

Vijiji vya Kijini na Matemwe Mbuyutende vinakabiliwa na tatizo la umaskini kutokana na ardhi yake kuwa na mwamba wa mawe na kurudisha nyuma maendeleo ya wananchi na kuathiri mahitaji ya wanafunzi kama viatu na sale kabla ya kuanza kunufaika kupitia mradi huo.

# 'Watoto wa kike walindwe kuwaepusha na udhalilishaji'

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

WAZAZI na walezi wametakiwa kufuatilia mienendo ya watoto wa kike ili wapate malezi bora yatakayowaepusha na changamoto za udhalilishwaji wa kijinsia.

Rai hiyo ilitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Tunu Juma Kondo, wakati wa kujitambulisha kwa kamati tekelezaji ya UWT Wilaya ya Dimani kichama.

Alisema wazazi, walezi na jamii kwa ujumla wanatakiwa kuwa karibu na watoto wa kile ambao kwa sasa wanaishi katika mazingira hatarishi ya kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji vinavyowasababisha kuwakosesha haki zao za msingi zikiwamo elimu, uongozi na haki ya kuishi wakiwa huru.

Aliwataka kuhakikisha watoto kila wanapotoka kwenda shule na sehemu zingine za kijamii wakaguliwe mabegi yao ya shule kwa kuwa ni wengine wanaondoka na nguo za ziada na kwenda sehemu za starehe hali inayosababisha kufanyiwa vitendo vya udhalilishaji.

Alieleza kuwa jukumu la malezi ya watoto ni la kila mtu, hivyo pindi watoto wakionekana katika mazingira hatari wananchi wa mtaa husika wanatakiwa kuchukua hatua za kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi ama kwa wazazi husika.

Alisema kwamba kuna baadhi ya wanaume wasiokuwa na maadili mazuri wamekuwa chanzo cha kuwadanganya na kuwafanyia vitendo vya udhalilishaji watoto wa kike hasa wanaosoma shule za maandalizi na msingi, jambo ambalo ni kinyume na mila, desturi na utamaduni wa Kizanzibari.

Naibu Katibu Mkuu huyo, aliweka wazi kuwa CCM kupitia UWT Zanzibar itaendelea kulaani vitendo vyote visivyofaa vinavyokatisha malengo ya maendeleo ya wanawake nchini na kuishauri serikali ichukue hatua stahiki kwa wahalifu wote wa matukio ya udhalilishaji.

Akizungumzia uimarishaji wa CCM, aliwataka wanawake hao kulipa ada za uanachama kwa wakati ili kurahisisha mipango ya kiutendaji ya chama na jumuiya kwa ujumla.

Akizungumzia maandalizi ya uchaguzi mkuu ujao, aliwasihi kuendelea kuongeza wanachama wapya na waliotimiza umri wa kupiga kura kisheria kwa lengo la kuongeza jeshi la ushindi la CCM, litakalopambana na vita ya kisiasa na kukiletea ushindi chama mwaka 2020.

Naye Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Dimani, Hussein Ali Mjema, alisema chama kitaendelea kuwa karibu na jumuiya zote kwa lengo la kuongeza nguvu ya kuleta mabadiliko ya kweli ya kimaendeleo.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 15 April**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 16 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 17 April**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 18 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 19 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 20 April**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Night of terror
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 21 April**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 15 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 16 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 17 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Documentary
22:00 Kipindi Maalum: Tatu mzuka
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 18 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Kipindi Maalum: TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 19 April**
05:30 Uwanja wa Ma0zoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 20 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 21 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Illegal sisters
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Illegal sisters 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)

## EATV



UJENZI

LEO USIKU SAA 3:00



**JUMATATU**
11:00 DADAZ (live)
15:00 FUNGUKA
16:00 UTAKE
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 KURASA
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
21:00 UJENZI
21:30 5SPORTS LIVE
22:30 BONGO HITS

***Ujenzi*** *Fahamu mambo mbalimbali kuhusu ujenzi, mapambo ya nyumba nje na ndani, mitindo na teknolojia tofauti zitumikazo kwenye ujenzi.*

## eastafrica RADIO

*05:00 EA Breakfast*
*09:00 Supamix*
*12:00 Kipenga Xtra*
*13:00 Planet Bongo*
*16:00 EA Drive*
*20:00 Kipenga*
*21:00 The Cruise*

88.1FM DAR ES SALAAM

## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

**CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM**
**FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE**

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

# Waandamanaji Sudan walitaka jeshi kukabidhi madaraka

**KHARTOUM, Sudan**

WAANDAMANAJI nchini Sudan wamelitaka jeshi kukabidhi madaraka mara moja na bila masharti kwa serikali ya mpito ya kiraia.

Waandamanaji hao wametaka kuundwa kwa serikali ya kiraia haraka iwezekanavyo na bila masharti ambayo itatawala kwa muda wa miaka minne.

Pia wameeleza kuwa watabaki mitaani hadi pale madai yao yatakapofikiwa.

Wamesema hatua ya kukabidhi madaraka katika serikali ya kiraia itakuwa hatua ya kwanza kuelekea kwa kuanguka kwa utawala wa Rais aliyejiuzulu, Omar Al Bashir.

Tangu kujiuzulu kwa Rais Omar Bashir jeshi limeteua baraza la kijeshi ambalo limesema litatawala kwa muda wa miaka miwili wakati uchaguzi ukitayarishwa.

Baraza hilo lilikutana na ujumbe wa watayarishaji wa maandamano juzi.

Jeshi la Sudan lilimpindua Omar al-Bashir siku ya Alhamisi, na kufikisha mwisho wa miaka 30 ya utawala wake na kumweka chini ya kuzuizi nyumbani kwake katika mji mkuu wa Khartoum.

Waandamanaji wanahofu kwamba jeshi ambalo linadhibitiwa na wateule wa al-Bashir ambapo litang'ang'ania madarakani ama kumchagua mmoja kati yao kumrithi.

Umoja wa Falme za Kiarabu (UEA) umewataka Wasudan kufanya kazi kwa ajili ya kulinda uhalali na kuhakikisha mabadiliko ya amani ya madaraka yanakuwapo.

Mfalme wa Saudia, Salman, ameamuru misaada ya bidhaa za mafuta ya petroli ngano na dawa vipelekwa nchini Sudani.

Katika taarifa nyingine iliyotolewa jana, Saudi Arabia na UAE zilielezea uungaji wao mkono wa uwapo wa baraza la mpito nchini Sudani lililoundwa na jeshi.

***DW***



Wapiganaji wa Taliban wakiwa wamebeba silaha, kundi hilo limetangaza kuanza mashambulio licha ya kufanya mazungumzo ya kuleta amani na Marekani. **PICHA: ALLIANCE**

# Shambulizi laua mmoja, mwingine mahututi

**CANBERRA, Australia**

SHAMBULIZI la bunduki lililofanywa na mtu aliyekuwa ndani ya gari lililokuwa katika mwendo, nje ya nyumba ya starehe ambayo ni maarufu mjini Melbourne, Australia, lilisababisha mtu mmoja kufariki na mwingine kujeruhiwa.

Taarifa kutoka Jeshi la Polisi nchini humo zilieleza kuwa katika shambulio hilo raia wengine wawili walijeruhiwa.

Polisi wamesema kuwa risasi ilipigwa kutoka katika gari ikilenga umati wa watu waliokuwa wamesimama nje ya klabu hiyo ya starehe ya ghorofa mbili ijulikanayo kama klabu ya Love Machine na kuwaathiri walinzi watatu katika sehemu hiyo ya starehe na msimamizi mmoja wa klabu hiyo.

Polisi wametangaza kuwa mtu yeyote aliyekuwa na picha za video au taarifa kuhusu tukio hilo kujitokeza.

Hadi kufikia jana jioni hakuna mtu yeyote aliyekamatwa kuhusiana na tukio hilo.

Watu wanne waliojeruhiwa walipelekwa hospitali, wawili kati yao wakiwa mahututi.

Hata hivyo, Jeshi la Polisi baadaye walithibitisha kuwa mwanaume mmoja mwenye umri wa miaka 37, alipoteza maisha. Polisi nchini Australia wanaendelea na uchunguzi ili kujua iwapo gari aina ya Porsche SUV nyeusi iliyokuwa ikiondoka katika eneo hilo inahusika katika shambulizi hilo. Gari hilo baadaye lilipatikana likiwa limechomwa moto.

"Mambo haya yakustaajabisha bado ni nadra kutokea, na hakuna tetesi yoyote inayoonyesha hivi sasa kuwa tukio hili ni sehemu ya ajenda pana zaidi ya uhalifu," alisema Andrew Stamper ambaye ni msemaji wa Jeshi la Polisi Jimbo la Victoria.

Mmiliki wa Love Machine, Steve Yousif, aliandika katika mtandao wa Facebook: "Tumeelemewa na simu mlizotupigia na ujumbe wa simu mliotutumia, hakuna zaidi ila ni upendo wetu kwenu nyote."

"Kilichotokea jana usiku ni jambo ambalo halikustahili na limetushtua. Kwa baadhi yenu ilikuwa ni usiku wa starehe, kwa familia yote ya klabu ya Love Machine imepoteza mtu mwenye roho nzuri hivi leo," aliandika mmiliki huyo.

Uhalifu wa silaha ni nadra nchini Australia kutokea baada ya kuboresha sheria za udhibiti wa silaha kufuatia shambulizi lililofanywa na mtu mmoja mwenye bunduki mwaka 1996 huko katika mji wa Tasmania mwaka 1996, na kuua watu 35.

***VOA***

## Polisi watumwa kukabiliana na waandamanaji

**ALGERS, Algeria**

ALGERIA inaendelea kukumbwa na maandamano licha ya Rais wa nchi hiyo, Abdelaziz Bouteflika, kuchukuwa hatua ya kujiuzulu kwa shinikizo la maandamano.

Jana maeneo mbalimbali ya nchi hiyo yalitawaliwa na maandamano, huku Jeshi la Polisi wakikabiliana nao.

Waandamanaji wanaendelea kuomba kujiuzulu kwa utawala mzima wa Bouteflika.

Siku ya Alhamisi usiku, polisi wa kuzima ghasia walionekana wengi kuliko idadi ya waandamanaji wakijielekeza kwenye eneo la Posta Kuu katikati mwa mji wa Algiers.

Vikosi vya usalama vimeweka vizuizi barabarani, hasa kwenye barabara zinazoelekea mji mkuu wa nchi hiyo. Ni maandamano ya kwanza kutokea tangu kuteuliwa kwa Abdelkader Bensalah kama rais wa mpito wa Algeria.

Bensalah ni rafiki wa karibu wa Abdelaziz Bouteflika ambaye anajaribu kutuliza hasira ya wananchi wa Algeria.

Hata hivyo, waandamanaji wanataka kiongozi huyo, naye pia aweze kujiuzulu.

Kwa siku kadhaa Mkuu wa Majeshi wa Algeria, Ahmed Salah, amekuwa akijaribu kutuliza hasira ya waandamanaji, bila mafanikio.

**RFI**

## UN: Mapigano Libya yameua watu 121

**TRIPOLI, Libya**

MASHIRIKA ya Afya ya Umoja wa Mataifa yamesema mapigano yanayoendelea nchini Libya kati ya makundi hasimu ya wanamgambo yanayogombania udhibiti wa mji mkuu wa Tripoli yamesababisha vifo vya takriban watu 121.

Shirika la Afya Duniani WHO limesema kwamba watu wapatao 561 wamejeruhiwa tangu mashambulizi makubwa ya jeshi la kibinafsi LNA linaloongozwa na Khalifa Haftar yalipoanza Aprili 5. UN umesema mapema wiki hii kwamba watu zaidi ya 8,000 wamepoteza makazi yao kutokana na mapigano hayo.

Machafuko hayo yanatishia kuzua vita vya wenyewe kwa wenyewe kama vile vya mwaka 2011 ambavyo vilisababisha kuondoshwa madarakani na kuuawa kwa kiongozi wa muda mrefu wa nchi hiyo, Moammar Gadhafi.

**DW**

# Mbunge apigania madiwani posho

Na Augusta Njoji, DODOMA

SERIKALI imeombwa kuongeza posho kwa madiwani kwa mwaka wa fedha 2019/20 kutokana na kufanya kazi kubwa ya kuisaidia serikali kusogeza maendeleo kwa wananchi.

Ombi hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Mbunge wa Muheza (CCM), Adadi Rajabu (pichani), wakati akichangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) pamoja na Utawala Bora na Utumishi kwa mwaka wa fedha 2019/20.

Alisema madiwani wanafanya kazi kubwa na kwamba kuna haja posho zao kuandaliwa kwa umakini ili waweze kutimiza majukumu yao kwa weledi.

"Hawa ni viongozi muhimu sana katika utendaji kazi wa serikali na ndiyo walio jirani na wananchi, kwahiyo, kuna haja serikali iwalipe posho kwa sababu kufanya hivyo ni njia mojawapo ya kuwapa moyo wa kutimiza majukumu yao ya kila siku," alisema Rajabu.

Kuhusu miradi ya kimkakati, Adadi alisema kwa Halmashauri ya Muheza wanatarajia kujenga stendi kubwa ya kisasa na kuiomba serikali iwatengee fedha za utekelezaji.

Naye Mbunge wa Manyoni, Daniel Mtuka(CCM), aliiomba serikali kuiongezea nguvu kifedha, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa(TAKUKURU) kwa kuwa ina majukumu mengi ya kufanya.

Kwa upande wake, Mbunge wa Viti Maalum, Grace Kiwelu (Chadema), alimlalamikia Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai ole Sabaya, kwa kile alichosema kuwa anashiriki kuua vyama upinzani wilayani humo.

Alisema mkuu huyo amekuwa akiwalazimisha wenyeviti wa mitaa na vijiji wanaotokana na Chadema, kuandika barua za kujiuzulu nafasi zao ili kukidhoofisha chama.



# Gavana BoT: Elimu ya fedha, taarifa za mikopo ni muhimu

Na Mwandishi Wetu

GAVANA wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Prof. Florens Luoga, amesema elimu kuhusu masuala ya fedha ni muhimu katika mfumo mzima wa taarifa za mikopo ili kuwawezesha Watanzania kupanga matumizi bora ya mikopo.

Prof. Luoga alitoa kauli hiyo katika uzinduzi wa kampeni ya uelimishaji umma kuhusu taarifa za mikopo na fedha iliyoratibiwa na BoT kwa kushirikiana na taasisi ya International Finance Corporation ambayo ni mwanachama wa Kundi la Benki ya Dunia. Akizungumza kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mpango, Dk. Philip Mpango, Prof. Luoga alisema taarifa za mikopo na elimu ya fedha ni muhimu ili kuhakikisha Watanzania wanaondokana na matumizi ya anasa ya mikopo.

"Kampeni hii ya elimu kwa umma inalenga kuwaelimisha watumiaji wa huduma za fedha na wadau wengine kukuza uelewa wao kuhusu taarifa za mikopo ili kuongeza ushiriki katika matumizi ya taarifa za mikopo hapa nchini," alisema.

Meneja Msaidizi, Mfumo wa Kumbukumbu za Wakopaji kutoka BoT, Nkanwa Magina, alisema kampeni hiyo ya miezi mitatu inalenga kuongeza uelewa, mwamko kuhusu taarifa za mikopo na kukuza upatikanaji wa mikopo.

"Wadau hao wameahidi kusaidia kusambaza ujumbe kuhusu umuhimu wa upatikanaji wa mikopo na jinsi Watanzania wanavyoweza kuishi maisha bora kwa kuweza kupata taarifa za mikopo yao na kujua historia ya mikopo yao," alisema.

Alisema usimamizi mzuri wa mikopo na historia nzuri ya mikopo ni muhimu katika kuwezesha kupata mkopo nafuu.

"Kuhakiki taarifa yako ya mikopo mara moja kwa mwaka ni huduma inayopatikana bila malipo, tena itakuletea mafanikio kwa kukuandaa vema utakapoenda kuomba mkopo.

"Historia nzuri ya mikopo inaweza kusaidia kustahili viwango vya chini vya riba na ada, hivyo kuondokana na kutenga fedha kwa ajili ya dharura na gharama zisizotarajiwa," alisema.

Meneja wa IFC - Tanzania, Manuel Moses, alisema taarifa ya mikopo inaonyesha taarifa binafsi; utambulisho na taarifa ya mawasiliano na ikiwezekana historia ya ajira; idadi na aina za akaunti za mikopo.

Naye Meneja Maendeleo ya Biashara kutoka Dun & Bradstreet, Josephine Temu, alisema kuna taasisi mbili zilizopatiwa leseni na BoT kuandaa na kutoa taarifa za mikopo Tanzania.

Alisema taasisi hizo zinakusanya na kutunza taarifa za mikopo na kutoa taarifa za mikopo kwa kampuni au watu wanaozihitaji kama vile benki.

Alisema ripoti hiyo ya mikopo inaweza kutolewa na taasisi hizo (Creditinfo na Dun & Bradstreet) mara moja kwa mwaka bila malipo. Meneja Maendeleo ya Biashara kutoka Creditinfo, Tonny Missokia, alisema muhimu ni taarifa binafsi kama vile jina, hadhi ya ndoa, anwani, taarifa za ajira na namba za mawasiliano ni sahihi.



Mkurugenzi Mkuu wa TBL, Philip Redman (wa pili kushoto), akichangia mada wakati wa kongamano la kimataifa kuhusu ajira kwa vijana (AISEC) lililofanyika katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. Kushoto ni mtaalamu wa ajira wa ILO, Jealous Chirove, wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Trade Mark East Africa (TMEA), John Ulanga na (kulia) ni Mwanzilishi wa AISEC Tanzania, na Profesa wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Lettice Rutashobya. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Visima vya zamani maji Dar kufumuliwa

Na Frank Monyo

MAMLAKA ya Majisafi na Majitaka Dar es Salaam (DAWASA) imeanza mchakato wa kuvifufua na kuvirejesha visima vyote vilivyojengwa na serikali na kuachwa kwa muda mrefu bila kutumika kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa pembezoni mwa mji.

Aidha, wamiliki wote wenye visima binafsi na wanaofanya kazi ya kusambaza huduma ya maji kwa wananchi wametakiwa kusajiliwa na mamlaka hiyo na maji yao kupimwa kuangalia ubora kama yanafaa kwa matumizi ya binadamu ikiwamo na kuuza maji kwa bei elekezi ya Ewura ya 1,663.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, ndiye aliyetoa kauli hiyo jana, wakati wa ziara ya siku tatu ya kukagua miradi ya maji, jumuiya za watumia maji na kukagua ubora wa visima vya maji.

Alisema yapo maeneo ambayo hayana mtandao wa maji ya bomba kwa hiyo wameamua kuvifufua visima hivyo vilivyojengwa muda mrefu na serikali au wahisani, ili viweze kuhudumia wananchi wa maeneo hayo na yaliyo karibu.

"Ninapoongelea asilimia 85 ya wananchi wanaotumia majisafi na salama ndani ya mkoa wa Dar es Saalaam wanapata maji namaanisha na huduma hii ya visima, na lengo letu ni kuhakikisha kuwa ifikapo Juni 2020 watu wote wawe wanapata maji," alisema Luhemeja.

Aliongeza kuwa kwa kuanza utekelezaji eneo la Gezaulole na Vijibweni kuna visima ambavyo wameanza kuvifanyia tathmini na vinatarajia kuanza kutoa maji kwa wananchi wa maeneo hayo na yaliyo karibu nao muda wowote kuanzia sasa.

Hata hivyo, Mhandisi Luhemeja aliziagiza jumuiya za watumia maji kuwaunganishia maji wananchi kwa mkopo na kuingia nao mkataba wa kulipa ndani ya miezi sita hadi mwaka.

Msimamizi wa Miradi ya Pembezoni, Mhandisi Gonsalves Rutakyamirwa, alisema wanaendelea na tathmini ya kufahamu visima hivyo vina uwezo wa kuhudumia wananchi wa ngapi pamoja na kujenga tangi la kuhifadhi maji.

## MATANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu:+255 26 2324455
Fax: +255 26 232233
Barua Pepe ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe:13/04/2019

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe **16/04/2019** kampuni ya **M.M. CORP LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka Dar es salaam kuelekea Mlandizi, gari hilo lenye namba za usajili:

   **T 898 APY HORSE / T 933 AFZ**


2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 22.00
   Upana - mita 3.50
   Kimo - mita 4.80

3. **Njia itakayotumika:** Dar es salaam hadi Mlandizi kupitia Morogoro Road
   Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

   Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.

115178102

### VYETI VIMEPOTEA



**LAMECK LUCHAGULA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S1885-0074** cha BUGARAMA SEKONDARI mwaka 2013. Leaving Certificate kidato cha nne **index namba S1885-0074** cha BUGARAMA SEKONDARI mwaka 2013. Cheti cha JKT namba **AQ 7882** cha RWAMKOMA JKT, KJ 822 mwaka 2016. Cheti cha darasa la saba cha shule ya Msingi IGWAMANONI 'B' mwaka 2009. Cheti cha kuzaliwa namba 1453211 kilichotolewa mwaka 2012. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **UD/RB/7951/2018.**

115177602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI KWA MDAIWA**
**MAHAKAMA YA MWANZO NYANKUMBU**
**WILAYA YA GEITA**
**SHAURI LA MADAI NA: 9/2019**
**MDAI: TABITHA J. KADIKILO**
**DHIDI YA**
**MDAIWA: DANIEL JAMES WA TABORA**

**AMRI:**
Unaamriwa na mahakama uhudhurie hapa Mahakamani mnamo tarehe 16/4/2019 saa 2:30 Asubuhi bila kukosa.

Usipohudhuria shauri hili laweza kusikilizwa upande mmoja bila ya wewe kuwepo na kutolewa uamuzi.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na muhuri wa Mahakama leo Jumanne tarehe 5 mwezi wa 3, 2019.

XXXXXXXX

**IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL FOR GEITA AT GEITA**
**LAND APPLICATION.....03.......2019**
**MARTHA MWANZALIWA LUSHANGA**

**(Administrator of estate of late PETRO MWANZALIMA LUSHANGA...............APPLICANT**
**VERSUS**
MACKDONARD MIHAYO............... 1ST RESPONDENT
VERONICA LAURIAN.......................2ND RESPONDENT
HALIMA CHASAMA.........................3RD RESPONDENT
HUSSEN LUCHONGA.....................4TH RESPONDENT
SIMON FROLIUS MASIRI.................5TH RESPONDENT
JAPHAR MWALIMU.........................6TH RESPONDENT
SAVE UPON
HALIMA CHASAMA
HUSSEIN LUCHONGA **WHERE YOU ARE**
SIMON FROLIUS MASIRI
JAPHAR MWAI **NOTICE FOR MENTION OF YOUR CASE**

**NOW THEREFORE:** That the above case has been fixed for mention in the district land and housing tribunal of Geita at Geita on 16th April 2019 at 08:30 A.M. in the forenoon before honorable A.M. Kapinga Chairperson.

You may appear in person or by Advocate or Agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the necessary documents upon which you intend to rely upon to support your case.
**TAKE FATHER NOTICE THAT**: in your default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

Given under My hand and seal of the court this day 09 APRIL, 2018
**A.M. KAPINGA- CHAIRPERSON**

115178002


**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga Simu: 0767 223 311

***KWA MATANGAZO MADOGO, MADOGO***

***Tupigie 0767 223311***

**JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?**

**Nipashe**

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

***Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku***
***Tupigie 0767 223 311***

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



# SOLSKJAER APEWA MIL. 200 ZA USAJILI

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anatarajiwa kupewa bajeti kubwa kwa ajili ya kukijenga upya kikosi hicho wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Tangu kustaafu kwa Sir Alex Ferguson mwaka 2013, United imekuwa aikisuasua kuwania taji la Ligi Kuu, na wapo kwenye hatari ya kukosa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Maofisa wa klabu hiyo kwa sasa wanataka kuiona United inarudi kwenye zama zake na Gazeti la The Express limedai kuwa Solskjaer atapewa bajeti ya pauni milioni 200 kwa ajili ya kukijenga kikosi hicho.

Man United sasa itakuwa inasaka wachezaji wenye majina makubwa kwa ajili ya kurudisha hadhi yake ya kuwa kikosi cha ushindi.

Taarifa zaidi zinasema kwamba, Solskjaer katika orodha yake ya wachezaji anawaowania, nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho ndiye anayepewa nafasi kubwa zaidi na anaweza kuwagharimu pauni milioni 100.

Pia Man United wanatajwa kwamba wanamwania chipukizi wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, pamoja na mkali wa Crystal Palace, Aaron Wan-Bissaka na Declan Rice wa West Ham United.

Bejati hiyo pia itamsaidia Solskjaer kufanikisha ndoto yake ya kutaka kumsajili beki wa kati wa Napoli, Kalidou Koulibaly ambaye amekuwa akiwania na timu hiyo kwa udi na uvumba.




# KROOS KUMPISHA POGBA MADRID

**MADRID, Hispania**

KLABU ya Real Madrid itaangalia uwezekano wa kumtoa kiungo wa kati Mjerumani Toni Kroos mwenye umri wa miaka 29 msimu ujao ili kupata nafasi ya kumsajili, Paul Pogba.

Pogba ambaye anaichezea Klabu ya Manchester United kwa sasa akiwa na umri wa miaka 26, amekuwa akinyatiwa na miamba hao wa Hispania kwa muda mrefu.

Pia Madrid imetajwa kutaka kumsajili nyota wa Tottenham Hotspurs, Christian Eriksen raia wa Denmark.

Hata hivyo, wameanza mazungumzo ya awali kwa ajili ya kusaini mkataba na Eriksen mwenye umri wa miaka 27, na mkataba huo unaweza kugharimu zaidi ya euro milioni 100.

Lakini kocha wa Man United, Ole Gunnar Solskjaer, anasema kuwa kichwa cha Paul Pogba hakitageuzwa na Real Madrid, licha ya kumshawishi kwa mkataba unaoandaliwa kwa ajili yake wa pauni milioni 130.

# Valverde: Nimeridhishwa kiwango cha Barcelona

**BARCELONA, Hispania**

ERNESTO Valverde amesisitiza kwamba alikuwa na furaha kwa kiwango kilichoonyeshwa na timu yake, licha ya Barcelona kulazimishwa sare ya bila kufungana na SD Huesca juzi Jumamosi.

Huo ulikuwa ni mchezo wa Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, ambapo Barcelona walionekana kubanwa katika kila idara, licha ya kutengeneza mashambulizi kadhaa, ambayo hayakuzaa matunda.

Mabingwa hao wa Hispania wanaongoza msimamo kwa tofauti ya pointi 11 na walishindwa kupata pointi tatu.

Valverde baada ya mchezo huo alisema kwamba, licha ya kushindwa kupata pointi tatu kwenye mchezo huo, lakini ameridhika na kiwango kilichoonyeshwa na kikosi chake.

Huku sasa wakiwa wamebakia na mchezo wa pili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Manchester United, ambapo kwenye mchezo wa kwanza walishinda bao 1-0 na Valverde amesema: "Tuna furaha kwa sababu ulikuwa mchezo mgumu kwetu.

"Watu wengi wamekuja, lakini wanaelewa nini tulichotakiwa kukifanya. Sikuwa na tatizo na kiwango cha wachezaji, kwani walicheza katika ubora wao.

"Ingawa matokeo hayakuwa mazuri, lakini pointi moja kwetu ilikuwa ni muhimu zaidi, kwani imeendelea kutuweka kileleni mwa msimamo wa ligi.





# ZIDANE

## AMWASHIA TAA YA KIJANI BENZEMA

**MADRID, Hispania**

ZINEDINE Zidane amemhakikishia Raul de Tomas kurudi kuichezea Real Madrid akitokea Rayo Vallecano alikopelekwa kwa mkopo ili kuwa msaada kwa Karim Benzema msimu ujao.

Mhispania huyo msimu huu ameonyesha yupo kwenye kiwango cha juu na kumshawishi Zidane kumrudisha kwenye kikosi cha Madrid kwa ajili ya msimu ujao.

Kwa mujibu wa Gazeti la AS, kocha huyo Mfaransa yupo tayari kumrudisha mchezaji huyo ambaye alipelekwa kwa mara ya pili kucheza kwa mkopo ili aje kumsaidia Benzema, kama klabu hiyo haitamsajili mshambuliaji mwingine wakati wa kipindi cha majira ya joto.

Wakati wa kipindi chake akiwa na klabu hiyo mwaka 2017, De Tomas alifunga mabao 24 na kuweza kumaliza nafasi ya pili kwenye orodha ya wafungaji bora kwenye La Liga, huku pia akifunga hat trick tatu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 kuongeza mkataba wake na Madrid na kumfanya kuwa hapo Santiago Bernabeu hadi mwaka 2023, hivyo wakamwongeza mwaka mwingine wa kucheza kwa mkopo pale Rayo.

Msimu huu, mchezaji huyo amefunga mabao 14 kwenye mashindano yote aliyoichezea timu yake na hivyo amemshawishi Zidane, ambaye alifanya naye kazi msimu wa 2014/15.

# Oblak ampandisha mzuka Simeone

**MADRID, Hispania**

DIEGO Simeone amemsifia Jan Oblak kama golikipa bora duniani wakati akiisaidia Atletico Madrid kupata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Celta Vigo kwenye dimba la Wanda Metropolitano.

Kikosi hicho kikicheza nyumbani kilikuwa na presha kubwa, na Oblak aliokoa michomo mingi ya hatari.

Antoine Griezmann aliiweka mbele Altetico kwa shuti la adhabu ndogo umbali wa yadi 20 na mpira ukajaa kwenye vyavu za juu katika kipindi cha kwanza.

Halafu Alvaro Morata akaongeza bao la pili na kuihakikishia timu hiyo kupata ushindi wa mabao 2-0.

Akizungumza na waandishi wa habari mara baada ya mchezo huo, Simeone alisisitiza kwamba, Oblak ni golikipa bora duniani kwa sasa baada ya kuonyesha kiwango cha juu kwenye mchezo huo.

Alisema: "Yeye ni golikipa bora duniani kwa sasa, alicheza kwa umakini mkubwa na aliokoa hatari nyingi langoni kwetu.

"Tunabahati kwamba alichagua kuichezea Atletico. Amejiimarisha kwa kiasi kikubwa kama golikipa bora kwa sasa, na kwa uhakika ni msaada mkubwa kwa kikosi chetu kwa sasa."



# Pacquiao aanza kumpika mwanawe, mamaye alia

**MANILA, Ufilipino**

BINGWA wa dunia wa masumbwi anayetajwa kuwa bondia bora wa muda wote, Manny Pacquiao, ameanza kumpika mwanawe Jimuel anayetaka kuingia rasmi ulingoni.

Jimuel mwenye umri wa miaka 18, ameanza rasmi mafunzo ya mchezo huo, huku mama yake akimsihi kuachana na kazi hiyo kutokana na namna ambavyo ni hatari kwa maisha ya wachezaji.

Pacquiao amelazimika kuanza kumpa mafunzo hayo baada ya Jimuel kusisitiza kuwa anaupenda mchezo huo kutoka ndani ya nafsi yake.

Mke wa Pacquiao, Jinkees ameeleza kuwa alitokwa machozi baada ya kusikia mwanawe ameamua kuingia kwenye mchezo wa masumbwi na hata kuanza kushiriki ngumi za ridhaa, akishinda pambano lake la kwanza. "Nilipokuwa nawaangalia, nilitokwa machozi. Mwanangu anataka kweli kuwa bondia. Nilimwambia mwanangu acha ni mchezo hatari, baba yako aliingia huko kwa sababu ya umaskini tu, lakini alisisitiza anataka kucheza kama baba yake," Jinkees ameandika kwenye Instagram akiambatisha na picha ya Pacquiao akimfua Jimuel.

Pacquiao ambaye sasa ana umri wa miaka 40, hivi karibuni alishinda pambano lake la 70 dhidi ya bondia machachari kijana, Adrian Broner. Mwanawe anataka kuwa na uwezo wa kuiwakilisha nchi yake kama baba yake.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: KABLA SIJAFA NITAFANYA KAZI NYINGINE

Miaka 71 kama Roy Hodgson? Sitarajii kufundisha katika umri mkubwa, naiona miaka michache imebaki...

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, anaamini kwamba itakuwa ngumu kwake kufikia rekodi ya Kocha wa Crystal Palace, Roy Hodgson na kubakia kwenye utawala wa soka hadi umri wa miaka 71.

Hodgson na Palace yake walicheza jana, Jumapili na vijana wa Guardiola, saa mbili kabla ya vinara wa Ligi Kuu, Liverpool kuwakaribisha Chelsea kwenye dimba la Anfield.

Mbio za ubingwa wa Ligi Kuu msimu huu wa 2018-19 zinaonekana kama ngumu, huku Man City ambao ni mabingwa watetezi wakitaka kulitwaa taji hilo.

Hodgson amebakia kuwa kocha mwenye umri mkubwa zaidi kuongoza timu kwenye Ligi Kuu England, lakini Guardiola hana mpango wa kuendelea kubakia kwenye uongozi wa soka kama kocha huyo wa zamani wa England.

"Kwa upande wangu? Hapana. Haiwezekani. Roy Hodgson anapenda hali hiyo. Kwa kile kinachotokea kwa upande wake ni kwa sababu ana mapenzi ya soka, lakini mimi hapana," alisema kocha huyo mwenye umri wa miaka 48 wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari.

"Ni vizuri kumuona akiendelea kufundisha kwenye umri wake.

"Nina hamu ya kufanya mambo mengine kabla ya kufa. Napenda kazi yangu, lakini mara zote huwa nafikiri kufanya jambo jingine. Kuna mke wangu na familia. Miaka 71? Hapana.

"Unatakiwa kuwa na nguvu ya ziada na nafikiri kwa umri wa miaka 71, namheshimu Roy Hodgson kwani wengine hawawezi.

"Hapana. Nina umri wa miaka 48, kufika miaka 71 ni kazi. Ni miaka mingi. Sifikirii kama nitapenda kuwa kwenye umri huo niendelea kuwa kocha na sina mipango hiyo. Nimejifunza kwamba maisha ni uamuzi wako muda wote.

"Nitafanya mambo mengine. Ingawa sijaamua nini cha kufanya, lakini katika umri huo huwezi kunikuta nikiwa kwenye benchi la ukocha. Misimu yangu 10 ilikuwa na mafanikio makubwa kwenye soka na ilikuwa ya kuvutia.

"Sitarajii kuendelea kufundisha katika umri mkubwa, na kwa sasa naiona miaka michache imebaki mimi kuendelea kuwa kwenye nafasi hii. Kwani nataka kupata changamoto mpya."

Guardiola amejijengea heshima kwa kutwaa mataji katika klabu za Barcelona, Bayern Munich na sasa akiwa na City.

## KWA UFUPI

### SOLKSJAER KUPEWA JEURI SOKONI

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solksjaer atapewa fungu litakaloweka rekodi katika klabu hiyo, kiasi cha pauni milioni 200 kwa ajili ya kufanya usajili majira ya joto. ***(Sunday Express)***

### ICARDI AWEKWA SOKONI INTER

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Muargentina Mauro Icardi, 26, anaweza kuondoka kwa pauni milioni 52. ***(As.com)***

### FABREGAS AMTAJA JORGINHO CHELSEA

KIUNGO wa Monaco, Cesc Fabregas, 31, amedai aliondoka Chelsea Januari kwa sababu aliamini kocha aliyetua Maurizio Sarri alivutiwa zaidi na Jorginho, ambaye alisema Mtaliano huyo alikuwa kama "mtoto" kwake tangu wakiwa Napoli. ***(Mirror)***

### WAN-BISSAKA LULU UNITED, CITY

MANCHESTER United itatoa upinzani kwa mahasimu zao, Manchester City katika mbio za kuipata saini ya beki wa Crystal Palace, anayethaminishwa na pauni milioni 40, Aaron Wan-Bissaka, 21. (Daily Mail)

### ERIKSEN APANDIWA DAU UNITED

MANCHESTER United itamlipa Christian Eriksen, 27, mara tatu ya mshahara anaolipwa kwa sasa Tottenham endapo kiungo huyo atajiunga na klabu hiyo majira ya joto. ***(Mirror)***

### BARCA KUMRUDIA TENA WILLIAN

Barcelona inaweza kujaribu tena mchakato wa kumsajili winga wa Chelsea, Willian. Miamba hiyo ya La Liga hivi karibuni iliweka mezani ofa kiasi cha pauni milioni 55 kwa Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 30, ambazo zilikataliwa. ***(Sunday Telegraph)***

### GOMEZ MTEGONI TOTTENHAM

Tottenham inamfuatilia straika wa Celta Vigo, raia wa Uruguay, Maxi Gomez, 22, ambaye mkataba wake unamruhusu kuuvunja kwa pauni milioni 43.5, na anataka kucheza michuano ya Ulaya. ***(Mail on Sunday)***

### DYBALA KUMPISHA FELIX JUVE

Juventus itamuuza mshambuliaji wa kimataifa wa Argentina, Paulo Dybala, 25, ili kufikisha kiasi cha pauni milioni 86.4, kuweza kuifuata huduma ya Mreno wa Benfica, Joao Felix, 19. Hiyo ni kutoka na Rais wa Benfica, Luis Filipe Vieira kukataa pauni milioni 65 kutoka kwa miamba hiyo ya Italia. ***(Tuttosport via Football Italia)***

### KUBO AZIGONGANISHA BARCA, REAL

KLABU ya Real Madrid na Barcelona zitapambana uso kwa uso katika kuisaka saini ya kiungo wa FC Tokyo, Mjapan Takefusa Kubo, 17. ***(Marca - in Spanish)***

### KOULIBALY AWINDWA OLD TRAFFORD

MANCHESTER United inampigia hesabu beki wa Napoli, Kalidou Koulibaly, 27. Msenegal huyo anathaminishwa na pauni milioni 110. ***(Sunday Express)***

### KOCHA GENESIO KUITEMA LYON

KOCHA wa Lyon, Bruno Genesio, ataachana na klabu hiyo mwishoni mwa msimu. ***(RMC Sport - in French)***

### MIAZGA KUFUNGA ATAKAPOTUA

BEKI wa Chelsea, Mmarekani Matt Miazga, 23, amesema ataweka wazi mustakabali wake baada ya mkataba wake na Reading kumalizika mwishoni mwa msimu. ***(The Reading Chronicle)***



## HABARI MICHEZO

# STARS KUJIPIMA NGUVU NA MISRI, CAMEROON

Na Somoe Ng'itu

BAADA ya droo ya fainali za Mataifa ya Afrika mwaka huu (Afcon 2019) kupangwa, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limesema linajipanga kusaka mechi za kirafiki dhidi ya Misri na Cameroon ili kukiimarisha kikosi cha Timu ya Taifa (Taifa Stars).

Taifa Stars ambayo imefuzu kwa mara ya pili katika historia ya michuano hiyo itakayofanyika Misri kuanzia Juni 21 hadi Julai 13, mwaka huu, imepangwa Kundi C pamoja na Algeria, Senegal na Kenya.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa TFF, Wilfred Kidao, alisema endapo Taifa Stars itapata mechi mbili za kirafiki dhidi ya timu ya Afrika Magharibi na Kati, itasaidia kuwajenga wachezaji wao na kwenda katika michuano hiyo wakiwa wameiva.

Kidao alisema watakaa pamoja na benchi la ufundi ili kuhakikisha kila jambo litakalopendekezwa liweze kutimia kwa sababu wanataka kwenda Misri kushindana na si kushiriki.

"Tumepangwa na Senegal, maana yake tukipata mchezo na timu kama Cameroon itakuwa bora sana kwetu na kuhusu Algeria itakuwa vema tukijipima na nchi kama Misri, Kenya ni majirani zetu na mara kadhaa wachezaji wetu wamekuwa wanakutana katika mashindano tofauti ya ukanda huu," alisema Kidao.

Aliongeza kuwa wanatarajia kuona nguvu na kasi iliyotumika katika kusaka nafasi ya kushiriki fainali hizo inaendelea na kuipa heshima bendera ya Tanzania.

"Naamini tutaenda Misri katika mashindano hayo tukiwa katika ubora, tunazidi kushukuru kuwa ushirikiano tunaoupata kutoka kwa wadhamini, wadau na serikali yetu ni mzuri, naamini tutakuwa washindani katika fainali hizo," Kidao aliongeza.

Katika fainali hizo, Taifa Stars itatupa karata yake ya kwanza Juni 23 kwa kuwavaa Senegal, mchezo utakaochezwa kwenye Uwanja wa Cairo.




Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa, Tarimba Abbas (kulia), akimkabidhi mfano wa hundi, Hassani Thabiti, mkazi wa Mtwara mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, baada ya kupatia ubashiri wa mechi 12 kati ya 13. **PICHA: SPORTPESA**

# Dereva bodaboda aamka na mil. 37 za SportPesa

Na Mwandishi Wetu

KWA mara nyingine tena, Jackpot ya SportPesa imeendelea kuwanufaisha Watanzania wiki hadi wiki, huku washindi wakiendelea kumiminika kutoka kila kona ya Tanzania.

Wakati Jackpot hiyo kwa sasa ikifikisha Sh. milioni 597.8 ambapo unaweza kushinda kwa Sh. 2000/= tu endapo utapatia mechi zote 13 kwa usahihi katika ubashiri wako, wengi wameendelea kujishindia bonasi kila wiki kwa kupatia kuanzia mechi 10, 11 na 12. Na wiki hii imekuwa nzuri sana kwa Hassani Thabiti baada ya kubashiri na kupatia mechi 12 kati ya 13 na kujinyakulia bonasi ya Sh. milioni 37.9.

Akizungumza na waandishi wa habari, Hassani ambaye ni mkazi wa Tandahimba mkoani Mtwara, alisema ushindi huo ni kutokata tamaa na kuamini ipo siku atashinda.

"Nilivutiwa sana kucheza na SportPesa nilivyoona tangazo la Jackpot ya milioni 500 na pia nilivutiwa na jinsi SportPesa walivyokuwa wana masoko mengi.

"Matarajio yangu baada ya ushindi huu ni kuendeleza ujenzi wa nyumba yangu na kuongeza kipato kwenye biashara yangu ya bodaboda, kwa kweli SportPesa imebadilisha maisha yangu," alisema Hassani ambaye ni dereva bodaboda, huku akielezea furaha yake ya ushindi baada ya kupatiwa ujumbe wa ushindi Jumapili Aprili 7, mwaka huu.

Kwa upande wa SportPesa, Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa kampuni hiyo, Tarimba Abbas, alianza kwa kumpongeza Hassani kwa kucheza na kutokata tamaa na hatimaye kuibuka na ushindi wa kiasi cha Sh. millioni 37.9.

"Tunapata faraja sana kuona jinsi huduma zetu zinawafikia watu walioko sehemu mbalimbali nchini na kubadili maisha yao hasa kwenye sekta ya kiuchumi nikimaanisha kuwawezesha kukuza mitaji yao na kujiendeleza kifamilia," alisema.

Hata wewe unaweza kuibuka mshindi wa Sh. milioni 597.8 wikiendi hii. Bofya *150*87# au tembelea www.sportpesa.co.tz kucheza Jackpot ya SportPesa uwe milionea kama Hassani Issa Thabiti.

## Zimamoto yazima moto wa KVZ

Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR

MAAFANDE wa timu ya Zimamoto wamefanikiwa kupanda hadi nafasi ya pili wakitokea nafasi ya tatu baada ya hapo juzi kuibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya vinara wa ligi hiyo Maafande wa KVZ.

Zimamoto baada ya ushindi huo imefikisha alama 69, huku vinara wa ligi hiyo KVZ wenyewe wakiwa na pointi 70.

Mchezo huo uliopigwa katika dimba la Amaan majira ya saa nane mchana huku ukihudhuliwa na mashabiki wachache, mabao ya Zimamoto yalipachikwa na wachezaji Mustafa Muhsini dakika ya 32, Ibrahim Mohmed dakika ya 58, Amejabir dakika ya 75 na bao la nne likifungwa na Hakim Khamis dakika ya 89 kwa mkwaju wa Penalti baada ya kufanyiwa madhambi katika eneo la hatari. Maafande wa KVZ wenyewe walipata bao la kufutia machozi kupitia kwa Saleh Ali dakika ya 41.

Mchezo mwingine ambao uliopigwa katika uwanja huo majira ya saa kumi alasiri, ulizikutanisha timu ya maafande wa Polisi na timu ya Mlandege, huku maafande hao wakikubali kichapo cha bao 1-0 lililofungwa na Ibrahim Ally katika dakika ya 21, kwa matokeo hayo Mlandege imefikisha alama 66 na kujiweka katika nafasi ya tano ikitokea nafasi ya saba, huku Polisi wenyewe wakiendelea kusota katika nafasi ya tisa na alama zake 46.

## Kampuni zatakiwa kuiga Ligi ya Alaf

Na Mary Geofrey

OFISA Utamaduni wa Manispaa ya Temeke, Daima Mwangati, amezitaka kampuni mbalimbali kuanzisha ligi za michezo ili kuwajengea afya wafanyakazi wake ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono juhudi za Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, katika kuhamasisha mazoezi sehemu ya kazi.

Mwangati aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati akizindua ligi kwa wafanyakazi wa Kampuni ya uzalishaji Mabati ya Alaf. Alisema kampuni ya Alaf imefanya jambo nzuri na ligi iliyozunduliwa ni kwa ajili ya kuleta umoja kati ya wafanyakazi pamoja na kuimarisha afya zao. "Lengo ni kuwafanya wafanyakazi wafanye mazoezi na kuunga mkono juhudi za Makamu wa Rais ambaye amekuwa akisisitiza wafanyakazi kufanya mazoezi, hivyo hili lililofanywa na Alaf ni kitu kizuri na mimi naungana nao," alisema.

Naye Meneja wa Masoko wa Kampuni ya Alaf, Isamba Kasaka, alisema kuanzishwa kwa ligi hiyo ni kutoa motisha kwa wafanyakazi, kuongeza umoja na kuimarisha afya za wafanyakazi. Alisema ligi hiyo iliyoanza rasmi Aprili 13, mwaka huu, kilele chake kitakuwa Oktoba 10, ambapo mshindi ataibuka na Sh. milioni 3.5, huku mshindi wa pili akizawadiwa Sh. milioni 2.5 na wa tatu Sh. milioni 1.8.

Alisema timu zipo sita katika idara ya mabomba ya chuma na waya, mabati na rangi, mazingira, utayarishaji na idara ya viwango.

Michezo
Jumatatu Aprili 15, 2019
Nipashe



Guardiola: Kabla sijafa nitafanya kazi nyingine
HABARI UK 30



Wachezaji wa Serengeti Boys wakishangilia moja ya mabao yao kwenye mechi ya ufunguzi ya michuano ya Afcon U-17 dhidi ya Nigeria iliyopigwa Uwanja wa Taifa jana na wenyeji hao kufungwa 5-4. **MPIGAPICHA WETU**

# AUSSEMS AFUNGUKA KIPIGO TP MAZEMBE

## Kagere atoa yake, Makonda amwandalia zawadi Manula kuokoa michomo, waifuata Coastal Union huku...

**Na Somoe Ng'itu**

BAADA ya kutolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems, wachezaji pamoja na wanachama wa klabu hiyo wamesema watajipanga kufanya vema zaidi katika michuano hiyo hapo mwakani.

Simba imeiaga michuano hiyo baada ya kufungwa ugenini mabao 4-1 na wenyeji TP Mazembe katika mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Afrika uliochezwa juzi usiku kwenye Uwanja wa Lubumbashi.

Aussems aliliambia Nipashe jana kuwa timu yake ilistahili kusonga mbele katika mashindano hayo baada ya kuanza kupata bao la mapema lililofungwa na mshambuliaji Mganda Emmanuel Okwi, lakini hali ilikuwa tofauti. Mbelgiji huyo alisema wapinzani wao walijipanga na kupeleka mashambulizi ya mara kwa mara na hatimaye walifanikiwa kurejesha bao hilo na kufunga mengine matatu ambayo yaliwakatisha tamaa wachezaji wake.

"Haikuwa mipango yetu, lakini tulistahili kusonga mbele, kwangu kuingia hatua ya nane bora ilikuwa nafasi kubwa sana na wote tulikuwa na nafasi sawa, ila uzoefu na ubora wa vikosi vyetu ndio umechangia matokeo haya, naamini msimu ujao tutakuwa imara na bora zaidi," alisema Aussems.

Kocha huyo ambaye keshokutwa Jumatano atakuwa ugenini jijini Tanga kuivaa Coastal Union, aliongeza kuwa kikosi chake kinarejea Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo nayo ina changamoto kubwa ya kucheza mechi mfululizo.

**MANULA, KAGERE WAFUNGUKA**

Kipa chaguo la kwanza wa timu hiyo, Aishi Manula, alisema Simba ilikuwa na matarajio makubwa zaidi msimu huu, lakini hawana budi kumshukuru Mungu kwa hatua waliyoifikia katika mashindano hayo ya kimataifa.

Manula alisema hatua ya kucheza robo fainali kwao ni faraja na wataitumia kama hamasa ya kupambana kuhakikisha wanatetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara ili waweze kukata tiketi ya kushiriki tena michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika hapo mwakani.

"Tulikuwa na matarajio makubwa zaidi katika Ligi ya Mabingwa Afrika msimu huu, hapa tulipoishia inatupa nguvu ya kuanzia kwa wakati ujao, nguvu na jitihada zetu sasa tunazikita katika Ligi Kuu ili tupate tiketi ya kurudi tulipoishia leo (juzi), Mungu tubariki," alisema Manula, kipa wa zamani wa Azam FC.

Mshambuliaji Meddie Kagere, alisema kamwe hawawezi kukata tamaa na wanajipanga kufanya vizuri katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo zinawasubiri.

Kagere alisema soka ni mchezo wa furaha na maumivu, hivyo mashabiki wa Simba wanatakiwa kutulia na kusubiri mazuri watakayoyapata kwenye kutetea ubingwa wa Bara wanaoushikilia.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na shabiki wa Simba, Paul Makonda, alisema walichokifanya Wekundu wa Msimbazi msimu huu ni kikubwa na hasa pongezi zake zinakwenda zaidi kwa Manula.

Makonda alimweleza kipa huyo kuwa amemwandalia zawadi kutokana na kupangua "michomo" kadhaa iliyokuwa inapigwa na mastraika wa TP Mazembe hapo juzi.

# Serengeti Boys kufuzu bado kupo

**Na Somoe Ng'itu**

LICHA ya Timu ya Soka ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 17, Serengeti Boys, kuanza vibaya kampeni ya kuwania ubingwa wa Afrika (Afcon U-17 ) baada ya kukubali kufungwa na Nigeria mabao 5-4 katika mchezo wa ufunguzi wa michuano hiyo, uliochezwa jana kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, bado ina nafasi kubwa ya kufuzu Kombe la Dunia U-17 nchini Brazil.

Iliwachukua dakika 20 kwa yosso wa Nigeria kuandika bao la kwanza kupitia kwa Olatomi Olaniyani ambaye alimalizia pasi nzuri kutoka kwa Wisdom Ubani.

Hata hivyo, bao hilo lilidumu kwa dakika moja kwa wenyeji Serengeti Boys kusawazisha kupitia kwa Edmund John ambaye alifanikiwa kuwazidi mbinu walinzi wa Nigeria na kupiga shuti lililomshinda kipa, Suleiman Shaibu kudaka.

Nigeria ambao walikuwa vizuri katika safu ya kiungo waliendelea kushambulia lango la Serengeti Boys na dakika ya 29 walifunga bao la pili kupitia kwa Ubani ambaye aliwahi kuunganisha mpira uliookolewa na kipa, Mwinyi Yahya.

Wageni hao waliendelea kufanya mashambulizi na dakika ya 36 walifunga bao la tatu kupitia kwa Akinkunmi Amoo. Kipindi cha pili kilianza kwa timu zote kucheza kwa kasi, lakini ni upande wa Serengeti Boys ndio walicharuka zaidi kwa kupata mabao ya haraka haraka na kuwarejesha mchezo.

Dakika ya 51, Kelvin John aliwaandikia Serengeti Boys bao la pili kwa shuti la mbali zaidi ya mita 50 baada ya kupokea pasi kutoka kwa Edson Mshirakandi. Nahodha Mourice John alifunga bao la nne kwa penalti dakika nne baadaye, wakati Edmund John akifunga la nne na kwa njia ya penalti tena.

Ubani alifanikiwa kuifungua Nigeria bao la nne kwa mpira wa faulo uliokwenda moja kwa moja wavuni kwa kupiga mtamba wa juu na kuingia wavuni. Wageni hao hawakukata tamaa kwa kuendelea kufanya mashambulizi na dakika ya 78 Ibrahim Jabaar aliyeingia kuchukua nafasi ya Olatomi alifungia Nigeria bao la tano.

Serengeti Boys sasa italazimika kushinda mechi zake mbili zijazo ikianza na ya keshokutwa Jumatano dhidi ya Uganda kabla ya kuhakikisha inahitimisha kwa kuifunga Angola mechi yake ya mwisho ya Kundi A.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002